**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Saba – Tarehe 22 Juni, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 58

**Vikao vya Kamati za Bunge Vifanyikie Zanzibar**

**MHE. ALI SAID SALIM** aliuliza:-

Kwa kuwa, Bunge letu ni la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na azma ya Serikali ni kudumisha Muungano:-

Je, Serikali itakubali sasa kwamba, baadhi ya Vikao vya Kamati za Kudumu za Bunge vifanyike Tanzania Zanzibar badala ya Vikao hivyo kufanyika Dar es Salaam wakati wote?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. LUKA J. SIYAME)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 88(3) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004 zinazotumika hivi sasa, inatamkwa wazi kwamba Kamati za Kudumu za Bunge zitakutana kila zinapoitishwa ama na Mheshimiwa Spika au Mwenyekiti wake baada ya kupata idhini ya Spika. Aidha, Mikutano yote rasmi ya Kamati hizo imepangiwa kufanyika ama Mjini Dodoma au Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba Bunge letu lina Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na azma yake ni kudumisha Muungano. Hivyo basi, Serikali haina kipingamizi kuhusu baadhi ya Vikao vya Kamati za Kudumu za Bunge kukutana Zanzibar. Na inasisitiza kwamba kinachohitajika ni kwa Bunge kufanya marejeo ya Kanuni ili azma hiyo iweze kutekelezeka. *(Makofi)*

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Kanuni za Bunge siyo Msahafu wala si Biblia na kwa kuwa wakati huu tuko katika pilika pilika za kubadilisha Kanuni zenyewe. Sasa isingekuwa vyema tukachukua muda huu kubadilisha Kanuni ili baadhi ya Shughuli za Bunge zikafanyikie Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. LUKA J. SIYAME):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha kusema kwenye swali la msingi jibu ni kwamba kufuatana na Kanuni za Bunge pale ambapo suala litakuwa limejadiliwa na kukubalika basi Serikali haina kipingamizi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na shughuli kwenye *Speaker's Gallery* leo kuna wageni ambao wanawahusu Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo ya Mikumi, Kilombero na Mvomero. Wageni hao ni viongozi wa Vyama vya Wakulima wa Miwa kutoka Viwanda vya Sukari vya Kilombero na Mtibwa. Wanaongozwa na Mwenyekiti wao Dr. George Mlingwa. *(Makofi)*

Na. 59

***Mtwara Development Corridor* na *SADC***

**MHE. FATMA A. MIKIDADI** aliuliza:-

Kwa kuwa, mwaka 1997 nchi wanachama wa *SADC* zilikubaliana suala la uendelezaji wa Mpango Mzima wa Maendeleo ya Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (*Mtwara Development Corridor*), kwa lengo la kuondoa umaskini na kuendeleza biashara, uwekezaji na utalii katika nchi hizo wanachama na kwa kuwa ukanda huo ulihusisha Mikoa ya Rukwa, Iringa, Mbeya, Ruvuma, Mtwara, Lindi na maeneo ya Kaskazini ya Mto Rufiji katika Mikoa ya Pwani na Morogoro, na kwa kuwa tarehe 15 Desemba, 2004 Serikali iliweka saini Mkataba wa Kimataifa wa Nchi za *SADC* juu ya uendelezaji wa mradi huo Mtwara *Development Corridor'*:-

(a) Je, suala zima la *Mtwara Development Corridor* limeshapata ridhaa ya Bunge la Tanzania ili iwe sehemu ya sheria za nchi kwa utekelezaji?

(b) Je, kuna maelezo gani kuhusu mipango na mikakati thabiti ya utekelezaji wa miradi ya *MDC* ikiwa ni pamoja na programu ya kazi, Bajeti ya Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo hasa katika nyanja za Kilimo, Utalii, Miundombinu na Madini?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum, ningependa kwanza kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, juhudi za kuanzisha Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara, *(Mtwara Development Corridor (MDC)* zilianza tangu mwaka 1997 kutokana na uamuzi wa Wakuu wa nchi za Tanzania, Malawi, Msumbiji na Zambia wa kuongeza kasi ya maendeleo katika maeneo hayo kwa kushirikiana katika kuanzisha miradi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii katika nchi zote wanachama.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeiteua Wizara ya Miundombinu kuongoza Mradi huu na pia imelipa Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)* jukumu la kusimamia utekelezaji wa mradi huu na kutafuta wawekezaji wa miradi iliyopo kwenye Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara. Aidha, mradi huo umefanikiwa kupata Meneja Mradi ambaye ni Mratibu wa Shughuli za kila siku zinazohusu Mtwara *Development Corridor* kwa nchi zote. Mtaalamu huyu ameajiriwa kupitia msaada wa Serikali ya Afrika Kusini (Wizara ya Viwanda na Biashara) na alianza kazi tangu Machi, 2003. Baada ya kutoa maelezo hayo, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mkataba wa makubaliano ulitiwa saini na Wakuu wa Nchi wanachama tarehe 15 Desemba, 2004 huko Lilongwe Malawi. Wizara ya Miundombinu inawasiliana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili makubaliano hayo yaweze kuridhiwa na Bunge letu.

(b) Mheshimiwa Spika, kazi ya kuainisha maeneo na mipango katika maeneo ya Kilimo, Utalii, Miundombinu na Madini imekamilika. Meneja Mradi amekwisha andaa programu akishirikiana na Taasisi husika katika kila nchi katika kupanga malengo, mategemeo na namna ya kufikia malengo hayo.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa mradi huu wa Mtwara *Corridor* si Mtwara tu na Lindi peke yake upo katika sehemu ya Mkoa Rukwa, Iringa, Mbeya, Ruvuma, Mtwara, Lindi na maeneo ya Kaskazini ya Mto Rufiji katika Mikoa ya Pwani na Morogoro.

(a) Sasa ningependa kujua ni miradi ipi ambayo imepewa kipaumbele katika programu hii ya Mtwara *corridor?*

(b) La pili, daraja la umoja ni mojawapo katika Mtwara *Corridor* sasa limefikia hatua gani?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko na kwa niaba ya Wizara yangu mwenyewe maana Wizara yangu ndiyo Mwenyekiti wa Mpango wa *Mtwara Corridor*.

Ningependa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fatma Mikidadi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nia ya *Mtwara Corridor* kama swali la msingi lilivyosema ni kuendeleza utalii. Kwa hiyo, jambo la msingi kabisa kwanza, ni kusawazisha njia za kupitia watalii na kuwezesha watalii wenyewe kwenda kwenye maeneo yaliyopangwa. Kwa hiyo, kazi ya kwanza kabisa tunayofanya ni ya miundombinu kwa maana ya njia za barabara na ndiyo maana hapa tumekuwa tukisikia na tutaendelea. Nitakapozungumza wakati wa Bajeti yangu juu ya barabara zinazounganisha Dar es Salaam,Lindi na Mtwara, Mtwara-Masasi-Tunduru-Songea hadi *Mbambabay* ambazo tayari utekelezaji wake unaanza kwa hatua mbalimbali kama nitakavyoueleza baadaye.

La pili, tunashughulikia uboreshaji wa usafiri wa ndege kwa sababu watalii wanasafiri sana kwa ndege. Kwa hiyo, hivi karibuni ndege zinaweza sasa zikatua Lindi jambo ambalo lilikuwa haliwezekani na zikatua mara nyingi kule Mtwara. Na tuna mpango wa kuboresha kiwanja cha ndege cha Mtwara na kuangalia uwezekano wa ndege kuweza kutua Nachingwea na vilevile kuunganisha na Songea na Mkoa wa Mbeya kama ilivyo kwenye kiwanja cha ndege ambacho kinajengwa kule Sogwe na vilevile kuunganisha Mkoa wa Iringa kwa ndege ili kuweko mzunguko wa njia za ndege.

Mheshimiwa Spika, tuna mpango vilevile ambao uko pia kwenye Ilani ya Uchaguzi kurejea upya uwezekano wa kuanzisha reli ambayo ilikuwa imefutwa. Kufufua na kwenda kwa kasi zaidi na mpango wa kuanzisha mgodi wa Mchuchuma ambao umeundiwa Kamati na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, Wizara ya Miundombinu na Wizara ya Nishati na Madini. Tuna Kamati ya Mawaziri ambayo tunashughulikia kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi nataka niseme kwamba jambo hilo tunalifahamu na ninalielewa pia kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii yenyewe ina mpango wa kuboresha Utalii kwa ajili ya Mikoa ya Kusini baada ya mambo yangu hayo yote kukamilika. Kwa hiyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Fatma na Waheshimiwa Wabunge hao wa Mikoa husika kwamba jambo hili tunalipa kipaumbele kikubwa ndani ya Serikali na tutazidi kuomba Mungu kwamba tukijaliwa tutafanikiwa na *Mtwara Corridor* itakuwa ni ya halali.

Mwisho kabisa, daraja la umoja tayari lile linatengenezwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Tanzania na Msumbiji na kuna mpango wa kuunganisha daraja hilo kilomita 60 katika Wilaya ya Masasi ili ndani ya miaka mitano ijayo kuweko barabara na daraja la kutuunganisha sisi na Msumbiji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Pamoja na majibu marefu sana bado kuna swali la nyongeza Mheshimiwa Devota Likokola.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, naomba kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa wananchi wengi wa Mikoa hii ya Kusini hawaelewi vizuri mpango huu wa Mtwara *Corridor*. Je, Serikali ipo tayari kuanzisha programu maalum ya kuwaelimisha wananchi ili waweze kushiriki katika kuelewa na kutekeleza miradi ya mpango huu wa *Mtwara Corridor*?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo, ndiyo.

Na. 60

**Umiliki wa Nyumba za Msajili**

**MHE. MUSSA A. ZUNGU** aliuliza:-

Kwa kuwa, Nyumba za Msajili sasa zinaendeshwa na Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC);* na kwa kuwa, katika nchi nyingi, nyumba kama hizo hutambulika kama *Council Houses* na hutolewa kwa Halmashauri za Miji/Wilaya kuziendesha na kwa lengo la kuzipatia Halmashauri hizo mapato na kuzipa uwezo wa kuwapelekea huduma nzuri wananchi: Je, Serikali haioni kuwa sasa wakati umefika wa kuzipa Halmashauri za Miji/Wilaya nyumba hizo ziendeshe?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haina mpango wa kuzipatia Halmashauri za Miji na Wilaya nyumba zilizokuwa chini ya Msajili wa Majumba kwa kuwa utaratibu unaotumika kwa sasa unalenga kuwanufaisha Watanzania wote. Nyumba hizo zilitaifishwa chini ya Sheria ya Utaifishaji wa Majumba Na.13 ya Mwaka 1971.

Aidha, kutokana na kutungwa kwa Sheria Na.2 ya Mwaka 1990 iliyounda upya Shirika la Nyumba la Taifa, Sheria ya Msajili wa Majumba ilifutwa na dhamana ya umiliki wa nyumba hizo uliwekwa kuwa chini ya Shirika la Nyumba la Taifa. Katika kipindi hicho, miliki ya nyumba 5,759 zikiwemo zilizokuwa chini ya Shirika la Nyumba zilihamishiwa kwenye Halmashauri za Miji na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, maamuzi ya baadhi ya nyumba kuendelea kumilikiwa na Shirika la Nyumba ulichukuliwa ili kuwezesha mapato yanayopatikana yaweze kuwanufaisha Watanzania walio wengi. Mapato ya kodi za pango kutoka kwenye nyumba hizi yanatofautiana kati ya Mji na Mji. Maeneo yenye mapato kidogo, hupata ruzuku kutoka kwenye maeneo yenye mapato makubwa. Lengo la utaratibu huu ni

kuitunza rasilimali nyumba katika maeneo hayo na kujenga nyumba sehemu zingine. Halmashauri zenye majengo ya Shirika zinanufaika na malipo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kodi za majengo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000, Halmashauri za Miji na Wilaya ni baadhi ya wadau muhimu wa makazi nchini. Sera inazishauri Halmashauri za Miji na Wilaya kujihusisha na uwekezaji wa sekta binafsi kujenga nyumba za makazi. Aidha, zinapokuwa na uwezo kifedha zinayo nafasi ya kujenga nyumba za kupangisha au kuuza kwa ajili ya wakazi wake.

Hivyo, nazishauri Halmashauri hizo kuzingatia Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 badala ya kuendelea kutegemea kupewa nyumba za *NHC.*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

La kwanza, je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kuwa Shirika la Nyumba sasa hivi limepoteza mwelekeo wa kuwajengea nyumba Watanzania wenye kipato cha chini?

La pili, watakapozinduka na mwelekeo huo je, wanaweka mikakati gani ya kuzuia wenye uwezo kutokuingia kuzichukua nyumba kama hizo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Shirika halijapoteza mwelekeo wa kujenga nyumba au kuhakikisha kwamba nyumba ziko kwa ajili ya watu wenye kipato cha chini. Kwa sababu katika jibu langu la msingi nimesema kuwa Shirika lilitoa nyumba 5,700 kwa Halmashauri za Miji ili ziwezeshe watu walio na kipato cha chini. Lakini tunasikitika mpaka sasa hivi Halmashauri hazikufanya tulivyotegemea. Mheshimiwa Mbunge ni shahidi yangu ambaye anatoka katika Mkoa wa Dar es Salaam. Kuna nyumba nyingi sana pale Magomeni na nyumba nyingine ziko Shaurimoyo, Ukonga na Ilala na mpaka sasa hivi bado zimebaki ndogo kama zilivyoachwa na *National Housing.* Vilevile napenda kuongeza kuwa Shirika linajenga nyumba kama Dar es Salaam limejenga nyumba 331 zilizoko Boko, Mbweni na katika maeneo kadhaa kama Tambata ambazo zote ni kwa ajili ya watu wenye kipato cha chini.

Tunajaribu kuhakikisha kwamba wale ambao wana uwezo wasije wakazing'ang'ania nyumba za *National Housing*. Tuna Mpango wa kujenga nyumba za *National Housing* kwa ubia baina ya Shirika na mtu binafsi. Nina hakika tuna nia ya kubadilisha Miji yetu mtu mwenye uwezo ndiyo anaweza akajenga ghorofa pale. Kwa hiyo, kwa upande huo pia tunatekeleza Sheria za Makazi kwa kuwezesha wenye uwezo kujenga nyumba kwa ajili ya wasio na uwezo.

**MHE. ANIA SAID CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri. Kwa kuwa nyumba za Msajili wa Majumba ni nyumba ambazo zimetaifishwa kutoka kwa wananchi wakati Serikali ilikuwa inahitaji msaada wa kupata fedha za kuendesha

nchi kwa wakati huo miaka 25 au 30 ya nyuma. Je, Serikali haioni kwamba wananchi ambao walitaifishiwa majumba yao miaka hiyo wana hakika ya kuangaliwa angalau kuwapa fidia au kuwarudishia majengo yao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, Serikali haikutaifisha hizo nyumba mwaka 1971 kwa ajili ya kupata fedha za kuendeshea nchi. Ilitaifisha nyumba hizo kwa manufaa ya Watanzania walio wengi.

La pili, kuna watu katika wale ambao nyumba zao zilichukuliwa wengine waliondoka nchini moja kwa moja na waliokuwepo walilipwa fidia. Hata miaka ya karibuni kuna watu wamelipwa fidia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaita muulizaji wa swali linalofuata. Nina tangazo hapa kwamba Waheshimiwa Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kuna Mkutano muhimu leo Saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa zamani wa Bunge. Ahsanteni sana.

La pili, inabidi nisimame kwa sababu hili ni la Kanuni. Namwomba Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, atoke nje akavue kofia, kwa sababu hairuhusiwi katika vazi la Bunge. Mheshimiwa Mbunge ukishaivua hiyo kofia unaweza kurejea hukutolewa moja kwa moja. *(Makofi)*

Na. 61

**Uwanja wa Ndege wa *KIA***

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA (k.n.y. MHE. KABWE Z. ZITTO)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imekodisha Uwanja wa Ndege wa *K.I.A* kwa muda wa miaka thelathini (30) kwa gharama ya dola za Kimarekani 1000 kwa mwaka:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kuuleta Mkataba wa makubaliano ya kukodisha uwanja huo hapa Bungeni ili Wabunge waweze kuufahamu?

(b) Je, Serikali ipo tayari kuupitia upya Mkataba huo ili nchi ifaidike na mapato ya uwanja huo ambao ulijengwa kwa gharama kubwa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro *(KIA)* umekodishwa kwa Kampuni ya *Kilimanjaro Airports Development Company* (*KADCO)* kwa Mkataba wa miaka 25 na sio 30. Katika ukodishaji huo Serikali ni mmoja wa wabia na ina hisa asilimia 24. Katika Mkataba huo kipo kipengele 30.4 ambacho kinatufunga pande zote mbili zinazoingia Mkataba huo kutoa habari kwa mtu yeyote ambaye si mhusika wa moja kwa moja na utekelezaji wa Mkataba huo.

Mheshimiwa Spika, mkodishaji ameweza kufanya mambo mbalimbali ya kuboresha kiwanja hicho ikiwa ni kulipia mkopo uliochukuliwa na Serikali, kufanyia matengenezo magari ya zimamoto na ukarabati wa Kituo cha Zimamoto, ukarabati wa paa ambalo lilikuwa linavuja, upakaji rangi majengo ya abiria, ukarabati a vyumba vya kufikia abiria na chumba maarufu, ujenzi wa barabara ya kutoka *BP Fuel Farm* hadi *DAHACO,* ununuzi na kujenga mitambo mbalimbali ya kuongozea ndege, misaada kwa taasisi za kidini, shule na afya na elimu kwa wafanyakazi na uboreshaji wa shughuli za mazingira. Jumla ya Shs.8,772,896,600/= zilitolewa na *KADCO* kwa kazi hizo. Wizara yangu imeona umuhimu wa kuupitia upya mkataba huo kipengele kwa kipengele kazi ambayo ilianza na bado inaendelea, shughuli hii inafanywa na jopo la wataalamu kutoka Wizara zifuatazo:- Wizara ya Fedha, Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Miundombinu, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha na Kilimanjaro. Tunategemea baada ya pande mbili kufikia muafaka, marekebisho hayo yatafikishwa katika ngazi za juu Serikalini kwa maelekezo zaidi.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, nataka kujua kama Naibu Waziri alivyosema Mkataba hauruhusu taarifa zitolewe. Lakini kama tunavyojua uwanja wa ndege ni mali ya Watanzania. Je, ni sahihi kwa mkataba wowote unaonyima taarifa kwa wenye mali wenyewe ambao ni wananchi wa nchi hiyo?

Mheshimiwa Spika, la pili, kuna taarifa kwamba sasa mazungumzo yanaendelea kuongeza muda wa Mkataba kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri. Je, Bunge hili kupitia Kamati yake itapata fursa ya kupitia Mkataba huo kwa sababu kwa muda mrefu mkataba huo umeleta manung’uniko kutoka kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, napenda nimfahamishe Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, kama makubaliano katika Mikataba yote si huu tu wa *KADCO* ni kwamba siri zisitolewe kwa wananchi au kwa watu ambao hawahusiki moja kwa moja. Nadhani bado tutaendelea kuheshimu maamuzi hayo ya Mkataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, ni kweli mazungumzo yanaendelea. Lakini napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itapata nafasi ya kupitia Mkataba huo kwa niaba ya Bunge hili ipasavyo.

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheeshimiwa Spika, kwanza ningependa nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Ningependa kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa katika miaka ya nyuma Serikali ilijenga karakana kubwa sana pale *KIA* na karakana hiyo ilikuwa ni kwa sababu ya kuweza kuhudumia utengenezaji wa ndege na ukarabati ndege mbalimbali. Je, katika mikataba hiyo inayoangaliwa hivi sasa uko uwezekano wa suala la karakana hii kuweza kutumika kama ilivyokuwa madhumuni wakati ikijengwa? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa John Samwel Malecela, kama ifuatavyo: Tutazingatia ushauri wake. *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali linalofuata ni la Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda kwa Wizara hiyo hiyo. Kwa bahati mbaya Dr. Samson Mpanda mwenzetu amelala hospitalini nadhani wote tutamkumbuka na kumtakia afueni. Lakini namwita Mheshimiwa Raynald Mrope aulize kwa niaba ya Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda.

Na. 62

**Ujenzi wa Barabara ya Njia Nne hadi Kipatimu**

**MHE. RAYNALD A. MROPE (k.n.y. MHE. DR. SAMSON F. MPANDA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali kupitia Wakala wa Barabara *TANROAD* imeamua kujenga barabara yenye njia nne hadi Kipatimu katika Jimbo la Kilwa Kaskazini na kwa kuwa, barabara hiyo yenye urefu wa takriban km.52 itajengwa kwa kiwango cha changarawe na hatua za kwanza za ujenzi kwa maana ya kuweka alama ya X kwenye majengo na mazao yatakayoondolewa imeshafanyika:-

(a) Je, ujenzi huo utaanza lini?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa fidia kwa watakaobomolewa nyumba zao na mazao?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Samson Ferdinand Mpanda, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Barabara ya Tingi (Njia Nne) hadi Kipatimu yenye urefu wa kilometa 52 ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Mkoa wa Lindi. Sehemu ya barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 21 itafanyiwa ukarabati

kwa kiwango cha changarawe kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Nchi zinazotoa Mafuta kwa wingi Duniani *(OPEC)* na Serikali ya Tanzania kwa gharama inayokadiriwa kufikia shilingi 1,133,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Samson Ferdinand Mpanda, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ujenzi wa barabara hiyo, unatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi huu wa Juni, 2006.

(b) Kama ilivyo katika miradi mingine ya ujenzi wa barabara na sheria zinazolinda hifadhi ya barabara, Serikali huwa haitatoa fidia kwa nyumba na mazao yaliyoko ndani ya hifadhi ya barabara.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu yaliyotolewa na Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, je Waziri atawaeleza nini wananchi wa Nangurukuru mpaka Mbwemkuru katika jimbo hili la Kilwa Kaskazini ambao hawajalipwa mpaka sasa fidia na katika hili umaskini ndio umetawala zaidi je, Waziri anasema nini juu ya hili?

Swali la pili, katika ujenzi uliochelewa sana wa barabara ya Kibiti/Lindi wananchi wengi walikuwa wamejenga karibu na barabara. Sasa hivi barabara hiyo ndiyo inajengwa upya. Je, ni halali kwa *TANROADS* kuweka alama za X katika nyumba za wananchi hawa ambao kwa muda mrefu kwa kweli hawakutegemea hata kama barabara hiyo itapita katika maeneo yao?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Miundombinu kwa kweli kinachofanyika ni kutekeleza sheria na sheria inavyosema ni kwamba nyumba au mazao ambayo yako kwenye hifadhi ya barabara hayatalipwa fidia. Lakini Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekuwa inaangalia vile vile hali halisi ya wananchi ambao wako katika maeneo hayo. Ndiyo maana mwaka juzi Wizara ilitoa tamko kwamba kwa maeneo ambayo yako kwenye hifadhi au maeneo ya barabara. lakini kwa wakati huo Serikali haina mpango wa kuyaendeleza maeneo hayo, wananchi wa maeneo hayo hawatabomolewa ingawaje zile X zitakuwepo kuonyesha kwamba ni hifadhi ya barabara na wasifanye maendelezo zaidi. Lakini mpaka pale ambapo Serikali itakuwa na mpango wa kuhudumia maeneo hayo au kuyaendeleza ndipo ubomoaji utafanyika na utafanyika baada ya kutoa notisi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kinachomwondoa mtu kwa kweli ni notisi ile ya miezi mitatu au sita lakini kuweka X ni kuonyesha tu kwamba hilo ni eneo la hifadhi ya barabara haitakiwi ukae hapo na uanze taratibu za kuhama. Lakini Wizara yangu inadhani kwamba kuna haja kuangalia sheria hii vile vile kwa maana ya kuangalia matatizo ambayo wananchi wanapata ili kwenda na ukweli au mazingira halisi. Kwa mfano kama wananchi walihamishiwa maeneo hayo katika ule mpango wa kuhamisha

wananchi kwa ajili ya vijiji vya ujamaa na wakawekwa eneo fulani na baada ya kuonekana kwamba eneo hilo ni hifadhi ya barabara waliletwa pale kihalali, Serikali kwa kutumia mazingira hayo inaweza kufikiria. Kwa hiyo kwa kweli haya mambo nadhani yatategemea sana mazingira yaliyopo wakati huo huo tukiheshimu sheria za nchi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nalazimika kutoa ufafanuzi kuhusu uamuzi wangu wa kumtoa kwa muda Mhe. Amina Chifupa Mpakanjia, chini ya Kanuni ya 74.

"Kofia kwa Mbunge mwanamke inaruhusiwa tu ikiwa amevaa na *gloves*. Kanuni ya 74 inasema hivi: "Vazi rasmi kwa Wabunge wanawake, fasili ya 3. Suti ya kiulaya ya kike ama ikiwa kamilifu pamoja na kofia na *gloves* au bila vitu hivyo"

Kwa kuwa Mheshimiwa hakuwa na *gloves* basi kwa mujibu hakuwa amekamilika. Ahsante sana. Wale wote walioniandikia waelewe hilo. Tunaendelea.

Na. 63

**Sekondari ya Kibakwe**

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE** aliuliza:-

Kwa kuwa, mfumo sasa wa elimu katika nchi yetu unataka wanafunzi wanaofaulu kuingia Kidato cha Kwanza, kwa asilimia kubwa wabaki katika Shule za Sekondari zilizopo katika Jimbo la Kibakwe zote ni za Kutwa na zipo katika mazingira ya vijijini ambako hakuna huduma kama umeme na nyumba bora za kupanga kwa ajili ya watumishi:-

(a) Je, Serikali haioni haja ya kuifanya Shule ya Sekondari ya Kibakwe ambayo tayari ina umeme kuwa ya Bweni ili wanafunzi kutoka sehemu mbalimbali za ndani na nje ya Jimbo hilo kusoma katika mazingira bora tofauti na jinsi wanavyokaa mitaani kwenye nyumba mbovu ambazo hazina mazingira yanayoweza kuwafanya wanafunzi kufanya vizuri katika masomo yao?

(b)Kwa kuwa, asilimia sabini (70%) ya wasichana katika Sekondari hizo hawamalizi masomo kwa sababu mbalimbali zikiwemo za kupewa mimba na kuolewa; na kwa kuwa, kumbukumbu zinaonyesha kuwa, na hata wanaobahatika kumaliza hawafanyi vizuri katika mitihani, na hivyo kukosekana kwa wanawake wasomi kwenye kwenye Jimbo la Kibakwe; Je, Serikali haioni haja ya kuteua Sekondari moja kati ya Sekondari kumi na moja zilizoko Kibakwe na kuifanya Sekondari ya Bweni kwa ajili ya wasichana pekee yao?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mpango wa Serikali katika Maendeleo ya Elimu ya Sekondari nchini, ni kuwepo Shule za Sekondari za Kutwa ili wanafunzi wakae nyumbani katika maeneo ambayo shule iliyopo inahudumia wanafunzi kutoka mbali, wananchi wanashauriwa kujenga *hostel*. Serikali huunga mkono jitihada za wananchi kadri ya uwezo wake katika ujenzi wa *hostel* hizo na kuwaachia wananchi kuziendesha. Aidha, suala la kuboresha mazingira ya shule ni wajibu wetu sote kwa kushirikiana na wananchi na Halmashauri ili tuwe na shule zenye mazingira bora yanayowezesha elimu bora kutolewa.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inajitahidi kutoa elimu sawa kwa watoto wote wa kike na wa kiume. Mdondoko (*drop out*) wa asilimia 70 kwa wasichana kutokana na taarifa za Mheshimiwa Mbunge ni mkubwa sana. Wizara yangu kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Dodoma, Ukaguzi Kanda ya Kati na Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, tumefuatilia taarifa hiyo na kubaini kuwa tatizo la utoro lipo kwa asilimia 29. *(Makofi)*

Aidha, tangu shule hiyo ianzishwe mwaka 1999 ni mimba nane tu zilizotambuliwa. Imebainika kuwa wanafunzi walio wengi wamehamia katika shule za Kata zao na kuifanya shule hiyo ya Kibakwe kubakiwa na wanafunzi wachache wa Kata hiyo na wale wa vitongoji vichache vya karibu tu. Hata hivyo kwa pamoja tumekubaliana kuwepo umuhimu wa kuwepo kwa *hostel*. Hivyo napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na wanafunzi wa Kibakwe kujenga hosteli ili kukabiliana na matatizo yao.

Kuhusu kuwa na shule ya wasichana pekee, Halmashauri inashauriwa kuleta maombi rasmi kwa Afisa Elimu Kiongozi, ili kuona uwezekano wa kubadili moja ya shule hizo kuwa ya Wasichana pekee.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hadi sasa takwimu zinaonyesha kwamba hakuna msichana aliyemaliza katika jimbo la Kibakwe ambaye ameweza kwenda Kidato cha Tano na hali inayotishia kwamba baada ya muda mrefu tutakuwa sisi hatuna wasomi wa Chuo Kikuu. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuwa na mpango wa dharura wa kuhakikisha kwamba hayo mabweni na mazingira kukaa *bording* kwa wasichana yanafanyika haraka? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nilisema kwamba uamuzi wa kujenga hosteli utatokana na wananchi wenyewe kutegemea na hali ya uzito wa tatizo katika Kata yao. Kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge amebaini hili namwomba yeye kwa kushirikiana na wananchi katika jimbo lake na hasa kwa Kata hiyo ya Kibakwe na Halmashauri yake waangalie sasa umuhimu na namna ya kuanza kujenga hosteli hizo na Serikali kama nilivyoahidi itachangia pale itakapojaliwa.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza. Kwanza napenda niwapongeze wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa kwa kujenga shule zaidi ya 18 za sekondari. Sasa swali?

Kwa kuwa hivi karibuni mwezi Aprili kuna Walimu zaidi ya 300 ambao wamefuzu katika Chuo cha Ualimu cha Mpwapwa. Na kwa kuwa shule hizo 18 zina upungufu mkubwa sana wa Walimu. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na ushauri wangu? Pamoja na kwamba Walimu hawa watapelekwa katika maeneo mengine. Je, Serikali iko tayari kutoa upendeleo angalau shule hizi zipate Walimu wa kutosha ili kuboresha elimu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumwarifu kwamba Wizara ya Elimu imeshatoa orodha na mgao wa Walimu kwa kila Mkoa. Na Mkoa wa Dodoma imepatiwa idadi kubwa sana ya Walimu.

Ni matarajio yangu kwamba Wabunge wote wa Mkoa wa Dodoma akiwepo Mheshimiwa Lubeleje washirikiane na Afisaelimu wa Mkoa Dodoma kuhakikisha kwamba ugawaji wa Walimu hao unagawanywa kutegemea na kuzingatia mahitaji ya kila eneo.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupewa nafasi hii naomba kuuliza swali kama ifuatavyo:-

Je, suala hili ambalo limeonyesha kwamba wanafunzi wengi wa kike wanaacha shule kwa sababu ya kupata mimba. Ningetaka kujua Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akatamka ni lini sheria kwamba watoto hawa wanapata elimu baada ya kujifungua italetwa lini hapa Bungeni? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, kupata mimba ukiwa shuleni ni utovu wa nidhamu, ni kukosa la maadili.

Pili, wanafunzi waliopata mimba wakiwa shuleni wanaweza kuendelea na mafunzo yao kwa mpango usio rasmi MUKEJA kama atakuwa amefikia umri wa miaka 19 na kuendelea, MEMKWA kama atakuwa ameondoka akiwa na uja uzito katika Shule ya Msingi. Pamoja na hayo Wizara ya Elimu ina Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima akimaliza kujifungua, akinyonyesha mwanawe akimwona ana afya njema anaweza akajiendeleza kupitia taasisi ya Elimu ya Watu Wazima.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu hayo tatizo la mimba linatoa kiashiria kibaya sana kwa Taifa letu. Naomba niseme kwamba Serikali kwa kushirikiana na *NGO* mbalimbali tunaandaa utaratibu wa kukaa pamoja kuona namna bora ya kutoa elimu kwa jamii ili kuweza kuwanusuru wanafunzi kwa jumla wasipate tatizo hilo tena.

Na. 64

**Gharama za Kusomesha Watoto Yatima**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa, baadhi ya Shule za Sekondari zinazomilikiwa na watu binafsi zimejitolea kusomesha watoto yatima na kwa kuwa, gharama ya kusomesha mtoto mmoja ni kubwa sana:-

(a) Je, Serikali itakuwa tayari kuzisaidia shule za aina hiyo kwa kuchangia gharama ndogo ndogo kama vile sare za watoto na fedha kidogo kwa matumizi ya watoto hao?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani za kudhibiti Shule/Taasisi zinazowatumia watoto yatima kama chombo cha kupatia misaada katika shule zao?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK MWANANZILA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kutoa maelezo yafuatayo kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2003 Serikali ilianzisha mpango maalum wa kuwalipia gharama za Elimu ya Sekondari watoto wanaotoka katika familia zenye vipato duni bila kulenga watoto yatima pekee. Watoto hao ni sharti wawe wamefaulu Mtihani wa Darasa la Saba (VII) na kuchaguliwa kuingia Shule za Sekondari ya Serikali. Lengo ni kuwasaidia watoto hao ambao hawana namna nyingine yoyote ya kupata Elimu ya Sekondari. Hata hivyo watoto hao ni wengi kuzidi uwezo wa Serikali. Hivi sasa Serikali inalipia gharama za Elimu ya Sekondari kwa jumla watoto 36,000 wa aina hiyo wa Kidato cha Kwanza hadi cha Nne.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, majibu ya sehemu (a) na (b) ni kama ifuatavyo:-

(a) Kwa mwaka wa fedha wa 2006/2007, Serikali kupitia MMES inaangalia uwezekano wa kutoa Ruzuku ya Uendeshaji kwa shule zisizo za Serikali ambazo haziendeshwi kibiashara na pia siyo Shule za Seminari kulingana na uwezo wa kifedha zitakazopatikana. Hata hivyo jukumu la kugharamia elimu ya watoto yatima ni letu sote. Naomba kutoa wito kwa Mashirika, watu binafsi na jamii kwa ujumla kuendelea

kuisaidia Serikali ili kuwawezesha vijana hao kupata elimu ya Sekondari. Aidha, nazipongeza shule zisizo za Serikali zinazojitolea kusomesha watoto hao katika shule zao. Nawaomba waendelee kuwasomesha vijana hao katika shule hizo, hadi watakapohitimu elimu hiyo ya Sekondari.

(b) Si jambo zuri kwa Taasisi/shule kuwatumia watoto yatima kama kitega uchumi cha kuombea misaada badala ya kuwasaidia watoto hao kupata elimu iliyokusudiwa. Endapo kuna Shule/Taasisi zinazowatumia watoto yatima kama chombo cha kupatia misaada; nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge pamoja na jamii yote tushirikiane kubaini Taasisi/shule hizo ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Kwanza namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake, lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

La kwanza, kwa sababu watoto hawa wengi ambao Serikali inawasomesha mpaka Kidato cha Nne baadhi yao hufaulu kwenda Kidato cha Tano. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuendelea kuwalipia ada mpaka wamalize Kidato cha Sita? Pili, kwa sababu matumizi ya shule ni makubwa zaidi kuliko ada yenyewe ambayo Serikali inawalipia. Nina mfano Mheshimiwa Spika, kuna binti mmoja jimboni kwangu ambaye alimaliza Kidato cha Nne na kufaulu kwenda Kidato cha Tano, Halmashauri ikakubali kumlipia ada lakini tulipopiga hesabu matumizi yalikuwa zaidi ya shilingi laki mbili na mimi kama Mbunge na Mbunge mwenzangu wa Jimbo la Mbozi Magharibi Dr. Siame tukachukua jukumu la kuchangisha wenzetu ili mtoto aweze kwenda shuleni. Je, Serikali inatamka nini kuwasaidia hawa watoto mbali ya ada, matumizi mengine ili wapate kusoma Kidato cha Tano na cha Sita? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK MWANANZILA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli wapo vijana ambao wanahudumiwa na Serikali kwa kulipiwa ambao idadi yao kama nilivyotaja katika jibu la msingi ni 36,000. Wapo pia wanaofaulu Kidato cha Tano kwenda Kidato cha Sita ambao wanahitaji msaada huu. Serikali italiangalia suala hili ili kuona ni jinsi gani ya kuweza kuwasaidia ili waweze kujiendeleza mpaka Kidato cha Sita. Suala la pili, matumizi ya watoto hawa wanaosoma katika Shule za Sekondari ni kweli ni makubwa. Lakini kwa sababu hili ni jukumu letu sote Mbunge alipochangia kusaidia vijana wale ambao walikuwa wameshindwa kusaidia Halmashauri hii ni sehemu ya wajibu wake kama Mbunge na Halmashauri pia inao wajibu na jamii yote ina wajibu ndiyo maana Serikali nayo ina wajibu ule wa kuwahudumia vijana mpaka 36,000. Naomba Halmashauri, nawaomba Waheshimiwa Wabunge naomba na jamii yote tushirikiane kwa sababu hili ni jukumu letu sote.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Nashukuru sana kupata nafasi ya kuuliza suala la nyongeza.Kwa sababu watoto yatima ni watoto wa Jamhuri yetu na katika nchi hii tuko viongozi wengi sana. Wabunge wote ni viongozi, Wakuu wa Mikoa ni viongozi, Wakuu wa Wilaya ni viongozi, je Serikali inaweza ikaleta mkakati gani kutuhusisha rasmi sisi ili na sisi tuweze kuchangia katika kuwasomesha hawa watoto yatima? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK MWANANZILA):** Ni kweli kabisa wapo viongozi wengi sana wa Serikali wa ngazi mbalimbali ambao tukiungana wote kwa pamoja kuweza kuchangia hawa watoto yatima ambao wanapata usumbufu tunaweza tukasaidia watoto wengi ambao ni tatizo la Kitaifa. Natoa wito kwa viongozi wote, natoa wito kwa Wabunge wote kila mmoja wetu ashiriki kadri ya uwezo wake kuchangia suala la watoto yatima hapa nchini.

Na. 65

**Ujenzi wa Mabwawa Makubwa Nchini**

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, uharibifu wa mazingira umechangia kwa kiwango kikubwa ukame ambao umeikumba nchi yetu; na kwa kuwa, kwa asilimia kubwa kilimo chetu kinategemea mvua, ambazo sasa ni haba:-

Je, Serikali haioni haja ya kujenga mabwawa makubwa mawili au matatu Kitaifa kama ilivyo kwa nchi za Zimbabwe, au Afrika Kusini ili kupunguza athari za ukame katika nchi yetu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Jimbo la Namtumbo, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Wizara yangu kwa miaka mingi imekuwa ikijenga mabwawa nchini kwa ajili ya matumizi mbalimbali kulingana na upatikanaji wa fedha. Mifano tuliyonayo ni Bwawa la Nyumba ya Mungu, Bwawa la Ning’hwa, Bwawa la Sigi, Bwawa la Igombe na Bwawa la Mindu. Yote haya yalijengwa kwa lengo la kupambana na tatizo la kupungua kwa maji katika vyanzo vyetu. Mabwawa mengine yamejengwa kwa ajili ya kupata nguvu za umeme. Hata hivyo, baadhi ya mabwawa yamebomoka ama kujaa tope kutokana na uharibifu wa mazingira na kutotunzwa na kusimamiwa vizuri. Hivyo, ili kukabiliana na ongezeko la mahitaji na matumizi ya maji katika sekta zote ikiwemo ya kilimo, Wizara yangu inao mkakati wa ujenzi na ukarabati wa mabwawa katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Kwa kutambua uzito wa tatizo la nchi kutokuwa na hifadhi ya maji ya kutosha, Serikali inakusudia kujenga mabwawa sio mawili au matatu kama alivyopendekeza Mheshimiwa Mbunge, bali kila inapowezekana kulingana na upatikanaji wa fedha mabwawa yatajengwa. Nchi yetu ni kubwa na ina maeneo yenye mazingira tofauti. Maeneo mengine ni makame zaidi kuliko mengine, na yanahitaji kufikiriwa kwanza.

Wizara yangu katika mwaka ujao wa fedha itafanya utafiti zaidi ili kutambua maeneo yanayofaa kwa ujenzi wa mabwawa. Mwaka huu Wizara yangu itaanza maandalizi ya ujenzi wa bwawa kwenye mto Ruvu, katika maeneo ya Kidunda Mkoani Morogoro, kwa ajili ya kuhudumia Jiji la Dar es Salaam, na maeneo ya Kibaha na Bagamoyo. Wizara inaendelea kufanya uchunguzi wa maeneo ya kujenga mabwawa katika maeneo mbalimbali hasa yale yenye ukame kama Singida, Tabora, Arusha, Shinyanga, Mara, Dodoma, Same na Manyara. Kiasi cha shilingi milioni 20 zimetengwa kwa ajili ya utafiti wa kubaini maeneo yanayofaa kwa ujenzi wa mabwawa, na shilingi bilioni 6.5 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa yenye ukubwa wa kati kwenye maeneo kame nchini. Kiasi hiki cha fedha hakitoshelezi mahitaji halisi, lakini huu ndio mwanzo wa kazi kubwa iliyo mbele yetu.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Lakini kabla sijauliza swali la nyongeza naomba kueleza yafuatayo. Kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge nimesimama wanasema bado sijasimama naomba niwataarifu kwamba nimenunua viatu vya aina ya *liason* ambavyo nikivaa nikisimama mtakuwa mnaniona. Nashukuru sana kwa majibu mazuri toka kwa Naibu Waziri. Naamini Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kuwa nchi yetu imebarikiwa utajiri mkubwa wa mito na maziwa makubwa.

Kwa kuwa wananchi wengi ni wakulima na wanatumia maji ya mpito ya mabondeni wakati wa kiangazi kwa kilimo cha umwagiliaji. Na kwa kuwa Serikali ina mpango thabiti wa kuhimiza kilimo cha umwagiliaji na kuna Sheria ya Matumizi ya Maji namba 42 ya mwaka 1974 ambayo imefanyiwa marekebisho mara tatu. Sheria namba 10 mwaka 1987, Sheria namba 17 mwaka 1989 na sheria namba 8 ya mwaka 1997 ya kutoa adhabu na mengineyo kwa wale wote watakaotumia maji bila ya kupata hati za haki ya kutumia maji kwa umwagiliaji mashamba, uzalishaji umeme.

**SPIKA:** Swali Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Je, Mheshimiwa Spika, Serikali inaweza kupitia upya Sheria hiyo ya Maji ili wakulima wetu wasije kuingia kwenye mtego huo wa sheria na kuadhibiwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, katika mapitio ya Sheria ya Maji namba 42 ya mwaka 1974 itaweka bayana ukamilishaji mahsusi ya vyanzo vyote vya maji. Matayarisho hayo yamekamilika na kwa hivi sasa iko tayari kupelekwa Bungeni ili kupitishwa Sheria.

Na. 66

**Ujenzi wa Mradi wa Maji Busanda**

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Maji ni muhimu kwa maisha ya binadamu; na kwa kuwa, Maji ya visima katika maeneo ya Geita si salama kutokana na madini yaliyoko ardhini:-

(a) Je, Serikali itakamilisha lini ujenzi wa miradi ya Maji ya Chankorongo, Nyakagomba hadi Katoro?

(b) Kwa kuwa, mradi huo ulianza mwaka 1976 lakini mpaka leo haujakamilika. Je, Serikali haioni kuwa ni aibu kuanzisha miradi ambayo ni sawa na kuwadanganya Wananchi kwa sababu haitekelezwi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faustine Kabuzi Rwilomba, Mbunge wa Jimbo la Busanda, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Rwilomba kwa mwaliko aliotupa wa kutembelea jimbo lake na pia ushirikiano aliotupa wakati tukizunguka pamoja katika jimbo lake. Mradi wa Maji wa Nyakagomba ulianza kujengwa mwaka 1973.

Chanzo cha maji cha mradi huu ni Ziwa Victoria. Kwa wakati huo, mradi ulikusudiwa kuwahudumia watu wapatao 4500, katika vijiji vya Kubuguzo, Chigunga, Chemamba, Nyakaswa, Chikobe, Nyakagomba, Nyasembe na Butundwe.

Mheshimiwa Spika, awali mradi huu ulifadhiliwa na Mamlaka ya Pamba *(TCA),* kabla haijakabidhi mradi huu Wizara ya Maji mwaka 1986/1987. Tangu wakati huo, Serikali ilianza kutoa fedha kuendeleza mradi huu.

Lakini bila mafanikio makubwa, kutokana na udhaifu katika usimamizi wa fedha za ujenzi wa mradi. Hivi karibuni, Naibu Waziri akifuatana na wataalamu wa Wizara yangu walitembelea mradi huu, na kubaini mapungufu mengi ya kiufundi, ambayo yanahitaji kufanyiwa marekebisho. Kabla ya kuendelea na ujenzi wa mradi wenyewe.

Mheshimiwa Spika baada ya hapo napenda kujibu swali (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Wizara yangu imepanga kuufanyia tathimini upya mradi huu katika mwaka wa fedha 2006/2007 ili kuainisha matatizo yaliyopo na hatua za kuchukua na gharama zake. Baada ya tathimini hiyo kwa kushirikiana na Halmashauri ya Geita ili kuweka mkakati wa kibajeti kila mwaka hadi mradi utakapokamilika pia tathimini itaangalia uwezekano wa kupanua mradi kulingana na ongezeko la watu wa vijiji husika pamoja na kufikia mji mdogo wa Katoro. Tathimini hiyo ndiyo itatoa muelekeo wa lini mradi huu utakamilika.

(b) Ni kweli Serikali ilianzisha mradi huo miaka ya 1970 ikiwa na nia njema ya kutoa huduma ya maji kwenye vijiji vilivyotajwa hapo juu katika Tarafa ya Butundwe hata hivyo kutokana na matatizo niliyoyataja hapo juu huduma haikuwafikia wananchi kama

ilivyokusudiwa. Kwa msingi huo Serikali haikuwa na makusudi wala sababu ya kuwadanganya wananchi. Aidha baada ya kukiri haliyojitokeza badala ya kuona aibu Serikali inachukua hatua za kiufundi na kibajeti ili kutimiza azma yake iliyokusudiwa wakati wa kuanzishwa mradi huo. Pamoja na hatua hizo namshauri Mheshimiwa awashirikishe wananchi wa maeneo husika katika hatua zote hadi hapo mradi utakapokamilika na kukabidhiwa kwa Halmashauri ya Wilaya na Kamati za Wananchi za maji kwa uendeshaji.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge ingawa muda wa kawaida wa maswali umekwisha, lakini kwa kuwa tulikuwa na mambo mengine yaliyochukua muda huo. Basi nitaongeza dakika tano ili tuweze kumaliza maswali. Kuna swali la nyongeza Wizara ya maji Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba niulize swali dogo la nyongeza, nashukuru Naibu waziri kwa majibu yake mazuri. Kumekuwa na tatizo kubwa sana la maji katika Wilaya Geita na inaonekana kazi hiyo tena inaweza ikachukua muda. Lakini kwa ajili ya dharura Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akaahidi kwamba angalau mabwawa mawili angalau katika eneo la Katoro na Nyarugusu yawe yanawasaidia wakati wanafanya upembuzi ili mradi huo ukamilike wakati wanatumia maji hayo?

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, tunatambua sana matatizo makubwa ya maji yanayowakabili wananchi wa Busanda na Geita kwa ujumla. Vile vile tunatambua matatizo hayo hayo katika Mikoa mingine yenye ukame. Tatizo hili la kuchelewa kwa huu mradi ni tatizo la kihistoria na pengine haliwezi kufidiwa na mabwawa. Lakini ikiwa liko tatizo ambalo linaweza likapunguzwa kwa kufikiria kujengwa bwawa basi namwalika Mheshimiwa Mbunge tukae tuzungumza ili tuelewe ni eneo gani hilo ambalo tunaweza tukafikiria kujenga bwawa ili liweze kusaidia wananchi wa eneo hilo pamoja na mifugo hasa ndiyo sababu yenyewe ya kuwa na mradi wa bwawa.

Na. 67

**Wavuvi Wadogo Wadogo**

**MHE. JUMA H. KILIMBAH** aliuliza:-

Kwa kuwa Ziwa Kitangiri ni kubwa na ni maarufu kwa ufugaji wa samaki aina ya Perege, Kambale na Mamba na kwa kuwa, kwa kiwango fulani ziwa hilo limeweza kutoa ajira kwa wananchi wa jimbo la Iramba Magharibi hasa wale waishio maeneo ya Doromoni, Tulya, Migilango, Mesi, Shauritanga, Kidaru, Ndurumo, Tyegelo, Mwamapulina na kwingineko palipo jirani na ziwa hilo:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya wavuvi hao wadogo wadogo wa Kitangiri ambao tayari wameanzisha *SACCOS* kupatiwa mikopo ili wapanue shughuli zao za uvuvi?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia zana za kisasa/elimu wavuvi wadogo wadogo ili waendane na mazingira ya uvuvi wa kisasa?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Hassan Kilimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Ziwa Kitangiri ni kubwa na ni maarufu kwa uvuvi wa samaki aina ya perege, kambale, kamongo na nembe. Serikali inawapongeza sana wavuvi wadogo wadogo wa Ziwa Kitangiri kwa kuanzisha vikundi vya uzalishaji chini ya utaratibu wa *SACCOS*. Serikali inawashauri wavuvi hao kuomba mikopo kutoka kwenye Taasisi za fedha ili waweze kuboresha shughuli zao za uvuvi. Ninamshauri Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na wananchi wa Jimbo lake na Taasisi husika katika suala zima la upatikanaji wa mikopo kwa wavuvi kupitia *SACCOS* zao.

Mheshimiwa Spika, Serikali haina fungu la kuwapatia wavuvi hao zana za kisasa za uvuvi. Hata hivyo, Serikali imeendelea kuhamasisha wavuvi wadogo wadogo kuunda vyama vya kuweka na kukopa kutokana na mapato yao ili waweze kununua zana bora za uvuvi ili shughuli za uvuvi katika Ziwa Kitangiri ziwe endelevu. Aidha, Serikali imendelea kuwahamasisha wavuvi nchini kuunda vikundi vya uzalishaji na vyama vya ushirika kwa lengo la kuwawezesha kuwa na uwezo wa kukopa kutoka katika taasisi za fedha nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kuwapatia wavuvi elimu, Serikali imekuwa ikiwapa mafunzo wavuvi wadogo wadogo yakiwemo yanayohusu ulinzi wa rasilimali ya uvuvi pamoja na kuanzisha vyama vya kuweka na kukopa na mbinu za kupambana na umaskini. Mafunzo yalifanywa kwa ushirikiano na iliyokuwa Wizara ya Ushirika na Masoko pamoja na Idara ya Kuondoa Umaskini. Mafunzo yamekuwa yakitolewa kwa awamu na utaratibu huu utaendelezwa katika maeneo yote ya uvuvi nchini kwa awamu.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha ninayo matangazo yafuatayo:-

Kamati ya Katiba Sheria na Utawala wanaombwa wajumbe wote wakutane leo hii tarehe 22 mwezi Juni, 2006 kwa ajili ya kupitia taarifa za Kamati na kikao hicho kitafanyika saa saba mchana katika ukumbi namba 37 kwenye ukumbi wa zamani wa Mkutano ya Bunge. Taarifa hii inagongana na mwito kwa wale ambao ni Wabunge wa

Chama cha Mapinduzi ambao wanatakiwa kwenye *Chamber* ya zamani Saa saba kamili. Nitawaachia wenyeviti muamue sasa mtafanyaje.

Hata Kamati inayofuata inamuelekeo huo huo. Kamati ya Fedha na Uchumi wanaombwa kukutana saa saba ghorofa ya nne chumba namba 432. Lakini baadhi yao ni hawa hawa wanaotakiwa saa saba kwenye ukumbi wa zamani kwa ajili ya mkutano wa chama cha mapinduzi. Inayofuata nayo iko hivyo hivyo, Kamati ya Maendeleo ya Jamiii mkutano umepangwa saa saba kwenye chumba namba 219 ghorofa ya pili. Lakini tahadhali ni ile ile haya yote yanagongana na mkutano huo mwingine.

**MHE. HAROUB SAIDI MASOUD:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika Kanuni namba 55 (3).

**SPIKA:** Karibu Mheshimiwa Haroub.

**MHE. HAROUB SAIDI MASOUD:** Mheshimiwa Spika kwa heshima na taadhima nataka kueleza yafuatayo ili nipate Mwongozo wako. Kwa kuwa zaidi ya asilimia 50 ya Wabunge ya Wabunge waliomo humu ndani ni wapya kabisa, na kwa kuwa wiki nzima iliyopita hapa mimi mwenyewe binafsi nimedhihirisha kwamba kuna Kanuni nyingi zinatenguliwa mara kwa mara. Kwa mfano wewe unapotoka nje wakati ambao siwa limekamatwa na askari wako wanaoruhusiwa kufuatana rungu hilo ni Askari Makatibu watatu pamoja na wewe mwenyewe binafasi. Lakini ukifika eneo hili tuliopo hapa kuna Wabunge tunatoka tunafuatana na wewe wakati ambao ni kinyume na Kanuni.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile cha kusikitisha zaidi uko pale wewe unataka kuondoka kuja huku, kunatolewa matangazo ya Wabunge binafsi wenyewe wanazungumza. Mimi naomba tufanyiwe Semina ya siku moja kuhusu vifungu maalum vya Kanuni vya humu ndani Bungeni, (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana. Uamuzi wa Spika ni kuafiki pendekezo la Mheshimiwa Masoud, nadhani hata kwa mambo mengine ambayo Waheshimiwa Wabunge wameniandikia hapa kwamba pengine hatua niliyochukua mapema, wanashindwa kabisa kuielewa Kanuni ile na iko wazi kabisa ikiwa kitu hiki na hakuna suala jingine tena ama vyote havipo ama kinachukuliwa kimoja. Kwa hiyo, nasikitika inabidi kwenye kiti hiki inabidi nilinde Kanuni sina njia nyingine.

Hakuna huruma na niseme tu jambo hili kama lililotokea asubuhi, Waheshimiwa Wabunge zaidi ya wanne wameniandikia kwamba kama inaruhusiwa kwanini wengine walikataliwa. Ndiyo inatokea hivyo, kwa hiyo nikawatuma Makatibu kwenye meza wakatazama tafsiri walionipa nikaisoma nikaiangalia kwenye Kanuni nikaona ni tafsiri sahihi, lakini bado naendelea kupata karatasi zinasema Spika alikosea, nawambieni sikukosea ndivyo Kanuni inavyosema.

Kwa hiyo, Katibu naagiza kwamba tufanye utaratibu ili tuwe na siku moja ya kuzitazama vizuri sana Kanuni zetu kama zilivyo hivi sasa, kwa sababu hatuwezi kufanya kingine hadi hapo tutakapo zibadilisha ahsante sana (*Makofi*)

## KAULI ZA MAWAZIRI

### UTEUZI WA MHESHIMIWA YUSUF RAJAB MAKAMBA KUWA MBUNGE

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, wakati akichangia Hotuba za Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Hotuba ya Bajeti ya Serikali zilizowasilishwa Bungeni kwa pamoja tarehe 15 Juni, 2006.

Mheshimiwa John Momose Cheyo alionyesha wasiwasi kuhusu uteuzi wa Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba kuwa Mbunge. Uteuzi wa Mheshimiwa Yusuf Makamba kuwa Mbunge umefanyika wakati yeye ni Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na umefanyika kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 66, (1) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ibara hiyo inaelekeza kwamba bila kuathiri masharti mengine ya ibara hii kutakuwa na aina zifuatazo za Wabunge yaani:-

(a)Wabunge wasiozidi kumi walioteuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watu wenye sifa zilizotajwa katika aya ya (a) na(c) za Ibara ya 67 na angalau Wabunge watano kati yao wakiwa wanawake.

Mheshimiwa Spika, suala la mtu kuwa au kutokuwa na sifa za kuweza kuteuliwa kuwa Mbunge limewekewa masharti katika Ibara ya 67 ya Katiba. Masharti aliyoyazungumzia Mheshimiwa John Cheyo ni yale yaliyomo kwenye aya ya (g). ya Ibara ndogo ya pili ambayo inaeleza kwamba mtu hatakuwa na sifa za kustahili kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa Mbunge(g) ikiwa mtu huyo ameshika madaraka ya Afisa Mwandamizi katika watumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania isipokuwa madaraka ambayo Rais aweza au anatakiwa kukabidhi kwa Mbunge kwa mujibuwa wa Katiba hii au Sheria iliyotungwa na Bunge.

Ikiwa mtu ameshika madaraka kwa ngazi ya Afisa Mwanadamizi katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano madaraka hayo ni ya aina ambayo yanaweza au yanastahili kukabidhiwa kwa Mbunge basi mtumishi huyo hapotezi sifa za kustahili kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, kwa mazingira haya ni muhimu kufahamu sifa za mtu kuteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa. Ibara ya 61 imeweka masharti kwamba kutakuwa na Mkuu wa Mkoa kwa kila Mkoa katika Jamhuri ya Muungano ambayo bila ya kuathiri Ibara ndogo ya tatu atakuwa ni Kiongozi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano

Wakuu wa Mikoa katika Tanzania Bara watateuliwa na Rais baada ya kushauriana na Waziri Mkuu na Wakuu wa Mikoa katika Tanzania Zanzibar watateuliwa na Rais wa Zanzibar baada ya kushauriana na Rais.

Mheshimiwa Spika, ufafanuzi wa Ibara hii ni kwamba Ibara ndogo ya kwanza inaelekeza kwamba Mkuu wa Mkoa ni kiongozi wa kisiasa katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano na si Afisa Mwandamizi. Mtu anaitwa kiongozi katika Serikali anatajwa ni kama vile Rais, Waziri Mkuu, Waziri, Mkuu wa Mkoa na nakadharika. Watu hawa sio Maofisa Wandamizi katika utumishi wa Serikali kama walivyo Makatibu Wakuu au Wakarugenzi.

Mheshimiwa Spika, Mkuu wa Mkoa ni madaraka ambayo anaweza kukabidhi kwa Mbunge, kinyume chake pia ni sahihi kwamba Rais anawewa kuteua mtu ambaye ni Mbunge kushika madaraka ya Mkuu wa Mkoa. Kwa hiyo, Afisa Mwandamizi katika utumishi wa Serikali yeye hana sifa za kuteuliwa kuwa Mbunge.

Mwisho nimalize kwa kueleza kwamba Rais anapomteua Mkuu wa Mkoa kuwa Mbunge Uteuzi huo ni wa kisiasa hivyo haukiuki masharriti ya ibara ya 67 (2) (g) ya Katiba ya nchi kwani Ukuu wa Mkoa ni Ofisi ya kisiasa na sio utumishi wa Serikali. Ahsante sana.

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2005, Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2006/2007 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2006/2007

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia hoja zilizopo mbele yetu. Awali ya yote napenda kuwashukuru wananchi wa Wilaya ya Chunya kwa kunichagua mimi kuwa Mwakilishi wao kwa kipindi hiki cha mwaka 2005/2010.

Nimesema wananchi wa Wilaya ya Chunya na sijasema Jimbo la Lupa ninakotoka kwa sababu sisi Chunya ni Wilaya moja na tuna Wabunge wawili. Tunapendana, tunaheshimiana, tunafanya kazi kwa pamoja Jimboni na hata kwenye ukumbi wako tunakaa pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimesema hivyo kwa sababu kuna pepo ambalo baadhi ya sisi wa Wabunge tunatoka Wilaya moja au Mkoa mmoja lakini tunanuniana utafikiri tunatoka Jimbo moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza sana watoa hoja na viongozi wote waandamizi wa Serikali waliotutengenezea Bajeti hii. Pia napenda kuchukua nafasi hii kumponza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa juhudi zake alizofanya za kuwafanya wanafunzi wa Mkoa wa Mbeya na Wilaya ya Chunya kwenda sekondari wale ambao hawakuchaguliwa.

Napenda kumwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba kwa juhudi zake hizo wanafunzi 800 Wilaya ya Chunya ambao walifaulu lakini hawakuchaguliwa wameenda sekondai. Hiyo ni karibu asilimia 75 ya wananfunzi wa Wilaya hiyo. Namwomba Waziri Mkuu aendeleze juhudi zake ili mwaka kesho wanafunzi watakaofaulu mia kwa mia waende sekondari. Maana naamini kwamba Mawaziri Wakuu wajao watatokana na wanafunzi hawa ambao Mheshimiwa Waziri Mkuu anafanya juhudi waende Sekondari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Bajeti hii ambayo ni ya kijani ambayo ni mwananchi *friendly* na Bajeti hii inaonyesha kwamba asilimia 39 ya Bajeti inatokana na misaada na mikopo kutoka nje. Kiasi hiki ni kikubwa sana Mheshimiwa Spika na hasa hasa inapokuwa mikopo kwa wananchi hapo siku za mbele. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali misaada hii na mikopo ielekezwe kujenga kwenye sehemu ambazo zinajenga uwezo wa kujitegemea hapo baadaye. Moja wapo wa sekta hizi ni kilimo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hayati Baba wa Taifa aliwahi kutamka kwamba katika maamuzi ambayo yalimpa wakati mgumu sana maishani mwake ilikuwa ni kuomba msaada kwa *Colonial Master* wakati ya maasi ya mwaka 1964. Ilimpa wakati mgumu sana na ninaamini sana Waziri Mkuu katika kipindi chake kifupi akiwa ofisini alipata wakati mgumu sana kuamua kwenda kuomba chakula kwa Mataifa ya nje, najua alipata wakati mgumu sana. Napenda kumwambia Waziri Mkuu kwamba hata kuwa na uamuzi kama huo siku za usoni kama Serikali itakipa kilimo kipaumbele kinachostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mikoa inayoitwa *big-four*, pamoja na Mkoa wa Kigoma inaardhi nzuri, inarutuba inamvua ambazo zinanyesha kwa wastani kila mwaka, naiomba Serikali ifanye mapinduzi ya kilimo katika Mikoa hii ili iweze kulisha nchi yetu na kuweka ziada ya kuuza nje. Ifanye mapinduzi ya kweli kweli. Mheshimiwa Saddiq juzi akichangia hoja hii aliomba walau katika Halmashauri zetu kuwepo na greda moja kila Halmsahauri. Mimi nasema kabla ya greda moja, hii mikoa mitano hii kila Halmashauri iwe na trekta moja. Trekta moja la kuwakodishia wananchi ili waweze kulima mashamba makubwa ili nchi iwe na chakula cha ziada na cha kuuza nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuongeza kiasi cha ruzuku ya mbolea kwenye Bajeti hadi kufikia bilioni 21. Lakini kiasi hiki hakitakuwa na maana kama bei za mazao hazitaangaliwa. Hii biashara huria tumewaachia mashirika na watu binafsi wananunua chakula na mazao mengine kwa wananchi wanapanga bei wao wenyewe. Naiomba sana Serikali iangalie sana bei za mazao. Hawa watu wanaonunua mazao kwa wananchi wetu hawana huruma wanapanga bei ambazo ukilinganisha na bei za soko la dunia utashangaa wanapatafaida za ajabu sana naimbo Serikali iliangalie sana naiomba Serikali iliangalie sana hili. Hatuwezi kuongeza tija katika kilimo na kiasi cha mazao kama wananchi watakuwa wanapewa bei ambazo ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuipongeza Serikali kwa kuangalia mishahara ya watumishi lakini pamoja na hayo naiomba Serikali iangalie na mafao ya wastaafu. Inasikitisha sana wastaafu wanaishi maisha ya taabu sana wengine mpaka wanaenda

kutafuta ajira ambazo zinazalilisha staha zao. Mfano siku za usoni tuliona Katibu Mkuu Mwandamizi mstaafu aliishi kwa taabu sana mpaka Serikali ilipokwenda kumwona na kumuongezea mafao zaidi ya yale ambayo yako kwenye ajira yake. Kwa hiyo, naomba Serikali inapoangalia mishahara ya watumishi iangalie na mafao ya wastaafu.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kidogo Elimu ya Juu. Katika hotuba yake Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete alisema kwamba Serikali yake ya awamu ya nne kwa kipindi hiki itajenga angalau Chuo Kikuu kimoja. Napenda kuipongeza kwamba inatimiza hoja hiyo ya Rais kwa kujenga Chuo Kikuu hapa Dodoma. Lakini Chuo Kikuu kimoja hakitoshi, kama tulivyoelezwa kwamba wenzetu katika Afrika Mashariki wengine wanafunzi wa vyuo vikuu wako laki moja wengene 60,000, sisi tunakaribia 40,000. Inapokuja *Federation* ya Afrika Mashriki hata ajira itakuwa ni ya soko huria kwa hiyo wananchi wa Kenya wa Uganda watakuja kuzichukua ajira nyeti hapa kwetu. Watoto wetu wao wataishia ajira za chini, kwa hiyo ningeomba Serikali ingalie kufungua Chuo Kikuu kingine Mbeya. Mbeya tuna chuo cha ufundi ambacho kinafaa kuwa Chuo Kuu, na ninaimani kwamba tukikifnaya Chuo Kikuu cha Mbeya walau tutawakaribia wenzetu wa Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee miundombinu. Naipongeza sana Serikali kwa kuamua kujenga uwanja wa ndege wa kisasa Mbeya, lakini uwanja huu utakuwa ni *white elephant* kama hatuta boresha miundombinu inayoelekea kwenye uwanja huo. Ilani ya CCM imetamka kwamba barabara ya kutoka Mbeya kwenda Chunya mpaka Makongorosi itajengwa kwa kiwango cha lami kwa kipindi hiki cha miaka mitano. Lakini naona Serikali mpaka sasa bado inavuta miguu kuhusu suala hili. Pia Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete aliahidi akiwa Mbeya kwamba barabara ya kutoka Mbalizi kwenda Mkwajuni mpaka Makongorosi tumwachie yeye. Napenda kuikumbusha Serikali kwamba Rais alitoa ahadi hiyo kwa hiyo ni wajibu wenu Serikali kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami ili barabara hizi ambazo zinahudumia kiwanja cha Mbeya, barabara ya Mbeya – Chunya, Makangorosi, barabara ya Mbalizi- Mkwajuni Makongorosi, barabara ya Mbozi kwenda Ileje, barabara ya Tunduma kwenda Sumbawanga ziwe zote kwa kiwango cha lami.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kidogo, mradi wa umeme wa kutoka Makongorosi kwenda Lupa-tingatinga.Lupa-tingatinga kuna kilimo cha tumbaku ambacho kina karibu kilo milioni 5 kila mwaka na mradi huu wa ujenzi wa umeme umeanza mwaka 2000, hii ni 2006 bado uko robo sijui kwanini? Na huu mradi ungefika mahala pake ungefika Lupa-tingatinga ungesaidia sana kutunza mazingira. Kwa sababu wananchi wa kule wanatumia sana miti na kuni kukaushia tumbaku wangeweza kukaushia umeme. Kwa hiyo naiomba sana Serikali ikamilishe mradi huu wa meme. Bajeti inasura mbili, kupanga matumizi ni sura moja lakini vilevile kusimamia matumizi ni sura nyingine. Ripoti ya Mkaguzi Mkuu hii hapa kwa kipindi kinachoishia 2005 mwenzi Juni, inaonyesha kwamba ni Wizara chache sana ambazo zimepata cheti kisafi cha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu. Naomba nizitaje hizo, Wizara zilizopata cheti kisafi ni Ikulu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais Ofisi ya Spika, Tume ya Maadili, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Maendeleo ya Jinsia, Wanawake na Watoto, Tume ya Haki za Binadamu, tume ya Sheria, Wizara ya Mipango, Wizara ya

Mawasiliano na Utalii na Mikoa ya Arusha, Lindi, Mara, Mbeya, Morogoro, Tanga, Kagera na Manyara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara nyingine zote Mheshimiwa zimepata aidha cheti cha kati au cheti kichafu, sasa itakuwa kila mwaka tunapanga Bajeti wanaenda wanatumia wanapata cheti kichafu, nimeona katika Halmashauri walipoambiwa kwamba mkipata cheti kichafu hamtapata ruzuku ya maendeleo. Mwaka jana Halmashauri ambazo zilikuwa cheti kichafu ni nne tu, kwa hiyo naiomba Serikali suala hili liangaliwe kwa makini sana ili hawa *Accounting Officers*, kama wakipata cheti kichafu au cheti cha kati, angalau wakatwe hata mshahara.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema yote haya naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii nami nichangie katika hotuba za Mawaziri wa Mipango na Fedha. Kwanza kabisa nataka nichukue nafasi hii kumkaribisha Mheshimiwa Yusuf Makamba katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano, anastahili kuwa hapa na sifa zake ni nyingi kwa sisi tunayemfahamu kwa muda mrefu tangu akiwa ni kada tu wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nina haya:- Kwanza, nataka ninukuu Katiba ya Jamhuri ya Muungano katika Sura ya 3 inayozungumzia kazi za Bunge. Na hii ni kifungu cha 63(3)(c). Kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu na wa muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano na kutunga Sheria kusimamia utekelezaji wa mpango huo. Ninalisema hili kwanza kama *preamble* ya *paragraph* katika mazungumzo yangu.

Mhehimiwa Spika, mazungumzo tunayoyazungumza hapa, kwanza, yatakuwa na maana kama tutakuwa tunaanza kwa kushukuru kazi nzuri ambayo imeishafanywa. Mimi kwa upande wangu nikiwawakilisha wananchi wa Wilaya ya Ukerewe, ningependa kuishukuru sana Serikali kwa kufikisha umeme katika Kisiwa cha Ukerewe? Na ni matumaini yangu kwamba katika Bajeti hii tunayoizungumzia itakuwepo kasma ya kusambaza umeme katika Visiwa hivi hasa ukizingatia kwamba sekondari zimejengwa kwa wingi na tunahitaji kuondoka hapo tulipo, tuingie katika *technology* za kisasa ukizingatia kwamba Ukerewe ni mahali ambapo tuna sehemu finyu ya kufanyia kazi, tutahitaji *high technology* katika kufanya kazi zetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ningependa pia nizungumzie mantiki ya paragraph niliyoinukuu katika Bajeti hii. Moja; Bajeti ndiyo inayoeleza kwa kuweka rasilimali katika yale matashi tunayoyatamka kupitia katika Ilani ya Uchaguzi na pia kutia kwa kauli mbali mbali za Viongozi wetu wa Kitaifa ambao tumewapa madaraka ya kufanya hivyo. Kwa hiyo, mtu akisoma bajeti, ndipo pale tunaelewa kama kweli tutafika huko tunakokwenda. Katika hotuba ya Wairi wa Fedha mara kwa mara alirudi katika msingi wa Ilani ya Uchaguzi ambayo tulijinadi kwa wananchi na wakatukubali ya kwamba tutakapokuwa tumeshinda, ni haya ambayo tutayatekeleza.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa, nina machache tu ya kuongezea, kuboresha hiyo kazi inayofanywa. Kwanza, Bajeti si suala la kugawana pesa. Ni suala la kuunganisha hiyo mantiki ya maendeleo. Nitatoa mfano; Rais alipokutana na wakulima wa Pamba katika nchi hii alisema tuondoke katika kilogramu 300 kwenda kilogramu 1000 kwa kila hekta. Maana yake nini, maana yake Pamba hii ikishazalishwa ni lazima iondolewe vijijini ifikishwe mahali pa kuisindika kwenda viwandani au kwenda nchi za nje. Tusipofanya hivyo, tunakuwa na *crisis* ya kubaki na Pamba isiyoliwa majumbani na ambayo ni hatari kwa moto na haitakuwa imefikia lengo kwa sababu lengo la kilogramu kutoka 300 mpaka 1000, maana yeke ni kufufua uchumi katika mazingira haya na kwa maana nyingine kuondoa umaskini miongoni mwa hawa watu. Kwa hiyo, maombi ya barabara na hasa barabara za Geita ambayo ni Wilaya ya kwanza katika kutajirisha nchi hii kwa kilimo cha Pamba inaendana kabisa na dhana ya Rais ya kwamba hawa wakulima wa Pamba wa Geita watakaotoka kilogramu 300 mpaka 1000, lazima waipate hii huduma. Haina maana nyingine yoyote. Inamaa pia ya kwamba hii dhahabu ambayo sasa imepanda bei na ambayo mimi ningependa baadaye Serikali ieleze ni kiasi gani tumepata kama nchi kwa kupanda kwa dhahabu kutoka 300 *dollars* kufika kwenye 700 *dollars*, itafika! Ni kiasi gani hizo hesabu nazo tuzijue. Kama hatukufaidika na chochote, tumeibiwa, tumeliwa.

Mheshimiwa Spika, sasa, nataka niitumie Geita kama mfano tu wa mantiki ya kupanga maendeleo ya kwamba Geita ukishaipa zile barabara, utazoa Pamba ile, utarahisisha uchimbaji wa dhahabu na kwa maana hiyo utakuwa umechangia katika pato la Taifa, si suala la Wasukuma tu kusimama hapa na kulia lia na barabara. Manti hii, inaweza ikatumika pia katika Kanda ya Magharibi, ya kwamba ukitaka kufungua uchumi ulioko katika Kanda ya Magharibi, huwezi kuacha kuona kwamba giza linalotanda usiku katika sehemu hiyo ya Magharibi inaashiria kutotumia rasiliomali ulizonazo katika Ukanda huu.

Kwa hiyo, mtu anayetoka Kigoma anapozungumzia kufungua Kanda ya Magharibi, si kwa sababu tu ni Mbunge wa kule, ni kwa sababu itasaidia pia kuleta mapato katika Taifa. Kwa hiyo ndiyo maana, bajeti ina amaana hiyo. Hata unapozungumzia barabara ya kutoka Bunda kwenda Ukerewe mpaka Ilangala, ni mantiki hiyo hiyo, minofu ile inasombwa na magari kutoka katika sehemu za Ilangala – Ukerewe zikitoka kwenye visiwa vya Ganakamasi kuelekea katika barabara kuu ya Msoma - Mwanza ili iwezwe kufikishwa viwandani na iweze kusafirishwa.

Kwa hiyo haya mambo lazima tuatizame kwa mantiki. Huwezi kusema watu waongeze Pamba, hawana barabara katika eneo hilo. Huwezi kusema watu wavue zaidi, hakuna barabara ya kuweza kuchukua kwa malori mazito samaki wanaopelekwa viwandani. Kwa hiyo lazima tupange hivyo na tuelewane ya kwamba tunapofanya hivyo. Tusifanye vitu ambavyo havileti mantiki kwa hiyo unakuta tumegawana pesa, tunapomaliza kugawana pesa, basi mambo yamekwisha.

Mheshimiwa Spika, nataka niongeze *point* ya tatu, ugawanyaji wa watu wataalam, lazima uwe sasa *Pan-Territorial*. Nchi yetu haijaweza kuwa na wataalam wa kutosha

kuajiri *within the environment*. Kwa mfano; Wilaya ya Ukerewe ukituambia tutangaze kumtafuta Ofisa Mipango, utakuta yakwamba akitangazwa mtu wa Mwanza Mjini na mimi wa Ukerewe, mtu ata-*apply* Mwanza mjini. Au wa Mafia aki-*apply* pamoja na mtu wa Dar es salaam na sasa hivi Mafia hata usafiri hamna. Hakuna meli hakuna ndege! Mtu atakuwa ni waajabu kwenda kujitolea kama Mmisionari Mafia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo unajikuta ya kwamba Serikali isiposimamia watumishi kama rasilimali katika kufanya hizi kazi, tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu. Tutagawa mapesa, wataalam hawapo na mwenzangu aliyemaliza kuzungumza Mheshimiwa alieleza tatizo moja tu la kusimamia pesa. Hivi sasa tunaanza kuwapa adhabu wananchi ambao watendaji wao ni wabovu. Tunawanyima ruzuku, *Capitation Fund* kwa sababu tu anayesimamia pesa katika Wilaya hilo amekuwa mbovu, kosa ni la nani! Mimi nina Ofisa Mipango sijui amekaa miaka ishirini na ngapi huko! Una kitu tena hapo! Hakuna kitu. Kwa hiyo watu hawa wawe katika *Pan- Territorial* ili wagawiwe katika Wilaya na wafanyiwe kazi na wasimamiwe kwa sababu hawa ndiyo wanarudisha hii kasi yetu nyuma. Bado Local Government, kwa kweli zinarudisha kasi nyuma ya kasi hii tunakwenda. *Local Government seriously*, Waziri anayehusika, lazima azitizame kwa karibu. Wtendaji wake hawajaelewa na hawajaenda kwa kasi hii.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba vijana. Vijana ni Rasilimali. Vijana ni watoto wetu. Kuna wakati vijana wakinyenyeka hivi, tunakuwa na wasi wasi hasa sisi wenye umri mkubwa. Lakini, ukiwa ni mzazi, kijana wako anapozidi kupendeza na kunawiri na kushika madaraka unakaa chini na unajisikia wewe ni mama wa yule kijana. Ndivyo tunapaswa kufanya kwa vijana wetu na ninapenda niwapongeze vijana waliomo katika Bunge hili ambao wamethubutu kugombea nakuja hapa. Lakini, kwa sababu mimi ni Kamanda wa Vijana wa Mkoa wa Mwanza, ninapenda niwaambie kwamba hatutakwenda mbali kama hatutapeleka rasilimali katika kuwa jenga vijana wa nchi hii. Hizo kilogramu kutoka 300 mpaka 1000 za Pamba katika mkoa wa Mwanza zinahitaji vijana, watu wanaoweza kupiga makasia katika kuvua ni vijana, watu wanaoweza kufanya kazi zote hizi, tusipokubali ni vijana. Kwa hiyo bajeti hii ni lazima tuipime tuone ni kisi gani ambacho tumepeleka katika kuimarisha vijana. Vijana kati aya umri wa miaka 15 mpaka 35 wana kuwa kama *per cent* 35. Lakini ukichukua wote watoto mpaka vijana kufikia umri wa miaka 35, *they are 46%*. Kwa hiyo, ni wengi mno tusipowalenga hawa. Ninataka na *point* nyingine, tuna *bombshell* kwamba tufikapo mwaka 2009, vijana wote tuliowaingiza mwaka huu shuleni, watakuwa wanatoka *Form Four*. Tumejiandaa kiasi gani na Bajeti hii ikiwa ni *building block* ya kujiandaa kwa mwaka 2009. Kwa hiyo, haya mambo ya vijana tuwachukulie seriously, tuwawezeshe tuweze kufika mahali ya kwamba hawa ndiyo wanaoweza kuifanya kazi ambyo sisi wazee kwa kweli sasa hivi tutakuwa na ninyi humu hatutoki, tutakuwemo humu humu. Lakini, tutakuwa tunawasaidia kuwapa mawazo ya kusonga mbele, vijana mkiwa wapiganaji wa mstari wa mbele.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Visiwa! Ningeomba visiwa katika bajeti viwekewe mkakati maalum. Ukiangalia Mafia na Ukerewe, unatoa kilomita 2 za barabara ya lami, unataka mtu aende na tingatinga kupeleka Mafia, akodishe meli kwa kilomita mbili! Ni *logic* hiyo inaweza kuwa kama unalima Kibaha kwa sababu utatoka tu unaenda kuchukua

tena Dar es salaam. Lakini siyo mantiki ya ku-*treat* visiwa. Ningekuwa na muda ningeelza zaidi jinsi tunavyohitaji hata kwenye elimu na mambo mengine, tunapaswa watu wa Visiwani kuangaliwa kwa namna ya tofauti kwa sababu tunakwama tunakuwa kama ni *prisoners in our own country*.

Mheshimiwa Spika, ningependa tu kumalizia kwa kusema ya kwamba barabara ya Geita, Usagara na barabara zingine katika maeneo inakolimwa Pamba, itatekeleza Azma ya Rais kutoka kilogramu 300 kwenda kilogramu 100. Barabara ya Bunda mpaka Ilangala Ukerewe, itakuwa inatekeleza azma yetu ya kuongeza *export* za minofu ya samaki, na vijana wa Tanzania hakuna atakayeleta kitu kingine zaidi kama tunataka kwenda kwa kasi mpya na Ari mpya katika utendaji wakazi na katika utekelezaji.

Mwisho, ningeiomba Serikali siku moja ifike mahali ifanye lile lililofanywa na Uganda. Bajeti ni sheria. Kama mtu akikiuka katika utekelezaji, amevunja sheria. Kwa hiyo, tunahitaji sheria ya utekelezaji wa Bajeti. Kama ni Waziri, kama ni Mkurugenzi, kama ni mtu yoyote ameacha kutekeleza sheria ya bajeti, anapaswa kuchukuliwa hatua kama mtu yeyote anaye vunja sheria ya nchi hii, kwa sababu hatuwezi tukazungumza, tukagawa pesa halafu mtu mwingine avunje. *And finally*, naunga mkono hoja. *( Makofi)*

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, na mimi napenda kwanza kusema kwamba naunga mkono hotuba zote mbili za Mawaziri wa Mipango na Uwezeshaji na Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, hotuba hizi za Bajeti zimekuja katika muda ambao Watanzania sote kwa pamoja tunaingia kwenye mchakato wa mabadiliko ya kifikra. Kwa sababu ili tuweze kuelewana hapa, lazima tuwe na fikra ya aina moja. Unapozungumzia Bajeti ya nchi, unazungumzia namna ambavyo nchi inaweza ikakusanya mapato yake, ikapata mapato mengine na ikapanga matumizi kulingana na vipaumbele vilivyopo.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa Bajeti hii, bado tuko tunachechemea kwa asilimia 39. Utegemezi wetu ni asilimia 39. Kwa msingi huo, mimi napenda niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri kwa kuandaa Bajeti hii. Lakini, kimsingi, labda niangalie zaidi namna gani tunajikita katika kuboresha mapato yetu. Kwa sababu huo ndio msingi mkubwa wa kugawana matumizi hapa ndani ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo labda niseme kwamba kwa kipindi kilichopita, wenzetu wa *TRA* wamefanya kazi nzuri ya kukusanya mapato na Mheshimiwa Rais ameagiza kwamba ikiwezekana, wakusanye zifikie bilioni mia mbili kwa mwezi. Ni lengo ambalo linawezekana kufikika. Lakini litafikiaka kwa namna gani, wataendelea kukamua ng’ombe yule yule au wataongeza ng’ombe wengine kuwakamua zaidi ili kuweza kupata hayo mapato. Hiyo ndiyo changamoto kubwa sana. Nina imani kabisa kwamba yote yakifanyika, yawezekana na *theme* ya Watanzania na haswa ikiongozwa na Rais, ni: “Maisha bora kwa kila Mtanzania”. Sasa, maisha bora tutayapataje? Tutayapata tu iwapo kweli Bajeti hii itatekelezeka kama ambavyo tunaitegemea.

Mheshmiwa Spika, in changamoto nyingi sana. Uwezo wa Serikali, bado mdogo, tunahitaji kuongeza ukusanyauji wa mapato. Lakini, vile vile bado tuna sehemu kubwa sana ya mapato ya nje na misaada ambayo tunaitegemea pamoja na mikopo, kwa sababu bidhaa zetu tunazouza nje, bado hazijaweza kuleta mapato mengi sana kuweza kui-*cover* Bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, tatizo lililopo, ni namna ya kusimamia matunmizi yetu ya ndani na hii nadhani ni tatizo kubwa sana. Wachangiaji wenzangu wamezungumzia na wamegusia gusia hapa. Sasa hivi utakuta fedha nyingi sana tunai-*pump* kwenye Halamashauri ya Wilaya pamoja na Miji na Majiji. Lakini usimamizi wake ukoje! Hivi inakuwaje leo tunapeleka fedha nyingi kwenye Halmashauri zetu za Wilaya halafu watendaji kwa sababu moja au nyingne,hawatumii fedha vizuri na tatizo tumekuwa mara nyingi tukisema Madiwani msimamie, Madiwani msimamie. Sasa huyu Diwani ambaye kwanza hana mshahara, ana posho. Diwani huyu huyu ambaye unamtegemea asimamie zaidi udhibiti wa matumizi kwenye Halmashauri, bado hana uwezo wa kufanya vile na hii inasababisha matumizi mengi yanatumika, baadaye mnawaambia Waheshimiwa Wabunge mnavyokuja Bungeni, ninyi Madiwani mshirimkiane na Halmashauri zenu. Nadhani ningependa kushauri kwamba muda sasa umefika, hebu tuangalie upya ushiriki kikamilifu wa Madiwani katika kusimamia matumizi ya Serikali. Hii itawasaidia wao kuongeza changamoto kubwa sana katika mchakato mzima wa kusimamia matumizi.

Mheshimiwa Spika, ni aibu kubwa sana kuona kwamba, Halmashauri zinapewa fedha kwa ajili ya maendeleo, Ruzuku ya Maendeleo. Lakini kwa sababu watendaji hawakufanya kazi vizuri, pengine ni kwa sababu hawana uwezo wa kutekeleza majukumu yao vizuri zaidi, Halmashauri zinapata hati chafu na ukupata hati chafu maana yake huwezi ukapata fedha ya ruzuku ya maendeleo. Sasa hapa unayemuadhibu ni nanui, ni mwanannchi. mwananchi ana kosa, hana kosa. Je, Serikali inawachukulia hatua gani watu ambao wamesababisha matatizo kama haya. Mimi nafikiri kuanzia bajeti hii tungesema kwamba kuanzia sasa hivi mtendaji yeyote, *Accounting Officer* yeyote yule ambaye atabainika kwamba hakusimamia fedha vizuri, basi awajibishwe moja kwa moja, yeye mwenyewe na siyo kuwaadhibu wananchi wa Halmashauri husika, wa eneo husika.

Mheshimiwa Spika, tukifanya namna hii itachochea zaidi tija hata kwa wananchi wenyewe kuchangia shughuli za maendeleo. Ninaamini kabisa kwamba wananchi wakiona udhaifu huu umesimamiwa na Serikali vizuri, itasaidia sana kuboresha na hata kuimarisha matumizi vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye taarifa ya Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti Mkuu wa Serikali, ameonyesha wazi kwamba kuna baadhi ya Wilaya, Idara za Serikali, Halmashauri za Wilaya hazikufanya vizuri. Mahesabu ni machafu. Lakini bado tunasema hivi, leo huyu Mkaguzi Mkuu wa Serikali aliyepo sasa hivi ni Kaimu Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, ni Kaimu. Atakaimu mpaka lini! Huyu mtu hawezi kuwa na *responsibility* vizuri, hawezi ku-*take up responsibility* vizuri zaidi. Ningeshauri Serikali ijaribu kuangalia, nafasi kama hii iko Kikatiba na ni nafasi nyeti sana. Unamtegemea mtu huyu adhibiti mahesabu na akague mahesabau, leo anaendelea kuw Kaimu, Kaimu. Atakaimu mpaka lini? Ningeiomba Serikali iliangalie hili, kwa

sababu ndiyo chanzo cha ulegevu katika usimamizi wa matumizi ya fedha za Serikali.Pamoja na hayo nizungumzie kuna suala moja ambalo wengi tunapenda kulizungumzia. Ni uwiano wa uchumi wa kijiografia. Hii kwa kweli tukubaliane tu, tuangalie wenzetu wa Mtwara *Corridor* wanatakiwa wafanyiwe nini katika bajeti. Bajeti iainishe vizuri mambo ya msingi mwaka hadi mwaka kwa miaka mitano nini ambacho watu wa Mtwara *Corridor* yatapaswa yafanyike. Tuangalie watu wa *Central Corridor*, tuangalie watu wa *West Lake* au *Lake Zone*, tuangalie wa *Northern Corridor* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, bila kufanya hivyo na kuweka *priority*, bado tutakuwa na tatizo moja la matumizi ya Serikali kwa sababu nasema hivi, kuna kuwa na watu wanakuwa na *vested interest*, wenye kufanya maamuzi. Nitatoa mfano sasa hivi Mheshimiwa amemaliza kuzungumza mtu wa Mbeya hapa, anasema kwamba kule Mbeya Uwanja wa Songwe umeishakamilika kwa kiwango Fulani lakini hauna miundombinu. Lakini, Uwanja wa Mwanza una miundombinu, una *runway*, hauna *terminal* peke yake. Ukiujenga Uwanja wa Mwanza, ukaujengea *terminal*, maana yake ni kwamba unakuwa ni Uwanja wenye hadhi ya Kimataifa utakaoongeza uchumi katika nchi hii. Sasa unaendelea kutumia kule Mbeya, Mwanza umeacha nusu. Matokeo yake Mwanza ni nusu, Mbeya ni nusu. Unakuwa mtu wa nusu nusu. Hatuwezi kwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, tufike mahali tuwe na *economic priorities*. Kama tumeamua kujenga Mbeya, basi tujenge pakamilike, ndio tu-*move* mahali pengine. Kama ni Mafia, tujenge pakamilike, ndiyo tu-move mahali pengine. Kama ni Mwanza, basi tukamilishe. Mimi nafikiri itakuwa vizuri sana. Ninaamini kwamba kila Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge hapa wanawakilisha *interest* za maeneo wanayotoka. Lakini tuangalie kama nchi, kwa sababu ukitaka iweze kuwa na uchumi mkubwa zaidi, lazima uwe na *priority* katika bajeti yako. Hatuwezi kujigawa gawa. Leo hii bajeti sawa sawa na Sungura. Huwezi ukagawa hii bajeti kwamba kila Jimbo lipate pesa za kutosha. Kila Mbunge apate pesa za kutosha, haiwezekani. Lakini tukienda kwa miaka kwamba mwaka huu *Priority number* moja, ni mambo ya kilimo kwa mfano, ongeza pesa kwenye kilimo umo. Mpatie Mungai afanye kazi vizuri. Leo Mungai ukimpa pesa kidogo ya kilimo atafanyaje na kilimo ni dude kubwa sana na sijui kama tutapona safari hii, tuko na wewe tu upande wa kilimo. Kwa sababu shida ni kwamba siyo Mungai, shida ni kwamba fedha hazitoshi.

Mheshimiwa Spika, mimi ningeomba sana katika uwiano mzima wa kupanga Bajeti, tujaribu kwenda kwa *priorities* na hii itatusaidia. Mheshimiwa Mongella amezungumza hapa. Kanda ya Ziwa kuna Wavuvi wengi sana, wengi sana. Kuna mabonde mazuri, mimi Jimbo langu la Busega limepakana na mwambao wa Ziwa Viktoria, lakini njaa ndiyo vijiji vya kwanza kupata njaa kila mwaka ukiingia. Tumeshindwa kufanya kilimo cha umwagiliaji, simple like that. Tulimpigia kelele Mheshimiwa Keenja wakati huo alikuwa Waziri wa Kilimo. Akaleta *pump* nne za miguu za kukanyaga hivi. Hivi kweli hawa watu unawasaidia umwagiliaji kweli! Leo, pump nne za kukanyaga na miguu eti unataka nkuanzisha kilimo cha umwagiliaji, ni kilimo kweli au ni mzaha. Huu ni mzaha! Ninaomba Mheshimiwa Mungai anapozungumzia suala la kilimo cha umwagiliaji, hebu ajaribu kuangalia maeneo yepi tu-*invest* ya kutosha. *It's*

*better* tu-*invest* katika maeneo machache, lakini tupate chakula cha kutosha na kila mwaka tutakwenda hatua kwa hatua. Bila kufanya hivi tutakuwa tunafanya mchezo wa kuigiza.

Mheshimiwa Spika, hata kukaa ndani ya Bunge lako hapa, tutakuwa tunapiga kelele tu, lakini haitusaidii.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, labda tu nishauri. Mimi ninaona kidogo namna ya kujadili hotuba hizi mbili ya Mipango na Fedha. Waheshimiwa Wabunge tunajadili labda kwa sababu tuna muda mchache wa kujadili. Lakini, ukizungumzia Bajeti ya Serikali pamoja na mipango yake, tunapaswa kujikita zaidi katika masuala ambayo yana uwiano wa kitaifa. Tukianza kujikita kila mtu Jimboni, Jimboni, *therefore* nadhani tuna-*miss a point*. Hii ingekuja zaidi kwenye Bajeti za kisekta ili tuweze kuongelea kwa kina zaidi na Mawaziri husika waweze kuchukua *full responsibility*. Ninadhani kuna haja safari ijayo, labda tufanyiwe semina kidogo namna ya kujadili hiz Bajeti zetu. Itatusaidia sana. Vile vile napenda tu kuzungumzia kwamba, suala la kilimo siku hizi ni biashara. tunaomba hili suala la kusema tunatoa ruzuku kwa aajili ya mbolea ni sawa. Lakini ruzuku ya mbolea hii inakwenda wapi! Watu wasiotumia mbolea hii ya kemikali watafanya nini? Kwa hiyo, kuna haja zaidi ya kuweza kuangalia kwamba pengine kuwe na mradi wa kuweza kutoa mikopo kwa wakulima. Tukiwakopesha wakulima, tutawasaidia zaidi kuliko kusema tunatoa ruzuku ya mbolea. Tuwajengee mazingira ambayo yatawawezesha wao kuwa *s ustainable*.

Mheshimiwa Spika, ruzuku hii sasa ni sawa *it's like a hand to mouth*, unakula inakwisha. Mwaka kesho unahitaji tena ruzuku. Lakini, ukimwezesha mkulima ukampatia mikopo ya kilimo, utakuwa umemsaidia zaidi. Na mimi ningeshauri kwamba hizi Benki ambazo zinamitandao zipewe mamlaka ya kuweza kusambaza mikopo hii. Kwa sababu hizi benki ziko karibu na wananchi, leo unaipa *Exim Bank* kusambaza pesa za pembejeo na mikopo ya wakulima. *Exim Bank* iko Mwanza mjini, iko Arusha, Dar es salaam sijui na Mtwara, basi. Sasa, mimi nafikiri kuna haja ya kujaribu kuangalia upya suala zima hili ili tufanye kilimo kiweze kuwa biashara. Tukifanya kuwa biashara, itasaidia zaidi wakulima kuona faida ya kulima na kupata faida katika mazao wanayouza.

Mheshimiwa Spika, zamani mkulima alikuwa analima kwa kulima tu na hasa Wasukuma tulikuwa tukilima Pamba sisi, ukishauza Pamba unakwenda dukani kwa Bwana Shah unasema nipe Baskeli kama ya Masunga au ya Masanja. Haulizi hata bei, kwa sababu alikuwa ana pesa za kuweza kutosha gharama zao ambazo wametumia katika kilimo. Lakini leo hii kilimo ni gharama. Tutapiga hadithi kwamba tutoe kilo 300 mpaka 1000, haiwezekani, kama bei yenyewe hatuwezi kuigarantii kwa mkulima kwa sababu gharama za uzalishaji wa zao lolote lile imekuwa ni kubwa sana. Sasa ifike mahali Serikali iangalie ni nmna gani ya kuweka bei ambazo zitakuwa na mvuto kwa mkulima. Sasa hivi kila mkulima ukigusa Kahawa anakwambia gharama ni kubwa, Pamba, Korosho na kadhalika. Kuna wakati wakulima wanasema kwamba ni heri kuachana na kulima pamba, tukalima nyanya au mazao mengine ambayo nitapata *cash* kwa haraka, siyo mtu unakwenda, pembejeo bado unasumbuliwa kuipata.

Mheshimiwa Spika, napenda nimalizie kwa kusema kwamba, suala la umeme ni muhimu sana kwa Serikali na naipongeza na ninaomba kweli tukipata nishati, itasaidia sana sana kukuza uchumi na hata *TRA* watakusanya sana pesa kama tutakuwa na nishati ya kudumu na ya uhakika na ya kuaminika. Vinginevyo. Hii kata umeme ni tatizo kubwa sana kwa uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho namalizia kusema naunga mkono hoja hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, namwita Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, taarifa niliyonayo ni kwamba Mheshimiwa Monica Mbega, hajisikii vizuri amepumzika nyumbani kwake, naye kama kawaida yetu tumkumbuke katika dua zetu ili apate afueni haraka. Nadhani msemaji wa mwisho kwa asubuhi hii atakuwa Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa fursa hii. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Zakia H. Meghji, Waziri wa Fedha, kwa kuwasilisha Bungeni hapa bajeti nzuri ambayo kwa kiasi kikubwa inajibu changamoto mbalimbali zinazotukabili kama Taifa katika kukuza uchumi na katika kuboresha maisha ya Watanzania. Vile vile nimpongeze Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, kwa muhtasari mzuri wa hali ya uchumi na mapendekezo ya mpango wa muda wa kati wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wangu kama Wabunge wenzangu walivyosema, bajeti hii kwa kweli haina tatizo kimwelekeo na kimaudhui. Tatizo kubwa naliona kiutekelezaji kutokana na athari za tatizo la umeme ambalo limeanza kutukumba. Wenzangu wameliongelea kidogo. Mwaka jana tukumbuke tarehe 30 Desemba, 2006 Mheshimiwa Rais wa nchi alikuja kulihutubia Bunge alifananisha umuhimu wa nishati ya umeme na chembe za damu mwilini. Mwenye kitabu cha hotuba ya Rais anaweza akafungua ukurasa wa 57. Kwenye ile hotuba, Mheshimiwa Rais alikuwa na haki kabisa kusema hivyo. Wote hapa tunajua athari za mwili kukosa chembe za damu. Vile vile wote tunaweza tukahisi na tukajua athari za upungufu wa nishati nchini, *of course* ni uchumi kuzorota. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, si rahisi hata kidogo kutekeleza kikamilifu bajeti yoyote ile kwa umeme wa mgao. Umeme wa mgao maana yake utekelezaji wa bajeti kwa mgao. Naipongeza Serikali kwa hatua za dharura ambazo imechukua. Nimeona kwenye hotuba ya Waziri wa Mipango, Uchumi na uwezeshaji na Waziri wa Fedha, kwanza kuna kuongeza uzalishaji umeme kwa kutumia makaa ya mawe ya *Kiwira Coal Mine*. Kwa hatua hiyo naipongeza sana Serikali kwa sababu siyo tu kwamba umeme utazalishwa, lakini vijana wangu wa Kyela watapata ajira, vijana wetu wa Ileje na Rungwe Magharibi, watapata ajira kwa sababu ukiongeza umeme na ajira zinaongezeka zaidi katika huo mgodi wa umeme. *(Mako fi)*

Mheshimiwa Spika, katika hatua ya pili tunaambiwa kwamba tutanunua umeme kutoka Zambia, vile vile tutakodisha umeme na vile vile tutaongeza uzalishaji wa umeme

kwa kutumia gesi ya Songosongo. Hizo ni hatua nasema ni nzuri lakini kwa dharura. Hazitatui tatizo la umeme nchini hapa *long term.*

Mheshimiwa Spika, tuna malengo makubwa kweli nchi hii na malengo haya yote yanahitaji umeme wa uhakika, umeme mwingi zaidi. Sasa hivi tuko katika kutekeleza *Mini Tiger Plan 2020* ambayo Waziri wa Mipango, Uchumi na uwezeshaji anatuelezea mara kwa mara. Hiyo *Mini Tiger Plan* inatutaka tupate wawekezaji wengi kwenye maeneo maalum *(Special Economic Zones)* na hizo *Special Economic Zones* zinahitaji kweli kweli umeme. Mheshimiwa Rais amezunguka hivi karibuni nchi nyingi duniani, watu wamemwelewa, wataanza kuja wawekezaji. Wakishakuja wawekezaji wanne, watano wakubwa, tutaanza kutafutana tupate wapi umeme. Haya majenereta ya kukodisha hayatoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunatekeleza *Development Vision* yetu ya mwaka 2025. Sasa hivi tumebakiza miaka 19, maana yake mnaielewa Mheshimiwa Peter Serukamba juzi ameliongelea hili. Ina maana kwamba kufika mwaka 2025 Watanzania tutakuwa *(middle income country)* nchi ya katikati ya kipato au *semi industrialized.* Maana yake ni kwamba kipato cha Mtanzania mmoja mmoja kitapanda kutoka dola 210 za leo kwa mwaka mpaka dola 3,420, ni safari ndefu, safari ngumu lakini safari hii tunaweza kuifikia tukiwa na umeme nafuu, umeme wa kutosha na umeme wa uhakika, bila hiyo tunaota ndoto za mchana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitaka nilisisitize hilo la umeme kwa sababu tuna uwezo wa kufanya hivyo. Ukiziangalia nchi za Asia, niliwahi kusema hili hapa, nchi ambazo zimefikia huko tunakotaka tufikia mwaka 2025 kama Malaysia *per capital consumption* ya umeme ni *watt* 388 sisi hapa leo Tanzania *per capital consumption* ni *watt* 24. Tunahitaji tuanze kujenga uwezo pole pole uweze ufikie hizo *watt* 388. Mwaka 2025 tutakuwa Watanzania pengine milioni 50 pamoja na huu UKIMWI kutumaliza. Milioni 50 kwa hesabu za haraka haraka kwa *watt* 388 tunahitaji zaidi ya *megawatt* 20,000 hapa. Bila kuwa na *megawatt* 20,000 hapa tunajisumbua. Hatuwezi kufanya lolote, tuanze kujenga uwezo huo sasa. *(Makofi)*

Jana nimefurahishwa sana na Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya. Ametueleza alikuwa *Mozambique*. Huko *Mozambique* kiwanda kimoja tu cha kuyeyusha vyuma kinakula umeme *megawatt* 900 yaani mara mbili ya umeme ambao Tanzania nzima inazalisha. Tunaweza tukafika huko na sisi, tunachohitaji ni *strategic planning*. Leo hii nenda kwenye *internet* utaona asilimia 76 ya umeme duniani kote inatokana na *fossil fuels* ukiwemo mkaa wa mawe. Ni asilimia 5 au 6 tu ya umeme duniani unazalishwa na maji kama sisi Tanzania. Watu wanakwepa maji, maji ni ubabaishaji. Twende jamani kwenye mkaa wa mawe. Leo hii Afrika ya Kusini, ambayo tunasema kwamba imeendelea kupita nchi zote Afrika kwa viwanda, zaidi ya asilimia 90 ya umeme wa Afrika Kusini inatokana na mkaa wa mawe. Watalaamu wetu wa *NDC* wanasema sisi tuna mkaa mwingi wa mawe kupita Afrika Kusini. Tuna maeneo 14 Tanzania yenye mkaa wa mawe. Tuutumie, *let us go coal,* tunababaika nini? *(Makofi)*

Nilitaka niseme kitu kimoja kwamba tunaamini mno wazungu, kuna wazungu wamekuja hapa wa *Net Group Solution.* Hawa wametukwamisha kweli kweli kutumia umeme kutokana na makaa ya mawe. Lakini sababu wanazo nzuri wanatetea maslahi ya kwao. Leo hii kiwanda chetu cha *cement* cha Tanga kinatumia mkaa wa mawe kutoka Afrika Kusini, meli kila wiki inatinga Tanga. Lakini tungekuwa tunautoa mkaa wa Mchuchuma. Kiwanda cha Mbeya kinatumia makaa ya mawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jamani tuamke tutumie makaa ya mawe Mungu ametupa tunaukalia tu hivi hivi hatuhitaji mkaa wa mawe kwa ajili ya *Special Economic Zones* au viwanda au maofisi tu, hata vijijini. Tumepata Uhuru mwaka 1961 wananchi wetu nao wanataka mwanga huko vijijini. Jamani umeme utakomboa wananchi wetu vijijini. Uchawi umezidi kule kwa ajili ya giza, ngono zembe zimezidi kwa ajili giza. Hebu jamani tupeleke umeme vijijini tulete *changes*. Mimi nina imani kubwa na Serikali yetu ya sasa, Serikali yetu ikidhamiria kufanya kitu, inatekeleza. Tumekuwa na njaa imetekeleza, imetusaidia Watanzania, tumekuwa na tatizo la vijana wa darasa la saba, Waziri Mkuu na Rais wamesimamia hilo suala, tumefika mbali sana. Tumekuwa na matatizo ya ujambazi tumeyatatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naiomba Serikali sasa hivi, hebu tuache hizi zimamoto *measures* oh! Kajenereta kakuazima sijui nini Zambia hapana, hebu tuweke mkakati wa kuzalisha umeme wa kutosha. *Let us be Africa's power house* hatutakosa mteja wa kununua umeme hapa. *(Makofi)*

Naomba nikimbilie haraka haraka niongelee mambo mengine mawili, matatu katika bajeti hii. Naomba nigeuze ukurasa wa 38 wa hotuba ya Waziri wa Fedha. Ukurasa wa 38 Waziri anasema kuhusu punguzo la kiwango cha ushuru wa mafuta ya taa na Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba hii anasema ana wasiwasi inawezekana kukatokea (*fuel adulteration)* kuchanganya mafuta ya taa na mafuta mengine ya petroli.

Mimi nataka kumhakikishia Mheshimiwa Waziri wa Fedha, usiwe na wasiwasi hilo linafanyika jana, leo na kesho. Linafanyika nchi hii. *Honest business practices* sijui aliondoka nazo Mwalimu! Hakuna. Nchi imegeuka ya watu wa ajabu, ajabu, matapeli, tapeli. Yaani mtu akipewa nafasi kidogo anatumia mara kumi kujitajirisha na kuwafanya wenzake wote wendawazima. *(Makofi)*

Juzi nimemwona Mheshimiwa Cheyo, yeye hakuniona akisukuma gari lake. Ameweka mafuta nafikiri robo tatu ya mafuta ni mafuta ya taa robo ndiyo petroli, ndiyo mchezo wa kila siku. Waheshimiwa Wabunge magari yenu hayo mliyonunua, anzeni kununua baskeli sasa, yata- *knock* yote kwa ajiili ya hii biashara ya mafuta ya taa kushuka bei. Tutachanganyiwa tu. Kutokana na hali ya nchi yetu kwamba watu hatujawa *honest* kabisa unapewa nafasi ndogo unaitumia kwa ajili ya ubinafsi tu. Siyo tu kwenye biashara hata kwenye siasa ukipata nafasi kidogo basi ndiyo kila kitu humo na biashara zako humo humo. Hatujawa *honest*. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tukiweka unafuu wa namna hiyo nilikuwa napendekeza Serikali vile vile itoe *enforcement mechanism*. Nilikuwa napendekeza kwa mfano suala la mafuta ya

taa tuipe uwezo zaidi *TBS.* Waziri anayehusika alete hiyo sheria hapa tuifanyie *amendment*.

Mheshimiwa Spika, *TBS* tumeshasoma kwenye magazeti inakikuta kituo cha mafuta. Nilisoma *news* wiki iliyopita kuwa *TBS* wamegundua vituo vitatu vya mafuta Dar es Salaam vikichanganya *diesel* na mafuta ya taa, *petrol* na mafuta ya taa. Wanaitwa waandishi wa habari, ndiyo mwisho wa *TBS.* Hawana madaraka zaidi ya pale. Wanapeleka *suggestions* zao kwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko. Kama Waziri amesafiri kwenda India mwezi mzima, basi jamaa wanaendelea tu kuuza hayo mafuta ya taa yaliyochanganyika na *petrol*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuwape meno *TBS.* Wakikuta kama kituo cha mafuta kinachanganya mafuta, wawe na uwezo wa kukifungia hicho kituo cha mafuta. Bila hivyo tunafanya utani. Hii Tanzania imebadilika sana. Mimi mara nyingine nafikiria kwamba kama Marehemu Mwalimu Julius Nyerere angefufuka leo, angetucharaza kweli na bakora hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 45 Mheshimiwa Waziri, anaongelea kuhusu kodi ya sukari. Nataka nimweleze Waziri wa Fedha hapa, Wilaya ya Kyela katika jimbo langu la uchaguzi wote tunatumia sukari ya Malawi, Rungwe, Ileje, Mkoa mzima wa Mbeya, Iringa, Ruvuma tunatumia wote sukari kutoka Malawi na Zambia kwa sababu uzalishaji wa sukari hapa kwetu ni mdogo mno. Hatuioni sukari ya Tanzania. Lakini kinachosikitisha zaidi ni kuwa hiyo sukari tunayotumia Ma-*RPC* wote wanatumia, wote wakuu wanatumia ni sukari ya magendo. Tuseme ukweli. Inaingia kwa njia za panya kwa sababu tumeweka kodi kubwa mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuwe *realistic* na huu mchezo umeendelea muda mrefu. Inatisha kwamba Serikali yetu haipati chochote kwa sababu tumeweka kodi kubwa mno. Tushushe kodi vijana wetu wapitishe sukari kwa njia sahihi maana tunaelewa hatuwezi tukazalisha sukari ya kutosha kukidhi mahitaji ya Mikoa hiyo ya Kusini. *(Makofi)*

Vile vile ningependa kumshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba tuwashushie kodi vijana hawa wanaoleta sukari kwa baiskeli, waingize bure. Lakini wenye malori ndiyo walipishwe kodi kubwa. Kwanza hiyo itakuwa inakidhi hata mustakabali wa CCM na kutaka vijana wengi wapate ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie haraka naona muda unakwenda. Jana Mheshimiwa Aggrey Mwanri alinifurahisha sana na Wabunge wengine, hasa kuhusu suala hili la *air time*, suala la kuongeza ushuru kwa matumizi ya simu za mkononi. Nafikiri huu siyo muda muafaka na ningemwomba Waziri wa Fedha sababu aliyoitoa siyo nzuri, aiondoe kabisa. Anasema tunaongeza ushuru ili kiwango kikalibiane na kiwango cha asilimia 10 kinachotozwa Kenya na Uganda. Hiyo siyo sababu nzuri hata kidogo. Kama Waziri wa Fedha, unataka kuanza kulinganisha linganisha vitu hapa basi linganisha mishahara ya Wabunge wa Kenya na Watanzania. Ipandishe kama tutafika. Kenya ni maji marefu tuachane nao, tusijilinganishe. Tunahitaji sisi *rates* zile zile tafadhali sana kwa sababu tunahitaji simu hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la ushuru wa mifuko ya *plastic.* Nashukuru kwa sababu ambazo Serikali imetoa. Lakini nataka kusema kitu kimoja, tume-*rush* mno kuweka ushuru mkubwa. Viwanda vingi vitafungwa, tutapoteza ajira na huku tumeahidi vijana wengi kuwapa ajira katika miaka hii mitano. Tuwape *challenge* hawa wenye viwanda. Kila mtu mwenye kiwanda cha *plastic* ajenge *plant* ya ku-*recycle* hiyo *plastic* na vile kila mtu awe na brigedi ya vijana kuokota hizo *plastic*. Tunahitaji ajira jamani. Tukifunga funga hivi vitu na kuweka kodi za ajabu ajabu, tunapoteza ajira.

Mheshimiwa Spika, nimalizie la mwisho kabisa, ikinigongea kengele basi nitaongelea wakati wa Waziri mwenye dhamana au anayehusika. Ukurasa wa 41 mpaka 45 Waziri anaongelea kuhusu marekebisho ya ushuru wa forodha wa *East African Community*. Bila kutueleza hatma ya malalamiko halali ya Watanzania wenye viwanda vya dawa baada ya Kenya kukiuka. *Common External Tariff* ya Afrika Mashariki. Halafu Watanzania tukaenda pale Waziri wetu mmoja sijui tukoje sisi, badala ya kutuuliza Wabunge wa *East Africa* tuliokuwepo pale jamani nifanyaje, kesho akaenda akakubaliana na uamuzi wa Kenya kukiuka masharti ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeingia kwenye hasara kubwa Tanzania na lazima Serikali ijibu hilo swali. Tukishindwa kulijibu basi tuwaruhusu wafanyabiashara wa Tanzania waende mahakamani wadai fidia. Kwa sababu ni *irresponsibility* ya hali ya juu. Kwa sababu tume- *negotiate Protocol* ya *East African Community* kuhusu *customs* miaka mitano usiku kucha, anakuja mtu Waziri mmoja tu sijui kwa misingi gani anakuja na kuiruhusu Kenya kuingiza dawa. Sasa tumekuwa *affected.* Viwanda vyetu hapa vinakufa kwa ajili ya dawa zinazopitia Kenya kuingia humu. Hatuna *market,* tena Serikali ina wajibu kulisikia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kusema kwamba naunga mkono hoja hii lakini nategemea Serikali itazingatia *constructive comments* za Wabunge wote. Ahsante sana.*(Makofi)*

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii na hasa zaidi kuwa mtu wa mwisho kuchangia katika mjadala wa leo. Lakini kabla sijaanza naomba niwasilishe salaam za shukrani za wananchi wa Wilaya ya Chunya. Wananchi wa Wilaya ya Chunya, wanaishukuru sana Serikali kwa msaada wa chakula ambacho walipelekewa, wanaishukuru sana. Lakini wameniomba vile vile kwamba ile njaa ambayo iliwakumba mwaka huu bado inaendelea na bahati nzuri Serikali ya Wilaya inafanya tathmini sasa hivi, baada ya kutathmini nafikiri tutaleta maombi kwa njia ambazo ni muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo vile vile naomba nichukue nafasi hii, kwa kuzipongeza hoja zote mbili kwa jinsi ambavyo zimeletwa hapa kwetu. Kitu kimoja ambacho pengine ningeweza nikakiongelea ni ule wasiwasi ambao wenzangu wengi wameuzungumza na ni katika utekelezaji. Ninavyofahamu mimi mipango yote ya maendeleo huwa kuna baadhi ya hatua ambazo lazima ziangaliwe kwa undani zaidi.

Kwa mfano, kuna miradi mingi sana ambayo ilitokana na mipango kama hii ambayo sasa hivi tunaizungumzia. Tulikuwa na miradi ya viwanda vya kusindika, tulikuwa na viwanda vya kubangua korosho, ambavyo vingi vilijengwa huko Kusini mwa nchi yetu, viwanda vya nguo, mashamba ya *NAFCO* na mengine mengi tu yote haya yalikuwa yamepangwa kwa lengo la kuleta maendeleo.

Lakini sasa hivi maeneo mengi tunayaita kama ni magofu hatimaye ndiyo tunakuja kuanza kuzinduka kwamba tubinafsishe, lakini yote haya kwa nini yanatokea ikiwa kama kweli tulikuwa tunaangalia vizuri wakati wa kuyapanga. Mimi nilikuwa nafikiri kwamba kama kweli mipango yetu inatakiwa kukamilishwa basi ni lazima tuzingatie zile hatua zote ambazo zinatakiwa wakati unapoandaa huo mpango wako. Lazima kuwepo na maangalizo kuona je, mpango huu utafanikiwa ama hautafanikiwa. Tusije tukaingia yale matatizo yote ambayo tayari tumekwishapata kama vile tulikuwa na *RTC,* tulikuwa na mambo mengi tu na *NMC* yote haya yamepangwa na tukayapokea lakini katika utekelezaji wake imekuwa ni vigumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunaanza kukumbushana kuhusu kuhamia Dodoma. Ni mpango wa siku nyingi, lakini tunasita, tunasitia nini wakati tukiamua hatukujua kwamba kunaweza kukawa na matatizo? Basi mimi nilikuwa nafikiri kwamba mpango huu kwa imani ambayo ninayo kutokana na ari, nguvu na kasi mpya ambayo tunayo nina imani kwamba tunaweza tukautekeleza na hasa zaidi nikiangalia Baraza la Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais aliyepita wa Serikali ya Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, alilipa jina lile Baraza lake kwamba ni askari wa miavuli. Mimi kwa imani yangu, Baraza hili la Mawaziri mimi labda nilipe jina kwamba ni askari wa medani. Askari wa medani kazi yake tumeshaiona ndivyo tunavyoona wanavyofanya hii kazi ambayo tayari limeshaanza kufanya ikiwa ni pamoja wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, ndiyo kazi za medani, nina imani kwamba mipango hii ambayo tunaiandaa itatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niingie katika Wilaya yangu ya Chunya, mwenzangu amezungumzia kwa kirefu tu jinsi gani sisi Wabunge tumeanza kushughulikia Wilaya ya Chunya, kwa kweli inasikitisha. Nakumbuka toka tupate Uhuru Mawaziri ambao wametembelea Wilaya ile hawafiki kumi. Sasa sijui kwa nini hii Wilaya imetengwa. Sasa matokeo yake ni kwamba hii Wilaya iko nyuma sana kwa kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukichukua upande wa elimu hebu tujaribu kuangalia madaktari katika ile Wilaya ni wachache sana. Kwenye jimbo langu ambalo natoka, tuko madaktari watatu tu, inasikitisha sana. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba kwamba Serikali ya Awamu ya Nne ijaribu kuiangalia ile Wilaya na iingizwe kama Wilaya nyingine. Wilaya ya Chunya, tuna mambo mengi sana, tuna shughuli za utalii ambazo hazijaanza hata kule kuguswa, tuna Bonde la Ziwa Rukwa, tuna shughuli za kilimo ambazo hivi tunavyozungumza kwamba kuna mpango wa kukuza uchumi kupitia kilimo, Wilaya ya Chunya ina nafasi nzuri sana ya kuweza kufanya hivyo. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali ya Awamu ya Nne, iangalie Wilaya ya Chunya na iipe uwezo wote. *(Makofi)*

Naomba nichukue nafasi hii, vile vile kuwashukuru baadhi ya viongozi ambao waliamua kuitembelea Wilaya ya Chunya, ni wachache sana ambao ni Mheshimiwa John Malecela alishafika kule, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, alishafika nahesabu kwa sababu ndiyo hali halisi nataka nionyeshe ugumu wa Wilaya ile na kitu wanachokikimbia ni hali halisi iliyoko kule ya miundombinu wanapokuja, wanakuja moja kwa moja mpaka Chunya, Chunya wanazunguka wanafuata ile barabara ambayo inaweza ikapitika. Lakini hawajawahi kwenda vijijini ni kwa sababu ya hali halisi ya ubaya wa eneo hilo. Namshukuru Mheshimiwa Joseph Mungai, naye alikwenda lakini yeye alijitahidi mpaka akafika kwenye kijiji cha mwisho kabisa cha Ngwala nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala moja ambalo kwa kweli huwa linatatiza katika utekelezaji wa mipango yetu yote. Kuna kikundi ambacho kwa kweli ndicho kikundi kinachofanya kazi na kikundi hiki ni cha Madiwani, watendaji wa maeneo ya vijijini. Hiki ni kikundi muhimu sana lakini tumekisahau. Wenzangu wamekizungumza na mimi nataka nikizungumzie kwa uchungu kabisa kwamba kikundi hiki cha Madiwani, watendaji naomba Serikali ya Awamu ya Nne, isianze kungojea kwamba sijui tufanye mwaka kesho kikundi hiki ndicho ambacho kinatekeleza maagizo ya Serikali. Lakini maslahi yake inasikitisha sana. Unakwenda kumpa Diwani shilingi 30,000 kwa mwezi. Sasa ukichukue mfano Diwani ambaye anatoka Ngwala maili 170 kuja Makao Makuu ya Wilaya. Nauli yenyewe ni shilingi 30,000 hizo hizo sasa huyo mtu atapata nini? Atakuwa na motisha ya namna gani huyu mtu? Kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali ya Awamu ya Nne iliangalie hili kwa makini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo la walimu limezungumzwa kwa kirefu sana na wenzangu, lakini kuna maeneo mengine kwa kweli inasikitisha, unakwenda unamkuta mwalimu mmoja anafundisha wanafunzi 140 kwenye kipindi, hilo siyo darasa huo ni mkutano wa hadhara. Sasa kwa kweli inasikitisha sana. Lakini naishukuru Serikali hasa Wizara hivi sasa ambayo imeamua kulivalia njuga hilo tatizo. Ni kitu ambacho kwa kweli kinasikitisha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, wenzangu wameshazungumza faida ya kuwa na Kiwanja cha Kimataifa kule Songwe, wameshazungumza na mimi naomba nisisitize tu kwamba ili kusudi tupate mafanikio makubwa katika kiwanda kile, basi ni lazima tuboreshe miundombinu. Miundombinu ndiyo itakayotusaidia kupata faida kutokana na kile kiwanja. Tunavyo vivutio vingi sana kuna milima ya *Livingstone* ambayo hifadhi yake bahati nzuri tumekwishaanza kuiwekea mikakati, tuna milima mingine kule kwenye Jimbo la Chunya. Wilaya ya Chunya ina milima ambayo ina vivutio vya kila aina. Waheshimiwa Wabunge kama mnataka kuona maajabu basi mimi nawakaribisheni katika Jimbo langu niende nikawaonyeshe. Kuna kuku wa mguu mmoja anatembea kule. *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Ni maajabu!

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nimesema kwamba ni maajabu, kuna maji yaani unaweza ukafika mahali ukakuta maji yanaporomoka. Ukitamka kwamba ni maji yanageuka yanakuwa damu kwa hiyo ni baadhi ya vivutio vizuri. Vitu hivi kama tuvitengeneza ni vivutio vikubwa sana, ni vivutio vizuri kwa watalii. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara ya Maliasili na Utalii ifanye utaratibu angalau kuja tu kuangalia. Tutakuja kuwaonyesha halafu mtakuja kuona ninyi wenyewe ni jinsi gani mnavyoweza kusaidia utalii katika eneo hilo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kilimo wamekizungumzia kwa urefu sana wenzangu, lakini suala la kuongeza tija katika kilimo ni kukifanikisha. Tunapozungumzia *sustainable agriculture* ni pamoja na vitendea kazi kama matrekta, sisi kule hatutaki mambo mengi sana Wilaya ya Chunya, kuna *draught animal*, wawe na mipango ya kuweza kukuza kilimo katika kutumia rasilimali ambazo tunazo kama wanyama, tunao punda wengi tu kule kama tukiwa na sehemu ya kuwafundisha hawa punda wanaweza wakafanya kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nafikiri suala la kilimo ni kama lilivyozungumzwa na wenzangu kwamba haliwezi likawa endelevu ikiwa kama hatutachukua hatua za kuimarisha. Katika Wilaya kuna maeneo ya uwindaji, nasikitika kwamba wale wawindaji ambao wako kule ule utaratibu ambao ndiyo unatakiwa wa kuwa na *blocks* zao sasa hivi unakiukwa, kuna *open areas* ambazo ndiyo zinatengwa kwa ajili ya wananchi, kwa ajili ya watu wengine ambao wakifuata taratibu basi wanayatumia yale maeneo.

Mheshimiwa Spika, lakini sasa hivi yale maeneo yamekuwa *annex* kwa hiyo inakuwa tu kwamba mwananchi sasa anakuwa katika hali ya utumwa, akitaka kuingia pale inabidi lazima aende kwa yule mwenye *block*. Sasa eneo ni la kwake na lilitengwa pale kwa madhumuni kabisa kwamba liweze kuwasaidia hawa watu wengine wasiokuwa na uwezo mkubwa lakini sasa hivi yameingiliwa. Namwomba Waziri anayehusika ajaribu kufanya utaratibu kama anaweza akaja kule tukamuonyesha hayo maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa na mimi kwa sababu ni mara yangu ya kwanza niweze kutoa shukrani kwa wananchi wa Jimbo la Songwe, Wilaya ya Chunya kwa kunifanikisha leo hii kusimama mbele ya umati huu. Nawashukuru sana hawa wananchi na kama nilivyowaahidi kwamba ugeni ndio tumeuanza, lakini kadri utakavyokwenda nina uhakika kwamba tutakuwa na mafanikio makubwa katika Jimbo letu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kulingana na shughuli ambazo zitafuata hivi punde, hapa ndiyo mwisho wa shughuli zetu kwa asubuhi hii. Napenda tu kukumbusha kwamba ingawa haionekani hivyo kwenye ratiba. Waheshimiwa Wajumbe wote wa *Steering Committee* ya Bunge na Makamishna wote wa Tume ya Huduma za Bunge watakuwa ni sehemu ya uwakilishi wa mapokezi pale nje ya Ukumbi wakati ambapo

Waheshimiwa Wabunge wengine watanyoosha nyosha miguu kidogo lakini wabaki katika Ukumbi. *(Makofi)*

Shughuli za mapokezi ni fupi sana baada ya mgeni wetu Mheshimiwa Rais wa Ireland kuja akisindikizwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, watakuwa na dakika kama 15 tu za shughuli zote zile za mapokezi pamoja na nyimbo za Taifa. Baada ya hapo nitawaleta humu Ukumbini.

Waheshimiwa Wabunge, mtaona kwa makusudi sikusema nitawaingiza kwa sababu nimejifunza maneno hayo hayastahili. Kwa hiyo, nitawaleta humu Ukumbini kwa kuongozwa na *Serjeant-At-Arms*, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote kwa heshima ya mgeni wetu tuweze kusimama wakati *procession* hiyo inaingia na baada ya hapo Mheshimiwa Rais wa Ireland nitamwomba kwa niaba yenu azungumze na sisi na atazungumza nasi.

Hotuba yake ni fupi tu, ni kama nusu saa hivi na baada ya hapo tutakwenda nje kupiga picha kwa utaratibu ambao umeonyeshwa hapa kwenye ratiba.

Waheshimiwa Wabunge, saa 11.00 jioni kikao chetu cha leo kinaendelea ambapo Msemaji wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Chacha Wangwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Chomboh na baada ya hapo Mheshimiwa Hassan Kigwalilo. Naomba wajiandae kwa saa 11.00 jioni. Kwa sababu mara nyingi Waheshimiwa wanajivutavuta kuja saa hizo na kwenye kiti hapa atakuwepo Mheshimiwa Naibu Spika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, ooh ni kweli nimekumbushwa kuhusu kutengua Kanuni. Kwa taarifa yenu wakati huu ambapo Mheshimiwa Waziri Mkuu kaenda kuwapokea wageni Uwanja wa Ndege, Kaimu Kiongozi wa Shughuli za Bunge ni Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib na kwa hiyo basi namwomba yeye aweze kusimama kutoa hoja ya kutengua Kanuni ili kuwaruhusu wageni wetu waweze kuingia. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kutoa hoja kwamba Fasili ya 1, Kanuni ya 114 itenguliwe ili mgeni wetu rasmi, Rais wa Ireland pamoja na mwenyeji wake waingie Ukumbini na kuhutubia.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge liliafiki kutengua Kanuni ya Fasili ya 1, Kanuni ya 114 ili kuwaruhusu Wageni wasioruhusiwa kuingia Bungeni kuweza kuingia ndani ya Ukumbi wa Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, Kanuni imetenguliwa kuwaruhusu wageni wetu kuja hapa Ukumbini. Baada ya Tangazo hilo sasa nasitisha Shughuli za Bunge kwa muda mfupi sana kama robo saa tu ili saa sita kasoro robo tuweze kuendelea na shughuli ya kumpokea mgeni. *(Makofi)*

*(Saa 05.35 asubuhi Bunge lilisimisha shughuli zake kwa muda)*

*(Saa 06.04 mchana Bunge lilirudia)*

*(Here the President of Ireland and the President of the United Republic of Tanzania, H. E. Jakaya M. Kikwete lead by Speaker enter the Chamber on procession)*

**SPEAKER:** Your Excellency Mary McAleese, President of Ireland, Your Excellency Jakaya Mrisho Kikwete, President of the United Republic of Tanzania, Honourable Edward Ngoyai Lowassa, Prime Minister of the United Republic, your Excellencies Members of the Deplomatic call, Honourable Ministers, Honourable Members of Parliament, invited guests, ladies and gentlemen.

On behalf of the Parliament of Tanzania, I am most humbled this morning to welcome to this August House a highly distinguished citizen of the World and the Leader of the friendly National of the Republic of Ireland, Her Excellency Mary McAleese. *(Applauses)*

In welcoming your Excellency into this Parliamentary Chamber, we note how appropriate it is that the first foreign dignitary to address us here in this new Parliamentary Chamber represents a nation with which we enjoy the most cordial of relations. We thank your Excellency and your delegation. We thank your Excellency and your delegation for this honour. *(Applauses)*

Your Excellency, kindly allow me now to introduce your Excellency to Honourable Members of the House. Honourable Members of the Parliament, Her Excellency Mary McAleese is the eights President of the Republic of Ireland. First elected in 1997 and re-elected to save a second term in October, 2004. *(Applauses)*

Her Excellency is a Barrister and former Professor of Law. She was born on the $27^{th}$ of June, 1951 in Belfast. Birth day soon to be, this is $22^{nd}$ of June, so in five days, we can say Happy Birthday. *(Laughter/Applauses)*

Her Excellency Mary McAleese is married to Dr. Martin McAleese, whom I will ask to rise. He is in the Speaker's Chamber. *(Applauses)*

And the union is blazed with three children. Your Excellency, on behalf of the Parliament of Tanzania I thank you, Your Excellency for making the long journey to

Tanzania and to Dodoma in particular to address this Parliament. My life knowledge and experience tell me that there is no borders and no doors that friendship can not cross. *(Applauses)*

Your Excellency's visit to Tanzania demonstrates that the relationship and friendship between our two nations will continue to flourish for the benefit of our people's of our two countries. It is now my honour and privilege to request Your Excellency to address the Tanzanian House of Parliament. *Karibu! (Makofi)*

**SPEECH TO THE MEMBERS OF PARLIAMENT DELIVERED BY H. E. THE PRESIDENT OF IRELAND**

**H. E. MARY McALEESE:** Mr. President, Honourable Speaker of the House, Prime Minister, Ministers, Members of Parliament and distinguished guests. Nina furaha kubwa kuwa hapa Dodoma leo na kuwa na nafasi ya kuhutubia Bunge. *(Makofi)*

I am so happy to be here today in Dodoma and I have such an opportunity to address each of you in this magnificat new chamber. *(Applauses)*

Here in this magnificient new chamber, this place where Tanzania's political leaders gather for the hopes and dreams of a nation, gather too for the future of a nation, is debated and crafted and I feel very deeply privileged to be the first visiting foreign Head of State to speak here today. I am so grateful to you for the invitation. And as I look round the chamber and I see such great gender balance. I long for the day when I see in my own Parliament. *(Laughter/Applause)*

I came to this great continent almost two weeks ago, visiting first Lesotho then Mozambique before arriving here in Tanzania a few days ago. I came as a student to learn more about each of these very distinctive of countries in this extra-ordinary continent and I came as the first citizen of a nation which has for many, many, many generations now been a firm friend to the people of Tanzania. *(Applause)*

So although I arrive as a stranger, I know from the warmth of the welcome that we have received through out of our visit that the people of Tanzania and Ireland hold each other and the highest regard and have greatest perfection from one another and have an instant capacity for friendship and I have experienced that. *(Applause)*

I have also in this few short days been able to experience just how exquisitely beautiful this country is already, I can say over I have been President of Ireland now for nine years. But I have to say that my visit to this country taking in all it is amazing site and absolving as friendship and landscapes nothing compares. *(Applause)*

For these nine years now I have good fortune to be my country's first ambassador, travelling around the world in the name of Ireland, strengthening, refreshing and renewing Ireland's international links and reaffirming our centuries solidarity with those in the developing world for whom life is such a very hard struggle.

In some respects, the developed part of planet earth has a rather narrow view of the huge continent that is Africa. Too often it is referred to as if it were one country, its 54 nations and 2,000 languages amazing people's packed into a one size fits or image. What is more those perceptions are often hardened and virtually exclusively defined by Africa's failures rather than its successes, it problems rather than its progress towards their resolution. *(Applause)*

Just as Europe is not comprehensively defined by Srebrenica and Beslan, or indeed my own country can not be defined exclusively by the conflict in Northern Ireland, neither should Africa exclusively be defined by the many tragedies of Rwanda, the DRC and Darfur. Overpoweringly grim though they are and righteously demanding of pan-African and international attention, but in and above themselves constitute, they can not tell fully the story of contemporary Africa. *(Applause)*

There are other realities which need African champions to articulate them to a wider world for when the West interests itself in Africa more often than not the voices of Africa's leaders are absent. And I hope you the representatives of a leading African country will seek to ensure that voice of hope. The voice of hope have been done, the voice of successs you have achieved, the voice of the steps that manifestly taken the country up to drag out poverty. i hope that voice get sad, is the hard work challenges the one dimensional image of this infinitely varied continent as you change the future of your own country by bringing confidence through tangible progress. I hope in my own country and the European Union to be a voice brings word and brings the story of the change. In these few days we have seen a new generation who have the chance to go to school. *(Applause)*

There is one who asked today to talk to the Masai elders in Arusha and to heir them tell me passionately they know, they believe education is the key to their future. To see new generation of farmers, of entrepreneurs and industrialists a new generation of political leaders, men and women who are attempting to build an egalitarian society and ethically based society, civic society that focus the job, a peaceful about poverty and disease elimination, job creation, underpinned by fair and just government. A place for true juniors of every individual can flourish and blossom with it impairment. *(Laughter/Applause)*

This is difficult story to write we now learn to know only too well because is not so long ago since new story to, but we know the Tanzania is leading by example with a clear and measurable roadmap for the development of your country and your people. Building on previous national development plans, MKUKUTA is one of the most progressive and inclusive in all of Africa. We recently in Ireland, with objectives of that plan, investing in human potential, because in Ireland our human resource, the biggest resource we in all of Ireland is our people. And I think the same as here. And we invest them through increase focus on education illiteracy, the key to themselves, the key to the on generous the provision of better health services, the fight against HIV/AIDS. The flight against deseases in general, the concentrates on job creation, livelihood generation and consistent economic policy and planning.

And crucially, MKUKUTA makes a clear political commitment to democracy, inclusive government and improved accountability.  And those efforts are beginning to demonstrate real and lasting positive results.  And we encourage in this work and support you strongly in this endeavour.  *(Applause)*

We congratulate you in the work in the terms recent health improvements in malaria prevention and treatment that well as that well as immunisations and nutrition all which are leading to very significant reductions in infant and child mortality.

Huge progress amazingly impress progress in the field of  primary education with enrolments growing to 7.5 million in 2005, an amazing story.  95% of your children aged between 7 and 13.  And we in Ireland know, what a journey that takes a country because it was the key to our own current prosperity.  *(Applause)*

As a result of course, of all the efforts you have made, Tanzania is likely to be one of only a few African countries to attain the Millennium Development Goal of Universal Primary Education. You should so be proud.  And that is of course is major achievement transforming the lives of millions.

We in Ireland remember the change in education made for us  back 1967 we were very very poor country we were not the Members of European Union that was some five years away, six years away, but in differ we joined the Union those few years later we were the poorest country in the European Union.   *(Applause)*

But in 1967 when we had very little money we introduced free secondary level education.  And 40 years later it was though newly educated generations who transformed our system very genius flooded every aspect of life very ambition and so today from being the poorest country inside the European Union we are now one of Europe if not Europe's where first most dynamic economy.  *(Applause)*

And we take great very proud in that transformation we also know a process step by step process.  There was no easy answer, there was no jumping straight into from poor poverty to wealth there was just pain step taken of hard work.  *(Applause)*

And no doubt the Government and the people of Tanzania are impatient as we were, for the social and economic benefits of successful development planning and investment to manifest themselves.  But our experience in Ireland  and guide, we know only little well these things take time to mature to blossom they require ongoing patients the determined implementation of the right policies.  They need both a kind of a strange makes of patients and inpatients.  We need them both an equal measure.  *(Applause)*

Our own development and experience now guides how we work with developing countries, such as Tanzania.  This year Ireland will spend over pound 700 million Euro working with some of the poorest countries in the world to reduce poverty.  Over 80% of that money is spent here on the Continent  of Africa.  It is important to say Ireland has no agenda beyond the elevations of suffering poor we look nothing for ourselves whatsoever.  We do not tie it to anything.  And by anything the  only thing we want say is

Tanzania will have a story to tell and soon like Irelands. That's feel our hearts with joy. *(Applause)*

And I think by any international measure our aid programme represents a huge commitment by the Irish Government on behalf of the Irish people. It is very real and it very practical articulation of the values the Irish people cherish and deep among them is very profound sense of moral responsibility that we feel we have to help to bring hope through help to the world's less fortunate citizens because we too were helped to get to where we are by one of the worlds largest the aid programme from the European Union. *(Applause)*

Honoroauble Speaker, Ireland has been supporting Tanzania since 1979 and in recent years the scale of our assistance to your country has increased. Over the period from the year 2000 to 2006 we provided over 140 million Euro in development assistance to Tanzania - supporting your efforts to reduce your people's vulnerability to drive forward your gender and to help your vision for your county to blossom. *(Applause)*

Our assistance has evolved over the last 25 years, moving from discrete Irish projects and area programmes to supporting the Government and people's nationally owned programmes. And that is important because people of Tanzania are firmly in the driving seat for national ownership of the development agenda and programmes we know that is the most effective way to move towards sustainable national towards national some we wish you well on that. *(Applause)*

This new way of working , this new way of engage we have is reflective of the trust that we place in you and your Government. It is reminiscent of the trust that the European Union placed on the Irish Government and the people when we joined in 1973 and became a large recipient of European aid and structural funds. We put them to very good use. We use to create a sustainable dynamic at the heart of our economic life. Building a hard infrastructure investing in schools investing intellectual infrastructure by far the most important investment we ever made. And today Tanzania faces the challenge of how best to effectively and qualitatively manage the very large flows of aid into your country as we also did.

And Ireland strongly supports the Government of Tanzania's intention to sign an agreement on enhancing the way at works with all donor countries, including Ireland. This agreement, the Joint Assistance Strategy, is a national, medium-term framework for managing the relationship between the Government of Tanzania and donors and we hope and pray that we will improving the way aid can help national development and reduce poverty. So whilst MKUKUTA describes what actions will be taken to address Tanzania's development challenges, the new Joint Assistance Strategy describes how within that framework Government and donors can work together to deliver the results that we all want to see happen. But most important their role the people of this lovely country need to see happen. It is utterly vital that all future aid takes on that sharper edged focus which will make much more systemically effective and I wish all the parties

to the agreement every success over the coming years. The partnership between our two countries of course goes far beyond the relationship between our two Governments.

Long long before the establishment by the Irish Government of a programme of official assistance. Irish missionaries and lay volunteers dedicated their lives and talents to Tanzania. They built schools and hospitals, they invested in community, they built lasting bridges of friendship, solidarity and joyful mutual curiosity between our two worlds. And we have both been great beneficiaries of that efforts. *(Applause)*

In more recent years new connections have been made. Since 1997 for example, the University where I taught law for a number of years, Trinity College in Dublin and the University of Dar es Salaam have jointly organised the programme on Constitutionalism for the Judiciary of Tanzania. And through this programme Judges from both Tanzania and Ireland have had the chance to visit each other's country to investigate each other system to share the experiences and to pull the knowledge and in that way to deeply and reach both judiciaries and both countries are we very grateful for those the kind of the partnership makes real against Ireland value for all of us from the resource knowledge to share the experiences.

Tanzania's geographical location at the heart of this great continent confers on it a key role in the Great Lakes Region, a region which has struggled to emerge from a tragic period of conflict. You have provided a safe heaven for thousands who fled conflict and murderous genocide on your borders and you host an international court I visited yesterday, that is seeking to end impunity and hold countable those who will responsible for some of those crimes. Your long role in the antiapartheid struggle is widely widely recognised and respected. *(Applause)*

We in Ireland and Europe we rely on you and we urge you to take that lead that you have always taken to continue to take that lead as the country which has always promoted peace always promote stability in the region. A country which stands as an ankle of peace and very tabulate times. *(Applause)*

We support you on your efforts to strengthening the role of regional institutions which can be so important to the strengthening the peace making capacity of the continental goes forward. We in Ireland know the value, the very important value of regional unity; it has served us extremely well. It has made of the European Union wants the place of the most better better enemies and those of you who are old enough would remember have the first part of the 20th century so Europe disseminated itself.

The second World War 57 million died as the result of man inhumanity to man and inability to resolve differences by simple negotiation. At the end of those wars we still had to face those differences and we still had to negotiate and end them. The European Union grew out of that, out of that deep woundness in people that all for signs of the draught full waste, and that determination that Europe could never waste its children in that way again. We know you have the same will for all of Africa. There could be no longer waste to children and its talents in worseness conflicts. But do what

you do here in this Parliament bring here your differences, talk about them, argue about them, yes, but resolve them. *(Applause)*

Resolve in the many way up left the human person, up left the dignity of the human person and make us so much stronger. And I am sure a strong African Union will do the same for you as European Union has done for Europe. Initiatives such as the African Peer Review Mechanism has also shown how African countries, cooperating within the regional framework of the African Union, can work together to improve governance on the continent. One shoulder to the wheel is an important shoulder but two or three shoulders to that same wheel and the job done much more quickly. *(Applause)*

Two days ago I visited the sites of the former slave market in Zanzibar and a horrific and dreadful place it is. As it should be as to remind all of us we will never forget as for we human beings are capable of and what is important to this that are all champions over people to say that is not a human decent way to live.

There are those who championed the end of slavery or all who championed the end of imperialism so often they spoke as long voice for long long time regardless renegades But ultimately truth and goodness truancy. To visit our place here us today to see the bronze memorial there that depicts a young family in chains. It reminded me in fact looking out over very very similar bronze memorial that sits on the banks of the river Liffey in our capital city Dublin, and it to pick very tragic Irish family ragged and bare and emaciated being driven from our country from Ireland by famine. Because she probability now 1800 our country was revered by famine. People died and even our people died from hunger and three million over paid of time emigrated reducing our population from 8 million to 4 million. *(Applause)*

We still 150 years later believe or not we have for the first time over 150 years reversed the tide of immigration in the last decade for the first time it just shows you how long these things continue and reflex. *(Applause)*

So both our countries share a history of poverty and of deep oppression. Both our countries have come a great distance since those dark days though it is self-evident that Ireland is at last enjoying the prosperity and peace, the influential role in European and global affairs that frankly so many generations went to their graves despairing of. We know the malaise the long standing malaise the psychological lonely of spirit that comes from fighting so many of this historical burdens. We also know the energy that comes from transcending and the truth that is they can be transuded at ex leadership at ex live at ex never giving up but ex makes passions and impassions but it happens when good people decide that is going to happen it does happen. *(Applause)*

And we wish the same for you that we wish for ourselves and for the people of Tanzania and while no-one-can go this journey for you, that is your journey to go. That we promise we will go the journey with you. As you work to reveal your country’s truth potential but lays in the heart of each child but manage women make them strong, you

make the family strong, make the family strong, the community is strong, make community strong the country is strong. *(Applause)*

And please be assured that you have a true friend a long long friend here for a long whole and a partner in Ireland. *(Applause)*

Honourable Speaker, my visit to Tanzania, to your magnificent land and to your gorgeous people has been just far far to breathe. But except me have been enough to send me back to my own country so impressed so reassured by what I have seen and experienced probably to tell everybody I meet when I go back to take all those experiences to put them into some kind of vocal form and to tell of the story or the remarkable story of this country, step by step changing its future. *(Applause)*

And am very proud within this chamber I have been given the opportunity to meet those who are the primary architects of the future of that new tomorrow. You are the custodians of the children's future, you are the custodians of Tanzanian's future and in the name of Ireland I wish you success and I wish you well, I wish you deep personal for fulfilment and I wish you every success and that journey. *(Applause)*

*Ahsanteni sana.* Thank you. *(Applause)*

**SPEAKER:** Excellency Members of the House, invited guest, before I request the Honourable Prime Minister, to move a vote of thanks, I have on your behalf, on behalf of the House, a small souvenir for Her Excellency President Mary McAleese which I shall shortly present. *(Applause)*

I just show the members, Waheshimiwa Wabunge hii ni picha ya Mheshimiwa Rais wa Ireland, pamoja na jengo, imechorwa na msanii hapa hapa nchini kama maandalizi yetu ya kumkabidhi mgeni wetu. *(Makofi/Vigelele)*

We are presenting the picture to Her Excellency the President of Republic of Ireland with a drawing, I think its accurate. *(Applause)*

**H. E. MARY McALEESE:** Thank you so much, thank you. That is beautiful. I look younger.

**SPEAKER:** Honourable prime Minister for vote of thanks.

**HON. PRIME MINISTER:** President of the Republic of Ireland H.E. Mary McAleese and Dr. Martin McAleese, President of the United Republic of Tanzania H. E. Jakaya Mrisho Kikwete, Speaker of the National Assembly Honourable Samuel Sitta, Honourable Ministers, Honourable Members of Parliament, invited guests, ladies and gentlemen

It's a great honour to have this opportunity to move a vote of thanks on behalf of the Members of Parliament of the United Republic of Tanzania. Today as Right Speaker

said we are privileged to have the first foreign President to address Members of Parliament after the 2005 general elections. This is not only a great honour to this august assembly but it is also a manifestation of the strong bond of friendship in our bilateral relations. We welcome you to our country and Dodoma in particular. We are grateful for your visit. Your speech has been very inspiring and indeed very moving. I have learned something new in development you require both impassion and passion. Thank you so much. *(Applause)*

Your Excellency, we received with great sadness the untimely death of our friend, the former Prime Minister of Ireland, Honourable Charles J. Haughey. The late Honourable Charles J. Haughey worked with great devotion to the development of his country and maintained a strong relationship with other countries including Tanzania. He will be remembered not only by the Irish people but also by the people of the United Republic of Tanzania for his profound contribution to the development of his country, and other Nations of the World. During his term, relations between Tanzania and Ireland remained cordial and strong. May God rest his soul in eternal peace and grant patience to the bereaved family and the peoples of Ireland.

Your Excellency, As President Kikwete said to you, your visit to Tanzania has further consolidated the long standing and historical ties of friendship that so happily exist between our two countries. We need to join hands and assist each other in various development initiatives. It is through partnership that we could be able to make great strides in our development efforts. We do what Dr. Martin Luther King said that: "We learn to live together as brothers and sisters or we will die together as fools." *(Applause)*

It is through the partnership of nations that we can make our world a better place for everyone. We are glad that Ireland has been very close to the people of Tanzania and that your assistance has always been just in time when it was needed. The theme of your Presidency is *Building Bridges.* Your presence here today is a clear testimony of how Ireland has continued to build bridges of economic relations with her friendly countries. Since we have many avenues through which Tanzania could cooperate with Ireland, we should explore how we could further strengthen the relations that already exist for the betterment of our people. *(Applause)*

Your Excellency, as Members of Parliament we understand that we have been entrusted with the task of overseeing development efforts of our people. We have a key role to play in contributing towards a more democratic, efficient and responsible global governance system. We are also responsible in helping our people in their struggle to reduce poverty, and hence improve their well being. The development of our nations hinges on how we can all benefit by working together and sharing the wealth of nations. That is why as leaders we have the task of ensuring that we actively participate in the integration of our national concerns into the international arena. *(Applause)*

Your Excellency, the challenges ahead of us are immense but we have to work hard so that we can be able to overcome them. Ireland has been in the forefront in addressing the challenges such as HIV/AIDS, education, good governance etc. Ireland aid

and programmes under Development Cooperation of Ireland (DCI) and Ireland Official Development Assistance (ODA) have greatly contributed towards our efforts to build a more vibrant society capable of meeting our development challenges. The ongoing programmes you are assisting in Tanzania indicate an upward trend of development assistance. For example during the past three years a total of over 70 million EUROs were received. We thank the people of Ireland for being our partners in our development endeavours. *(Applause)*

Your Excellency, The Fourth Phase Government is only six months old. It is true that we still have a long way to go but we understand that *"a journey of thousand miles must begin with a single step"*. We have given our people a promise of a better life. Through our own efforts and the assistance from our development partners like Ireland we can deliver that promise. We are determined to put in place workable plans and strategies that will enable us fulfil that mission and thank you for your encouragement. *(Applause)*

Mr. Speaker, I was given just a few minutes to thank the President of Ireland for her wonderful speech and for being so generous to spare her time to fly all the way to Dodoma. Your visit to our country will further strengthen the cordial relations between our peoples and governments. We wish you a safe journey back home, and we say in Kiswahili, karibu tena. *(Applause)*

**SPEAKER:** Thank you very much Honourable Prime Minister for speaking for all of us, now its time to adjourn, Waheshimiwa Wabunge, Katibu una matangazo.

**ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, tunasitisha shughuli za Bunge kwa sababu shughuli za asubuhi tumeshazimaliza.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa shughuli za asubuhi za kikao cha leo na kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa kumi na moja leo jioni.

*(Here the Procession of the Speaker and their Excellencies leaves the Chamber)*

*(Saa 06.48 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaahirisha Kikao mchana Mheshimiwa Spika,alishamwita Mheshimiwa Chacha Wangwe, akifuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Chombon na Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, ajiandae.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hii hoja. *(Makofi)*

Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuiwezesha hii bajeti ya kwanza ya Serikali ya Awamu ya Nne kuweza kuletwa mbele yetu ili tuichangie na pia

tunawashukuru wale waandaaji Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Waziri wa Fedha kwa jitihada zao na muda waliotumia kuiandaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli sisi wale ambao tupo katika vyama vingine tunachukulia kwamba ni fursa nzuri kwa sababu Serikali huwa inawashauri na sisi pia ni washauri wakuu katika kurekebisha mipango ya Serikali iliyopo na hii inaonyesha kwamba nchi yetu ina demokrasia ambayo inahitaji kujengwa kwa nguvu zaidi.

Kwa hiyo, mimi nitakachochangia sana sana ni kushukuru ya kwamba tuna Serikali mpya ambayo ina jitihada ambazo zina misingi ya kulenga katika ukweli,ndiyo maana hata sisi wa Kambi ya Upinzani tunaunga mkono jitihada ambazo zimefanywa mpaka sasa na wananchi vile vile wako bega kwa bega kwa kuangalia ya kwamba awamu hii inaweza kuwa tofauti na awamu iliyopita kwa sababu inachukua hatua za mara moja. Tukiangalia suala kama la njaa Serikali imejitahidi na hilo janga limepungua makali, tatizo la ujambazi Serikali inajitahidi vile vile lakini sisi tunaweza kujifananisha na wale manabii wa zamani kwamba hao manabii walikuwa wanawashauri wafalme na hao manabii walikuwa wanatoka hata maparoni kumwambia mfalme ukweli wakati mfalme ana waliomzunguka ambao sanasana wanamweleza mambo ambayo wanadhani anataka kuyasikia.

Lakini sisi tunakuja katika *spirit* ya ukweli kwa sababu ya upendo tulionao katika nchi yetu na ni lazima tuyaseme yale ambayo tunaona ya kwamba hayapo sawa na hii pia ni kuwaambia wenzetu watani wetu wa Chama cha Mapinduzi kwamba sisi sio maadui zao, sisi ndiyo rafiki zao. Kwa sababu sisi tusipowaambia itakuwa kama hadithi ya yule mtu aliyekuwa anakata tawi wakati amekaa juu ya tawi hilo lakini watu wengi walikuwa wanapita pale hawakumwambia na mmoja alipomwambia basi baadaye alipoanguka lakini alimshukuru na kumwambia kwa kweli wewe ndiye rafiki yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi hatuna nia mbaya kabisa na Serikali, isipokuwa naomba u-*take note* ya hili kwamba tunapokuwa tumesimama upande huu, tunapotaka kuzungumza kunakuwa na hali fulani ya baadhi ya Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kufikiria kwamba sisi tupo hapa kwa ajili ya kuidhalilisha Serikali, lakini sivyo, sisi ni sehemu ya Serikali hii vile vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ni nzuri kwa kiasi kwamba ni bajeti ya kwanza kwa hiyo, sisi tunaiunga mkono kwa sababu hii Serikali bado ina miezi sita kwa hiyo, tutaipa muda wa kufanya vizuri zaidi kwa hiyo, kuna haja ya kudodosa baadhi ya maeneo ambayo tunaona kwamba hayakusemwa. *(Makofi)*

Kwanza kabisa tukichukulia jinsi mwanzilishi wa Taifa aliposema kwamba ili tuwe na maendeleo tuna vitu vinne yaani watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora hiyo hakuna anayeweza kuleta ubishi. Watu tunao wakati anasema mambo hayo tulikuwa milioni 8 sasa tupo milioni 35 kwa hiyo tuna watu tele na kama tumemsikiliza vizuri mgeni aliyekuja hapa Rais wa Ireland ametamka kwamba raslimali ya maana zaidi waliyonayo kule Ireland ni watu wao na ndiyo wamewawezesha kufanya hayo yote

mazuri waliyoyafanya. Tatizo katika mipango yaani *strategy* ya *planning* katika nchi yetu ni kwama hatujatilia mkazo na umuhimu katika suala la *Human Resources* yaani watu, ni kweli Rais katika hotuba yake alisema ataangalia suala la ajira lakini tukumbuke ya kwamba asilimia kubwa ya watu wetu ni wale wanaoitwa wakulima wadogo wadogo *peasant* na hao wanakaa vijijini na pia asilimia 80 ya idadi ya wananchi wetu ni vijana wa umri kati ya miaka 13 hadi 35 lakini hii nguvukazi ambayo ndiyo ingeweza kutusaidia katika *production* kwa sababu *labour* ni sehemu muhimu katika uzalishaji, tumeiacha hivi hivi tumewapa elimu bure na pia tumewaacha waranderande nchi nzima.

Katika misamiati tunayotumia kuwaita ambayo inaonekana imekubalika ni kwamba tunawaita yatima, watoto wanaoishi katika mazingira magumu, wazembe na wazururaji, machinga, vibaka, machangudoa na majina ya aina hiyo na tunasahau ya kwamba wale ni watoto wetu ambao tumewazaa na ni wajibu wetu kuwaangalia na kuwapa nafasi ya kuweza kuchangia katika uchumi wa nchi hii ikiwa ni pamoja na kuwapa haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Bungeni tunapozungumzia suala la yatima pamoja na hao watoto waoishi katika mazingira magumu tunasema ya kwamba Serikali imesaidia, mtu fulani amesaidia, shirika fulani limesaidia lakini hatuzungumzi ya kwamba hao ni Watanzania wenzetu na wana haki na kile wanachopaswa kupata ni haki yao kama watu wengine, hapo nadhani tunakosea sana kwa sababu ukiangalia hao watoto yatima ndiyo hao hao wanoitwa watoto wenye mazingira magumu au pengine ndiyo hao hao baada ya miaka kadhaa wanaingia katika jeshi kubwa sasa ambalo ndilo la vibaka wazururaji, wazembe, machangudo na wanarandaranda nchi nzima. Utakutana naye Mwanza anauza bidhaa ameshikilia mkononi baada ya wiki mbili utamkuta Mbeya baada ya mwezi mwingine utamkuta Dar es Salaam na wengine wanaongea kingereza ambacho wamekisoma mpaka *form three, four, five* na hata *form six* ni watu wenye akili timamu na wenye uwezo.

Sasa hii ni *timed bomb* ambayo sisi kama manabii wa kisiasa ni lazima tuwaonye kwamba tuangalie Uganda, hao ndiyo walikuwa wanaitwa wayai wakionekana wanapigwa moto, wanachomwa kwamba ni vibaka lakini hao hao ndiyo waliokuja ku-*form NRM* na kufanya mapinduzi na hakuna aliyewazuia. Tuangalie vile vile nchi kama Sierra Leone, Liberia ni hao hao, kwa hiyo, mipango ya uchumi iendane vile vile na jinsi ambavyo tunawapanga hao ili watusaidie katika *production.* Sasa katika *production* ni kwamba hao watu hawana ardhi kwa hiyo, sera ya ardhi iangaliwe vile vile kwa sababu kama hao hawatakuwa na ardhi hizi *quilaterals* ambazo tunasema kwamba wawe nazo ili wakopeshwe watazitoa wapi? Hana hata redio, wala shamba lakini bila hao tena uchumi wa nchi hii hauwezi kwenda na bila kukiendeleza kilimo hatuwezi kuendeleza viwanda. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunapoambiwa kwamba kuna *Mini Tiger Plan* sijui kwa nini iwe *mini* badala ya *Mega Tiger Plan* kwa sababu nchi zote zilianza mapinduzi ya viwanda lakini baadaye wengi wamefanikiwa, hata wahindi. Sasa sisi mpango wetu wa viwanda hauwezi kuendelea kama hakutakuwa na watu wanaozalisha malighafi na hao watakuwa ni wakulima kwa hiyo, kila mtu apewe hati na aimiliki kwa *title deed* na siyo hizo hati

ambazo zinasemekena kwamba zitatolewa hati za kimila, ziwe ni hati kamili ambazo zimepitishwa na *Commissioner* na pia zimepewa *title* ili ziweze kuwa *legal document*s hapo tutakuwa tumefanya vizuri, hiyo ndiyo itakuwa hatua ya mwanzo katika mapinduzi ya kilimo ambayo tunayazungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni katika kuangalia utoaji haki wa nchi hii, vyombo vinavyotoa haki hasa Mahakama zimepuuzwa lakini zinafanya kazi nzuri sana, zinapata *percentage* ndogo sana katika bajeti yetu. Mahakimu wanatembea kwa miguu lakini ndiyo wanaopambana na majambazi na ndiyo wanaotoa haki kwa wananchi lakini hali yao ya maisha ni ngumu na vile vile vitendea kazi vyao havitoshi. *DC* anapewa gari lakini hakimu wa Wilaya hiyo hiyo hawezi kupewa labda ajinunulie kwa hela yake mwenyewe, sasa hii si sahihi, hii ni kupuuza utoaji wa haki nchini. *(Makofi)*

Vile vile tuangalie jinsi ambavyo tumeachilia hata majeshi mengine ambayo hayako Kikatiba, majeshi kama sungusungu, katika Wilaya yangu wanaua watu wengi sana, wanapora mali zao kwa sababu ni jeshi lisilokuwa na mshahara wala likizo, kwa hiyo, saa 24 wao ni kutafuta kuwapora wale wananchi maskini. Nadhani tubaki tu katika mambo tuliyokubaliana nayo kama Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Lingine pia tuangalie ya kwamba wale wastaafu wetu ambao makato yao ndiyo yamewezesha jengo kama hili kuwepo ambao ndiyo hao ambao tumetumia pesa zao kujenga majengo makubwa katika mji wetu wa Dar es Salaam waongezewe kipato na kile walichonacho wawe wanalipwa kwa wakati unaofaa kwa sababu wanalipwa shilingi 20,000/= kwa miezi sita. Sasa miezi sita unalipwa shilingi 20,000/= walipwe basi hata kwa mwezi au hata kwa miezi mitatu, unamkuta Kanali mzima amekaa kule aliyeendesha vita vya Uganda na sehemu nyingine anasubiri shilingi 20,000/= haiji na yeye ni mtu ana akili, alisoma, huu ndiyo mwanzo sasa wa kuwa na ma-*gangsters* na ma- *syndicates* ambayo huenda ndiyo yanayotusumbua kwa hiyo ningependa kwamba vile vile Jeshi la Polisi liangaliwe na lirekebishwe, wale majambazi waliomo mle watolewe kwa sababu hao ni watu ambao wameshaasi tayari, hakuna sababu ya kuwalea na tunaangalia vile vile hotuba ya Rais iliyotolewa tunaiangalia kama ndiyo dira inaonekana yale aliyoyasema sasa yaanza kuwa *contradicted. (Makofi)*

Kuna mambo ambayo aliyasema kwa mfano Rais aliyasema kwamba tuangalie wezi katika Halmashauri zetu maana mwizi, hiyo ni *police case* moja kwa moja sasa wakati ametoa hotuba na ku-*encourage* Madiwani nchi nzima Madiwani wakaanza kuchukua hatua lakini tena kukatokea sauti nyingine ambayo ilisema Madiwani hawawezi kuwa na uwezo hata wa kufukuza wezi ambao tayari wana *evidence* na kesi zilizoko Mahakamani zitolewe. Sasa hii ni njia moja ya kutaka kupunguza hiyo kasi ambayo watu wote tumeikubali. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba tumuunge mkono Rais na pia tufuate Sheria na Katiba ya nchi kwa sababu hayo ndiyo mambo tuliyokubaliana nayo. Ila mambo mengine kama Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi tunaikubali lakini historia inaonyesha ya kwamba hakuna Ilani ya Chama cha Mapinduzi iliyotekelezwa hata moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunadhani ya kwamba pengine hii ya sasa inaweza ikatekelezeka ila tutaipima kwa kipimo cha Katiba na Sheria za nchi hii, lakini siyo kwa vibwagizo katika hotuba zinazotolewa mara kwa mara kwa sababu hiyo Ilani imetokana na mipango ya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMMED AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na mimi kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba mbili za bajeti ya Wizara ya Fedha na na ile ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ningeanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia katika uhai wangu kupata nafasi hii adimu kabisa kuwa mmoja katika Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Magomeni, Zanzibar kwa kuniamini na baadaye kunichagua kuwa Mbunge wao, nawaahidi sitawaangusha.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo ningependa kwanza pia kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar, kwa kuchaguliwa kwao kuwa viongozi wakuu wa nchi hii. Aidha na Waziri Mkuu naye kupata nafasi hiyo pamoja na Spika wetu na wewe Naibu Spika wetu kwa kuliongoza Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze sasa na mimi kuchangia kidogo katika bajeti zetu mbili hizi ambazo zimetukabili mbele yetu hapa na kwa hakika zinaonyesha wazi au zinaashiria kwamba zitakidhi haja iliyokuwepo mbele yetu kama tunavyojua, haja kubwa tuliyokuwa nayo mbele yetu ni kunyanyua au kupunguza umaskini wa Watanzania na baadaye kila Mtanzania awe katika maisha mema na furaha katika nchi yake aliyojaaliwa nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo basi, mimi nilikuwa nataka kusisitiza tu utekelezaji wa bajeti hii na mipango hii ambayo ni mizuri kabisa na kama walivyotangulia wenzangu waliochangia ni bajeti ambayo imegusa kila mahali na imegusa kila mtu kwa hiyo sasa hivi kinachohitajika ni utekelezaji kwa sababu kupanga ni kitu kingine na kutekeleza ni kitu kingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningewaasa wananchi wenzangu wa Tanzania yaani Watanzania wenzangu kwamba jambo hili si la mtu mmoja, ni letu sote, kila mmoja na nafasi yake alipo anawajibika kutimiza wajibu wake kwa maslahi yake na Watanzania wenzake na hatimaye nchi yetu hii iondokane na hili neno umaskini jambo au neno ambalo kwa kweli mimi linanikera katika moyo wangu kwa sababu neno la umaskini tafsiri yake au maana yake ni kwamba kitu au mtu au nchi ambayo haina kitu na mimi mara nyingi sana huwa najiuliza umaskini wetu sisi Watanzania uko wapi? Kama ni nchi kwa maana ya nchi si maskini tuna kila kitu ambacho kina hitajika au kinahisi kwamba nchi fulani iwe nacho iitwe hii nchi ni tajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii juu ya ardhi wewe simamisha jiti tu au weka mti tu usimwagilie maji utaota na utakua, chimbua kidogo tu kuna kila aina ya madini ni nchi nzima, umaskini huu uko wapi? Tatizo letu sisi wenyewe Watanzania ndiyo wenye umaskini wa roho zetu bado tuna kutu katika roho zetu. Ili tuendelee tuna wajibu wa kila mmoja kwa nafasi yake aliyonayo, kwa kazi yake aliyokuwa nayo ikiwa ni ya kuajiriwa, ikiwa ya kujiajiri lakini aifanye kazi ile kwa madhumuni yake yeye na Watanzania na hatimaye kuna siku wala siyo mbali Tanzania hii itaitwa nchi tajiri kwa sababu ni tajiri kimaumbile. *(Makofi)*

Kwa mfano, Tanzania ina madini ya kila aina, kuna mengine hayako duniani kote isipokuwa Tanzania hii, ina mabonde, mito, maziwa, bahari, fukwe nzuri sana yaani siwezi kumaliza vitu vyote vilivyokuwepo Tanzania ina watu wake wazuri na ina usalama, sasa umaskini huu Watanzania wenzangu itabidi tujiulize hii desturi ya kujiita au ya kuambiwa maskini inatulemaza, tushtuke sisi ni matajiri na tunaweza kuwaonyesha watu kama sisi ni matajiri twendeni basi.

Kama alivyokwisha kutangulia kusema kiongozi wetu, Rais wetu tumeona na wote tunakiri hata watani wetu wanakiri kwamba ni kiongozi madhubuti na ameonyesha mfano na Waziri wetu Mkuu ametuonyesha mfano, basi sisi wafuasi wake tuliokuwa nyuma na tumfuate kiongozi wetu kama tulivyomchagua kwa wingi sana na tumfuate kwa wingi sana, tuonyeshe kwamba sisi kweli tuna nia ya kuondoa huu umaskini unaotajwa ambao haupo kwetu isipokuwa ni sisi wenyewe ndiyo tuliojikomaza tu, tufanye na ndivyo walivyofanya wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, duniani kote hakuna mtu ambaye anafanya kitu kwa madhumuni yake *personal* au binafsi, anafanya kitu kwa madhumuni ya nchi yake na watu wake, sasa sisi huu mpango wa kwamba mimi tu na mimi na jamaa zangu na mimi na familia yangu hatufiki mbali. *(Makofi)*

Baada ya hapo ningeingia kidogo kwenye shughuli au kwenye mambo hayo ya *TRA*. *TRA* ni chombo cha Muungano na sote tumekubaliana kwamba ni cha Muungano hata muundo wake kimeundwa ki-Muungano kwa maana ya wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TRA* ndiyo chombo kikubwa Tanzania hii cha kukusanya kodi au ndiyo mshipa wa roho ya mapato ya nchi hii, inakuwa ina njia mbalimbali na vifungu mbalimbali na sehemu mbalimbali za kukusanya mapato lakini yenyewe ndiyo *regulator* au yenyewe ndiyo msimamizi na mfuatiliaji wa makusanyo ya kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chombo hiki kinafanya kazi Tanzania Bara na Tanzania Visiwani na hata muundo wake wafanyakazi wa Tanzania Visiwani wa *TRA* kuna ambao wako Zanzibar na wa Bara hali kadhalika kuna wafanyakazi wa Tanzania *TRA* Bara, kuna Wazanzibar na Wabara, kuna jamaa zangu wengine nawafahamu mmoja yuko Kigoma, wengine wako Tanga na Tukuyu hii ni kuashiria kwamba hiki ni chombo cha Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Zanzibar *TRA* ndiyo inayofanya makusanyo yote ya kodi katika vyanzo vya mapato ya uchumi wa Serikali ya Zanzibari kwa maana ya Bandari, *Airport* na hizo ndizo njia pekee zinazoweza zikaingiza uchumi au kukusanya kodi Tanzania Visiwani kwa sababu kama tunavyofahamu Zanzibar ni Kisiwa, hakina ardhi ya kutosha kulima kikatosheleza chakula chake wala hakina madini kinachosaidia sasa hivi kidogo ni mambo ya utalii ndiyo yameanza, haina viwanda, kubwa zaidi kimaumbile si Zanzibar tu bali Visiwa vyote vinategemea uchumi wake kwa mambo ya Biashara na Utalii labda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar ili iweze kuendelea ni lazima iweze kuwa na *activities* yaani kuwe na harakati za kibiashara kwa maana ya kuwashirikisha wananchi wake kwa sababu hizo ndizo kazi zilizokuwepo. Zanzibar ndugu zangu hakuna ardhi ya kutosha hata ya kulima nyanya ikatosheleza pale Zanzibar kwa wale waliokuwa hawajui kule Zanzibar kuanzia nyanya, viazi, vitunguu kila aina ya mbogamboga unayoijua wewe inakuja kutoka Bara kulisha Zanzibar hali kadhalika na nafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo Zanzibar wanahitaji pesa za kununua vitu hivi kutoka huku ili viwaendeshee maisha yao na namna ya kupata pesa Zanzibar ni kufanya biashara na Zanzibar, biashara yake soko lake haliko Zanzibar liko Bara. *TRA* ya Zanzibar ndiyo inayofanya *clearance* ya mizigo kutoka Bandarini na ikafika kwa wafanyabiashara, wafayabiashara wanachukua mizigo kuileta Bara kwa ajili ya masoko. Wakifika Dar es Salaam Bandarini pale *Malindi Wolf* au *Bagage Room* unaanza kufanya *re-caption* upya na *TRA* hii ni kero, haya ni maudhi na kama mkisikia kuna kero zinazokera Muungano wetu hili ni namba moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kuna haja kubwa ya kuliangalia suala hili ili tufike na lile lengo ambalo Mheshimiwa Rais alilitamka katika hotuba yake alipolihutubia Bunge kwamba tutafanya kila njia ya kuweza kukuza uchumi wa Zanzibar, si kwa ajili ya Serikali tu, lakini kwa mtu mmoja, mmoja tunahitaji sana suala hili kulifikiria, linauma na linaudhi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo moja nikiwahadithia Waheshimiwa Wabunge mnaweza msiamini na hata kama mngekuwa mmeliona kwa macho yenu mngefikiri mko kwenye njozi. Kuna akima mama fulani wafanyabiashara ndogo ndogo tena wengi wao ni walemavu walikuwa wajiajiri wenyewe kila mmoja ana kimtaji chake cha laki moja au mbili, huwa wanakuja Zanzibar kununua vifaa vidogo vidogo kwenye dazeni za nguzo za watoto, viatu vya watoto na vitu vidogo vidogo ili mradi afanye biashara yake aje alete Dar es Salaam kwa ajili ya mauzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, basi watu wale walipofika Bandarini Dar es Salaam wakaambiwa mizigo yao iko pale na mizigo ile wameinunua dukani kule Zanzibar wana risiti ambazo zimelipiwa *VAT* na kila kitu wanaambiwa mizigo ile wailipie ushuru upya, ni watu ambao wanataka kujitegemea tena ni walemavu *just imagine*, tunajua sasa hii siyo sera ya Serikali wala siyo sera ya *TRA*, lakini kuna baadhi ya Maafisa wa *TRA* kwa maslahi yao binafsi na ndiyo pale nasema kwamba jamani suala hili kila mmoja aliko

sehemu yake ikiwa ni kazi ya kuajiriwa, kazi yake mwenyewe afanye kazi kwa maslahi ya Watanzania wote siyo ya kwake yeye.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu wamekuwa wakiwaambia wafanyabiashara ninyi si mna Serikali yenu bwana ukitaka mzigo teremsha hapa mimi nitakuonyesha kwa *Clearance Agency* fulani atakutolea mizigo yako hapa hapa, hiyo ni kauli ya Maafisa wa *TRA* tunaelewa vizuri sana kwamba siyo sera ya Serikali, lakini kuna watu wanafanya hivyo, suala hili Mheshimiwa Waziri wa Fedha kama yupo au hayupo salaam atazipata kuna haja kubwa sana ya kulifuatilia, *otherwise* litaleta mushkeli kidogo. *(Makofi)*

Mimi kidogo nilikuwa nataka kuzungumza suala la haya mambo ya simu hizi, mimi nilipata bahati, ni mtu wa mwanzo katika wale walioanza kufanya biashara ya simu mwaka 1994 wakati ilipokuwa inaingia hii teknolojia hii, niliajiriwa na Kampuni ya *Mobitel* nikiwa ni mmoja katika watu walioanzisha hii kazi na ndiyo mmoja baada ya Dar es Salaam kufanya kazi nikaanza Zanzibar, mimi ndiye niliyezipeleka Zanzibar. Nikawa *assigned* baada ya kufanikisha vizuri nikawa *assigned* nipeleke Mwanza, nikaenda Mwanza nika *establish*, nikaenda Arusha na Tanga pia kwa kazi hiyo naijua simu inafanya kazi kiasi gani, hawa wanachukua hela nyingi sana, wanachukua hela bila ya kitu chochote, Serikali inahitaji pesa au inahitaji kodi kutoka kwao si kwetu, ichukue kwao wale kwa sababu wale wanachukua pesa zetu *cream*. Ile *card* waliyokupa wewe unailipia, *production* na *manufacturing* yake unalipia kila kitu *hand set* ni yako wao badala ya kuweka mnara hapa na mnara pengine unachangiwa na kila mtu. Wewe uliye *Mobitel* unaweza ukauchangia mnara wa *Celtel* au wa *Vodacom* kwa sababu unaweza kumpigia mtu wa kampuni nyingine unatoka kwako unaingia kwake na yeye atatoka kwake ataingia kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru nami kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba zote mbili, hotuba ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimwia Dr. Juma Ngasongwa na ile ya Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Meghji. Naziunga mkono hotuba zote hizi mbili mia kwa mia pia nawapongeza wataalam waliotayarisha hotuba zote mbili, kwangu mimi naziona ziko kamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwelekeo wa bajeti unaonekana ni mzuri hasa pale ilivyogusia elimu, afya, maji, kilimo na hata maslahi ya wafanyakazi lakini ningependekeza kwamba kwa upande wa wafanyakazi hasa wafanyakazi wa kima cha chini mshahara wao ungekuwa shilingi laki moja, maisha ni magumu mno. Katika kufanya hivyo huu utakuwa ni mwanzo mzuri sana kwa Serikali ya Awamu ya Nne ambayo lengo lake ni kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kusema kwamba *there is no future without past.* Hivyo basi ningependa kupongeza Awamu ya Kwanza, Awamu ya Pili na Awamu ya Tatu ndizo zilizosaidia sana kwa kazi nzuri kutufikisha katika Awamu ya Nne ambayo imepokelewa kwa imani kubwa na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa kutoa pongezi au shukrani za dhati kwa Awamu ya Tatu kwa kazi nzuri waliyoifanya. Mimi nimepata mitandao miwili katika Awamu ile ya Tatu, *Buzz* pamoja na *Celtel*, nimeboresha maji katika Wilaya ya Liwale, nimeboresha umeme katika Wilaya ya Liwale, tegemeo langu sasa katika awamu hii yale yaliyobaki nitasaidiwa kikamilifu yaweze kuboreshwa, nitayataja hapo baadaye.

Awamu ya Tatu naipongeza kwa kazi kubwa moja ambayo imeifanya ambayo ni kuacha akiba ambayo itatuwezesha au ingeweza kutuwezesha kutumia kwa muda wa miezi nane, haijawahi kutokea kwa Serikali yoyote ile kabla, kwa hiyo, jukumu hilo ni kusema kwetu Serikali yetu ya Awamu ya Nne imepata urithi mkubwa sana kutokana na Awamu ya Tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupongeza au kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, mara tu baada ya kuapishwa alifanya ziara kila Wizara ya kujaribu kuhakikisha Wizara hizo zina *take off* vizuri, haijawahi kutokea kabla. *(Makofi)*

Pia ningetaka kutoa pongeza kwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa, ambaye kwa kipindi kifupi amejaribu kuchacharika vizuri sana amekwenda kwa kila tukio ambalo lilikuwa kubwa katika nchi hii, bila kupoteza muda amekuwa akiahirisha hata vikao kwa ajili ya kufuatilia matatizo ya wananchi huo ni mwanzo mzuri sana. Mimi nampongeza kwa kuwa alishafanya ziara katika Mkoa wa Lindi akafika mpaka katika Jimbo langu na ninamshukuru yeye mwenyewe binafsi kwa ziara ile kwa kuwa ziara ile imemsaidia kuona hali halisi ya Jimboni kwangu na jinsi gani ataweza kunisaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spik,a pia nachukua fursa hii kuwashukuru Mawaziri ambao aliambatana nao Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Utumishi, Mheshimiwa Margaret Sitta, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Manaibu Waziri Mheshimiwa Mathias Chikawe na Mheshimiwa Bernard Membe. *(Makofi)*

Pia ningetaka kuwashukuru kwa pekee Manaibu Waziri wengine wawili ambao walifanya ziara katika Wilaya ya Liwale, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza na Mheshimiwa Zabein Mhita. Nawashukuru sana kwa ziara zenu ningependa Mawaziri wengine wafuate nyayo hizo ili mkifika Liwale mtajua namna gani ya kuweza kunisaidia Jimbo langu kwa maendeleo ya wananchi wa Liwale vinginevyo kama ni kutegemea tu mimi niyaeleze halafu ninyi mkanisaidia hamtakuwa na uwezo wa kufanya hivyo, kwa hiyo najaribu kutoa rai kwa Mawaziri wengine wasaidie kutembelea majimbo yetu likiwemo Jimbo la Liwale ili waweze kutoa ushauri wa maendeleo ili tuweze kukwamua maisha ya wananchi ambayo sasa hivi yapo duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Nne kwa jinsi ilivyoweza kukabili tatizo la njaa mwaka huu huo ulikuwa ni mtihani mkubwa sana kwa Serikali ya Awamu ya Nne. Lakini hata hivyo kutokana na hali halisi ya mvua, naishauri Serikali kwamba iwe macho kwamba maeneo mengine pamoja na Jimboni kwangu hasa tarafa ya Kibutuka kwa kuwa mvua hazikutosheleza kwa hiyo, hata mvua tulizozipata ni

pungufu kwa hiyo, hata chakula tulichokipata ni pungufu. Kwa hiyo, patahitajika chakula cha ziada muda si mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningeishauri Serikali ijaribu kuwahimiza au kuwawezesha maafisa kilimo au wataalam wa kilimo waende kwa wakulima kuwaelimisha namna gani ya kuweza kutumia hizi mvua ambazo zinakuja wakati mwingine zinakuwa hazina uhakika au hazibashiriki waweze kupanda mazao ambayo yanaweza kukubali kutumia mvua hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningeomba wakati ule ambao mnaweza kupata chakula na kuleta timu za kuhakiki hali halisi ya njaa katika maeneo yetu.

Mimi naomba tafadhalini sana jaribu kuweka watu ambao wanahusika na maeneo hayo pia. Timu zingine zilikuja katika kipindi kilichopita nilichogundua ni kwamba baadhi yao wanatoka maeneo ya wafugaji sasa wakifika maeneo kama yale ya Liwale wanaona nyasi nyingi, miti mingi kitu cha kwanza akilini mwao wanasema huku hakuna njaa lakini binadamu wa Liwale hawali nyasi labda mawazo yaliyopo ni ya mifugo. Sasa mimi naomba sana mnapotuma Tume basi hizi Tume ziwe zinaelewa mazingira ya kila mahali ili muweze kutoa takwimu sahihi za kila mahali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kilio changu kingine kinakwenda kwa upande wa Madiwani, Madiwani ni wenzetu kiutendaji na ndiyo wanatusidia sana kimaendeleo katika Majimbo yetu, lakini hali ilivyo hali zao ni duni kutokana na kipato cha Halmashauri kusema kweli ni kidogo mno hizi halmashauri zetu hazilingani huwezi kufananisha halmashauri ya Liwale na halmashauri ya Temeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, Liwale pamoja na *39 square kilometers*, Temeke ni sehemu ndogo lakini ina watu wengi lakini pia utakuwa uwezo wake ni mkubwa zaidi kuliko uwezo wa Liwale na Halmashauri hizo zinategemea sana ushuru unatokana na korosho au ufuta na mazao hayo ukiangalia pia inategemeana na hali ya hewa na pia hali ya soko, hayo yote ni vikwazo kwa kupata *revenue* katika Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niliyepo kwenye mbuga za wanyama wiki iliyopita nilikuwa nimeuliza swali ikaonekana kwamba swali nililouliza wawindaji au fedha zilizokusanywa tangu mwaka 2000 mpaka 2005 walitoa *in dollars*, lakini ukifanya mahesabu ya haraka haraka ni sawa sawa na shilingi bilioni 5 kwa muda wa miaka mitano. Lakini ni kiasi cha shilingi milioni 76 tu kwa muda huo wa miaka mitano ndizo zilizoweza kutumika kwa ajili ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iangalie hili kuhakikisha kwamba hawa wawindaji wananufaika sana na pia Serikali itafute mwongozo wa kusaidia wananchi kwa *percentage* kubwa zaidi kuliko hali ilivyo sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, narudi kwenye miundombinu, tatizo tulilonalo sasa hivi ni barabara. Barabara kuu ya kwenda Kusini nayo ni barabara ya kutoka Dar es Salaam kwenda Lindi mpaka Mtwara. Barabara hii imejengwa kwa mizengwe sana na

sijui itakwisha lini. Mwanzoni ilikuwa imeanzia Kibiti kuelekea Lindi na Mtwara. Katika Awamu ya Tatu, katikati ikaanza Mwanza. Kwa mahesabu ya haraka haraka tu kitu unavyokipanua zaidi halafu kusema mtamaliza haraka mimi naona haiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hali ilivyotokea ni kwamba barabara ya kutoka Kibiti kwenda Lindi mpaka leo hii haijakamilika. Katika Awamu ya Tatu, tuliambiwa kwamba tutasafiri kwa gari ndogo kutoka Mwanza hadi Mtwara. Mimi ningeomba Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu kwa kuwa gari tulishanunua mimi na Mheshimiwa Mohamed Sinani la kutokea Mwanza tukishirikiana na Mheshimiwa James Musalika ili tutoke Mwanza na Mheshimiwa Mohamed Sinani twende mpaka Mtwara niwapeleke Jimboni kwangu wakati wa masika. Sasa ningeomba nipewe jibu wakati wa majumuisho ili nijue safari hii niifanye lini? Maana yake mpaka sasa nashindwa kwa ajili ya ubovu wa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, narudi kwenye Jimbo langu la Liwale. Wilaya ya Liwale inaonekana iko pembezoni kusema kweli, haiko pembezoni hata kidogo. Tatizo lililopo ni kwamba Serikali imepuuzia barabara ambazo zinakwenda katika Wilaya ya Liwale. Kuna barabara kutoka Nangurukuru kwenda Liwale kilometa 230 ambayo hiyo ni *shortcut* kwa kwenda Liwale inawasaidia sana wafanyabiashara, inawasaidia wananchi na pia bidhaa zikienda kwa kutumia barabara hiyo bei yake inakuwa ni nafuu na kwa hiyo, inakuwa nafuu kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo barabara ambayo ilikuwa inatumika kutoka Ilonga kwenda Ndapata barabara hii imezuiwa, sasa isijengwe tena na Wizara ya Maliasili na Utalii sioni sababu. Kuna barabara zinapita katika Mbuga za Wanyama za Mikumi na Serengeti. Sisi hatuhitaji barabara ya lami, tunachohitaji barabara ijengwe kutoka Ilonga ifike Ndapata katika Wilaya ya Liwale. Watu wa Wilaya ya Ulanga na Wilaya ya Liwale ni wana ndugu hawa, watu sasa wanalazimika kwenda mpaka Dar es Salaam wapitie Lindi kwenda Liwale hii kusema kweli ni adhabu kubwa sana na siyo hivyo tu. Wakati wa Uchaguzi karibu tukose Majimbo kwa kuwa wananchi walikuwa hawataki kwenda kupigia kura CCM kwa kuwa barabara zao kama hiyo ilikuwa haipitiki na Selous ndiyo wanasema kwamba barabara hiyo isijengwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nashangaa barabara zinapita kwenye mbuga ya Serengeti na sehemu zingine na mimi nimewahi kwenda na gari mpaka Robo. Sasa ni wanyama gani wa huko Kusini ambao hawataki barabara au ni kusema kwamba wanyama wa huko Kaskazini wamepelekwa shule ni shule gani Mweka kwamba hawaogopi barabara? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nahitaji barabara ya kutoka Ilonga kwenda Ndapata ijengwe na Waziri wa Maliasili na Utalii kama palikuwa na sababu zozote ambazo zilifanya barabara hiyo isijengwe kwa ajili ya Maliasili nadhani zimepitwa na wakati na wananchi wanataka kuwasiliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuna barabara ambayo inatoka Liwale inakwenda Tunduru inapitia katika Mto Ruhuhu, barabara hii pia ni maarufu. Bahati nzuri Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alivyokuja aliahidi kwamba atasaidia barabara hiyo kwa kujenga daraja na pia kuna barabara ya kutoka Liwale kwenda Nachingwea barabara hii ina mchanga sana kilometa kama 30 kutoka Liwale. Katika Awamu ya Tatu, tuliambiwa kuna kiasi cha fedha milioni 800 kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo. Lakini mpaka leo hii hiyo barabara haijajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la kushangaza mwaka huu mwanzoni katika kikao chetu cha *RCC* tukaambiwa kwamba zile fedha haziwezi tena kutosha kujenga kilometa 30 zile za mchanga ambazo ni tatizo katika kufika Liwale kwa kutumia barabara hiyo kwenda Nachingwea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya mpaka sasa hivi wanasema kwamba fedha zile sasa zitatumika kwa kilometa 13 na hiyo barabara itaanza kujengwa hivi karibuni na leo hii nimezungumza na wananchi wa Liwale hiyo barabara haijaanza kujengwa. Hizi fedha zimeenda wapi tangu mwaka jana au tangu kwenye Awamu ya Tatu na zinafanya nini katika kipindi hiki chote? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimwia Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja ya Mawaziri wawili, Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme tu kwamba naunga mkono hoja zote mbili ni hoja ambazo zimezingatia mahitaji ya Watanzania hasa kwa wakati huu wa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kuipongeza Serikali ya Awamu ya Nne tukianza na Mheshimiwa Rais pamoja na Baraza lake la Mawaziri limekaa vizuri na wamejipanga vizuri mno ni Mawaziri ambao wanataka kuhakikisha kuwa nchi yetu hii inaendelea. Kwa sababu nilipomwomba Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwenda kutembelea kwenye Jimbo langu katika maeneo yale ya *delta* ili kwenda kuona kuna nini *delta* basi yeye alisema mimi nitakwenda ingawa kulikuwa na baadhi ya viongozi wanasema ukienda wakati wa masika huko siyo kuzuri hakufai uende wakati wa kiangazi labda unaweza kufika.

Lakini yeye alisema wakati tulipokuwa tunaomba kura tulipita kila kona hatukujali mvua wala jua. Lakini mara baada ya kupata huu uongozi ndiyo tuone kule ni mbali, aliamua kwenda wakati ule na ulikuwa wakati mgumu, lakini alikwenda na kwenda kwake kumetusaidia na kumetupa faraja kubwa sana hasa maeneo yetu ya *delta.* Sasa nasema ni Serikali iliyojipanga ina lengo la kutaka kuiondoa nchi yetu katika hali tuliyokuwa nayo na kutupeleka mbele zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nianze kuchangia suala zima la miundombinu. Katika hotuba zilizotolewa na Mawaziri wetu wawili, walisema ili kutekeleza MKUKUTA basi ni lazima kwanza tuhakikishe Miundombinu yetu inakwenda vizuri ndipo MKUKUTA unaweza kutekelezwa vizuri. Hili mimi nawapa hongera kwa sababu bila ya miundombinu utekelezaji wowote hautekeleziki. Lakini bado kuna maeneo mengine yamesahauliwa katika utekelezaji huu na maeneo hayo ni Wilaya yetu ya Rufiji, imetajwa Mikoa mitano. Mikoa mitano itakayopewa kipaumbele ni ile ya pembezoni. Lakini kuna Wilaya ambazo mazingira yake ni magumu sana, mojawapo ni Wilaya ya Rufiji haikuingizwa katika Mpango huu. Hali hii sisi watu wa Rufiji inatupa wasiwasi kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo ya *delta,* ukubwa wake wa maeneo yale ya *delta* ni mara mbili ya Kisiwa cha Mafia. Lakini kuna wakazi kule zaidi 30,000 wapo katika maeneo yale ya *delta*. Lakini katika *allocation* ya *fund* zote hizi hakuna hata moja kusema kwamba wale watu wa maeneo ya *delta* tutawasaidia angalau boti nne kwa kila kata moja ipate boti ya kuwasafirisha kutoka huko waliko kuwaleta katika maeneo haya ya juu, haipo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa naomba sana kwamba wale ni wapiga kura wetu, wanachangia asilimia 80 ya kamba wanaozalishwa kwenye Tanzania yetu hii *prawns* hawa *eight percent* wanatoka kwenye Jimbo langu lile. Lakini bado Serikali haijajua ni namna gani ya kuwasaidia hasa katika upande wa usafiri. Watu wanafariki kutokana na kuzama kwa mitumbwi na kwa kutumia mitumbwi wanapinduliwa na viboko na mawimbi mazito na hata Mheshimiwa Waziri wa Fedha mwenyewe alipokuwa kwenye kampeni mwaka jana alifika kule. Lakini boti zilitoka Dar es Salaam na nyingine zikatoka Mafia zikaenda kule sasa zile boti zimeondoka na watu wale wanaendelea kusafiri kwenye mitumbwi ile ile tuliowaachia. Sasa mimi nilikuwa nafikiri sasa hivi ni vizuri Serikali ione kwamba kule kuna watu ambao wanahitaji kupewa usafiri kama *allocation* ya barabara zinatengenezwa vijijini kwa nini tusitoe boti angalau moja moja kwenye kata zile ziwasaidie kusafiria kwenda katika maeneo mengine. Barabara zinatengenezwa kila siku, leo inatoka hapa inakwenda huku, wale wa kule hawatengenezewi chochote. *(Makofi)*

Mheshimwia Naibu Spika, nilikuwa naomba sana kwamba hili nalo walizingatie watu wa maeneo ya visiwani nao eneo lile la *delta* waweze kuangaliwa kwa kupatiwa usafiri wa kutoka kwenye maeneo wanayoishi kuja katika maeneo ambayo wanaweza kupanda gari, na yale maeneo ni makubwa yana urefu kuanzia kisiwa cha kwanza mpaka mwisho zaidi ya kilometa 60 si maeneo madogo ni maeneo makubwa. Watu hao wanatakiwa wapate huduma. Walimu sasa hivi hawaendi na watumishi wengine hawaendi kwa sababu hakuna usafiri. Sasa ili na wao waingie kwenye karne hii ya 21, naiomba sana Serikali nayo iwaangalie watu wa kule waweze kupatiwa huo usafiri. *(Makofi)*

Lingine ambalo nilitaka kuchangia ni kuhusu suala zima hilo la miundombinu upande wa barabara ambazo zinatoka kwenye *track road* hii ya barabara ya Kibiti-Lindi kwenda katika maeneo mengine ya Wilaya ya Rufiji. Kwa kweli barabara nyingi ni

mbovu hazipitiki na zimesababisha hata baadhi ya huduma za jamii nyingine zitolewa kwa hali isiyokuwa nzuri. Ukienda katika Wilaya ya Rufiji utashangaa kuona shule ya Sekondari ina watu wawili. Sasa hivi kuna *allocation* ya hawa walimu ambao Mheshimiwa Waziri ametwambia wako tayari, lakini kuna *training* ya walimu 3,500 ambao wanatakiwa waende kule vijijini kufundisha shule zetu za sekondari. Lakini mwaka jana tulipatiwa walimu kama watano, sita, kwenda kwenye shule zetu za sekondari. Lakini walipofika kule wamechungulia na kuona kwamba barabara ni mbovu, wanakaa kwenye kituo zaidi ya saa saba, saa nane, huenda wakapata gari siku ile na wakakosa gari, wanakaa tena siku ya pili, wameamua wale walimu wote kuondoka bila kuripoti. Sasa *allocation* hii ya walimu na *training* hii ya walimu inayotaka kufanyika bila kuweka miundombinu vizuri, tutawasaidia watu wa Mikoa ya Kaskazini ambayo miundombinu yake ni mizuri, lakini kule watu wa Kusini bado hali yetu itakuwa ni mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba sana upendeleo wa pekee na ujenzi wa barabara ambazo zinaweza zikapitika karibuni mwaka mzima basi tuache kwanza kujenga barabara katika maeneo ambayo tayari barabara zipo zinazopitika na kuna watumishi wa kutosha. Tujenge barabara hizo katika maeneo ambayo watumishi hawaendi na kwa kuwa watumishi hawaendi watu wa kule wako nyuma, tuanze kupeleka kule, tusijenge barabara katika maeneo mengine ambayo tayari yameendelea tusifanya hivi. Wale ni binadamu, hatuendelei kule kwa sababu hakuna elimu, madaktari hawaendi, hakuna chochote kinachofanyika. Hivi sasa baadhi ya shule nyingine zimefungwa kwenye Jimbo langu, shule ina mwalimu mmoja anakwenda kufuata mshahara tarehe 20, shule hakuna. Sasa miundombinu haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Wizara, miundombinu katika Wilaya ya Rufiji iangaliwe kwa mtazamo wa pekee kwa sababu bila ya elimu hakuna maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pia suala zima la posho katika mazingira magumu. Mwezi Januari, 2006 katika Mkutano wetu wa Pili, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi alikuwa amezungumza kwamba huenda mwaka huu katika bajeti kwamba yale maeneo ambayo walimu wanaishi katika mazingira magumu watapatiwa ile *hardship allowance*. Hili ni suala zuri. Lakini nilikuwa naomba lisiishe tu walimu, kuna watumishi wengine ambao siyo walimu wanaoishi katika maeneo hayo kwa nini na wao wasiweze kufikiriwa. Kwa nini Serikali isitoe upendeleo huo wa kuwapatia *hardship allowance* watumishi wote wanaoishi katika mazingira magumu kama yale. Naomba sana suala hilo nalo lizingatiwe kuwapatia *hardship allowance* watumishi wote bila kubagua sekta yao wanayofanyia kazi wale wanaofanya katika mazingira magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kidogo suala la Ilani yetu ya Uchaguzi. Katika Ilani yetu ya Uchaguzi na Mheshimiwa Rais alikuwa anapita na kutangaza kuwa katika miaka mitano hii ya kipindi chake cha kwanza atahakikisha kila Mkoa unakuwa na Chuo kimoja cha *VETA.* Katika Vyuo vile vya *VETA* nilikuwa naangalia hii *public expenditure estimate development votes* kwamba hivi Vyuo vya *VETA* vimewekwa wapi?

Nimeangalia mwanzo mpaka mwisho sikuona kama kuna eneo lolote ambalo limewekwa kwa ajili ya kujenga Vyuo vya *VETA*, vyuo ambavyo vitaweza kuwapatia elimu wale vijana wanaomaliza elimu ya msingi. Nitaiomba sana Serikali pengine watakapokuwa wanajibu hoja wahusika, basi watwambie kwamba katika mwaka huu wa fedha 2006/2007 ni Mikoa gani ambayo itakayokuwa imepata awamu ya kwanza ya utekelezaji wa ujenzi wa Vyuo vyetu vya *VETA* katika kila Mkoa kwa nchi yetu yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la kupata *clean certificate* na adhabu wanayopewa wale watu ambao *certificate* zao ni chafu. Suala hili ukiliangalia lina upendeleo wa sehemu moja na lina uonevu kwa upande wa pili. Kwa upande wa kwanza, Halmashauri ambazo zinakosa *clean certificate* zinanyimwa ruzuku ya maendeleo, lakini Wizara zinazokosa *clean certificate* zinaendelea kupewa ruzuku ya maendeleo kwa nini? Mheshimiwa Mbunge mwenzangu hapa alikuwa amezitaja Wizara ambazo zilipata *certificate* chafu lakini zikaendelea kupewa ruzuku ya maendeleo wakati Halmashauri ya Wilaya inayopata *certificate* chafu inanyimwa ruzuku ya maendeleo. Mimi nadhani msumeno huu ukate pande zote. Wizara ambayo haifanyi vizuri na inapata *certificate* ambayo ni chafu basi nayo pia inyimwe ruzuku ya maendeleo, na wale wahusika wote Serikali iwape adhabu, kwa nini wamesababisha hivyo? Kwenye Halmashauri za Wilaya wamesababisha watu wachache wanakosa fedha za maendeleo, lakini kwenye Wizara wanaendelea kupewa ruzuku ya maendeleo mpaka lini? Nilikuwa naomba sasa suala hili nalo liangaliwe kwa uzito wake. *(Makofi)*

Mheshimwia Naibu Spika, mwisho mwenzangu Mbunge wa Liwale alizungumzia barabara ya Kusini. Kuna tatizo la wakandarasi katika utengenezaji wa barabara zetu. Sasa Mawaziri wanaposimama wanasema kwamba wakandarasi hawa ni jeuri, wakandarasi hawa hawafai hivi ni kosa la nani? Unapompatia ukandarasi wa kujenga barabara nadhani kunakuwa na wawakilishi wetu wa Wizara ambao wako pale ndani wanafanya kazi ya kuangalia utendaji wa Wizara. Lakini hawa watumishi wanafanya kazi gani? Barabara zinatengenezwa kwa muda mrefu, utaambiwa mkandarasi hafai kwa sababu anafanya kazi polepole na hana vifaa, hivi alitakiwa vifaa avipate wapi. Anapopewa kazi hii ya ukandarasi si anajiamini kwamba yeye ana vifaa vya kutosha. Lakini inakuwaje mpaka huyu mtu anachelewesha utengenezaji wa hii barabara na programu zingine.

Mimi nilikuwa naiomba Wizara ziangalie upya utoaji wa ukandarasi zisitolewa kwa upendeleo. Ukandarasi hutolewa kwa mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi hiyo na kwa kipindi kilichopangwa. Sasa hivi hii barabara ambayo inazungumzwa ya Kibiti-Lindi inatakiwa ifike mpaka Mwanza Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba ifikapo Desemba, 2006 barabara hiyo itapitika. Lakini haipitiki na haitopitika kwa mwaka huu, hata mwakani kama tukiendelea na kusuasua huku kunakoendelea hiyo barabara haitaweza kupitika. Sasa tunamwekaje Mheshimiwa Rais hapa?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba sana Wizara ziangalie nani wa kumpatia ukandarasi asiyekuwa na uwezo asipewe ukandarasi na mwenye uwezo apewe na wafuatilie kazi ya kila siku. Lakini makandarasi wengi wa Kusini kule kazi yao

wanafanya wanavyotaka wao wenyewe tu. Naomba sana hivi vitu viangaliwe. Barabara zinazoangaliwa ni za Kaskazini, barabara za Kusini kwa nini haziangaliwi?

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba ninaunga mkono hoja zote mbili na ninakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kushiriki katika kuchangia hotuba ya bajeti ya mwaka huu hii ikiwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia hoja ya bajeti ndani ya Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hiyo, napenda nitumie nafasi hii kuwashukuru wananchi wote wa Jimbo la Kahama kwa imani waliyokuwa nayo kwangu ya kuniwezesha leo hii kuchangia hotuba ya bajeti ya mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia hotuba hii, napenda niwapongeze Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa mada zao nzuri ambazo kwa hakika Watanzania wote wamezipokea kwa matumaini. Kwa hakika matumaini ya Watanzania yametokana na kazi nzuri ambayo wameifanya Mawaziri hawa katika kuandaa bajeti ya mwaka huu na wameifanya katika kipindi kifupi hasa ukizingatia kwamba wamekuwa katika Wizara hizi kwa muda takriban wa miezi sita. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mimi ninayo machache ya kuchangia hasa ukizingatia Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia katika maeneo mbalimbali ya bajeti hii hivyo, nitajikita katika maeneo matatu au manne yafuatayo, nitapenda kuanza na sekta ya Maliasili. Sekta ya Maliasili hapa nchini ni muhimu sana kama ikipewe umuhimu na kipaumbele inaweza kuchangia kwa kiwango kikubwa kabisa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu na pato la Taifa. Kwa bahati nzuri sana Tanzania imependelewa na Mwenyezi Mungu kuwa na maeneo mengi yenye maliasili nyingi ambayo imetapakaa katika nchi nzima. Kwa bahati mbaya sana sekta hii inaonekana kutokupewa kipaumbele na matokeo yake mchango unaotolewa na sekta hii ni mdogo. Hii inadhihirisha kabisa wazi katika hotuba hizo zote mbili ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na ya Waziri wa Fedha, na wote wawil ninavyofahamu mimi wamewahi katika nyakati tofauti kuwa Mawaziri wa Maliasili na Utalii na muda wote walipokuwa pale walifanya kazi kubwa kuhakikisha kwamba sekta hii inachangia pato la Taifa, lakini katika hotuba zao safari hii sekta hii hawajaipa kipaumbele. Fedha nyingi sana ambazo zingeweza kupatikana kutokana na maliasili iliyopo hapa nchini inaishia katika mikondo ambayo siyo rasmi kisingizio kwamba majangili wanapora mali. Lakini hata kampuni zile ambazo zimepewa leseni kwa mfano za uwindaji zinavuna hazina ya nchi hii, lakini kipato kinachoonekana ni kidogo. Ukiangalia takwimu za miaka mitano iliyopita pato linalotokana na uvunaji wa maliasili hususan wanyama imekuwa ikipanda kwa asilimia ndogo sana kwa sababu gani? Maliasili ya Tanzania kila siku inaondoka na sisi ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba hali hii inasitishwa la sivyo historia itakuja kutuhukumu. Watanzania wenyewe hata hawafaidi rasilimali hii, nimesema maliasili imetapakaa katika nchi nzima. Kule katika Jimbo la Kahama tuna misitu minene, mapori

ya akiba, wanyama wanawindwa, wananchi hawafahamu kinachoendelea na mwisho wa mwaka Halmashauri inapewa shilingi 1,000,000/= hii ni hatari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vitalu vya uwindaji ni eneo moja ambalo lingeweza kuipatia nchi yetu fedha nyingi na hivyo kuchangia katika maendeleo ya nchi yetu. Lakini vitalu hivi vinaipatia Tanzania *peanut*. Kuna nchi hapa Barani Afrika ambazo uchumi wake umeimarika kutokana na maliasili hii ya wanyama na sasa hivi kuna mtindo ambao Tanzania imefanywa kama shamba la kuja kuvuna na watu ambao wana makampuni Barani hapa Afrika katika nchi jirani. Lakini wanapofanya *market* wana *market* nchi zao na wawindaji wakifika katika nchi zao wanawaleta kwenye mashamba yao yaliyopo hapa Tanzania. Lakini bei ya mnyama yule anayochanjiwa mtu kule ni ya nchi nyingine. Viwango vinavyotozwa kwa wanyama wetu ni vya chini mno ukilinganisha na nchi kama Botswana na Namibia. Nafikiri wakati umefika sekta hii ipewe kipaumbele na iingizwe kwenye programu kuhakikisha kwamba inachangia kadri inavyostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchangia sekta ya utalii. Kwa zaidi ya miaka 10 nimefanya katika sekta ya utalii. Sekta hii inachangia asilimia 16 ya pato la nchi yetu. Sekta ya utalii ni sekta ambayo ndiyo pekee duniani inayotoa ajira kwa watu wa dunia hii. Nina hakika sekta hii hapa Tanzania kule Kanda ya Kaskazini inatoa ajira kubwa siyo tu kwa matajiri, lakini hata kwa watu wa chini kabisa kwa kuuza vitu vidogo vidogo kama mabangili na kadhalika. Lakini ukiangalia katika hotuba zote hizimbili pia sekta hii haijapewa umuhimu. Sijaiona bajeti, lakini nina wasiwasi kwamba bajeti kwa ajili ya kuitangaza nchi hii katika nchi za nje ili watalii wengi waje na pato liongezeke lipande kutoka asilimia 16 mpaka 20 mwaka huu ni ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Serikali inafikiria nini huyu ng’ombe anayetoa maziwa sasa hapewi chakula cha kutosha ili aweze kutoa hayo maziwa, mimi nasikitika sana. Nakumbuka Mheshimiwa Zakia Meghji alikuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba *TTB* inapata fedha ya kutosha kuweza kuitangaza nchi yetu. Leo hii sijaona mahali ambapo anatetea *TTB* ipate walau kuliko kilichopata mwaka jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi Watanzania tunabaki tunalalamika kwamba nchi yetu haitangazwi sawa sawa, nchi za jirani wanatumia vivutio vya Tanzania kujinufaisha. ni haki yao wafanye hivyo! Kama wewe huwekezi, unategemea nini? Nakumbuka mwaka jana 2005 katika kongamano la Kimataifa Mjini Nairobi ambapo Mawakala wa Utalii wa Bara la Afrika na la Wamerikani walikutana kujadili kuhusu mikakati ya kuitangaza Afrika nchini Marekani, Waziri mmoja wa nchi jirani alidiriki kusema kwamba Mlima Kilimanjaro uko katika nchi yake. Watanzania tulitoka nje ya Kikao. Lakini hiyo haisaidii, ni lazima kuwekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka haraka nitamalizia na Sekta ya Madini. Mkoa wa Shinyanga una madini mengi na Wilaya ya Kahama hususan ina dhahabu. Madini haya kwa hali jinsi ilivyo sasa hivi mwananchi wa kawaida wa Kahama haoni umuhimu wa madini hayo kuwepo pale Kahama. Ni kwa sababu hawaoni *direct profit* ya madini hayo. Mgodi wa Kahama unasafirisha tani nyingi za mchanga, wanatumia

barabara ya Halmashauri.  Miaka saba iliyopita kabla ya mgodi huu haujaanza kufanya kazi barabara ile ilikuwa nusu saa unafika Kijiji cha mwisho cha mpakani mwa Geita. Leo hii malori haya yameharibu hiyo barabara, imekuwa ni mwendo wa saa nne.  Hawa wenye migodi ukiwagusa ni mbogo!

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ni suala la utafiti.  Kahama dhahabu yake iko juu juu, lakini watu wanafanya utafiti miaka sita; wanafanya nini huko maporini? Wana-*scare* watu na hakuna ufuatiliaji, hakuna anayejua wanafanya nini kule maporini. Katika Kata ya Idahina kule Kahama wamekuwepo kwa miaka zaidi ya minne. Wanazunguka zunguka huko kwenye mapori wala sijui wanafanya nini.

Ofisi ya Madini Kahama Mjini haina hata baiskeli.  Mambo haya leo hii tusipoyachunga na kusimamisha kinachoendelea baada ya miaka 20 tutakuja kupata matatizo kama ambayo yanatokea katika nchi nyingine hapa Barani Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima kuwe na utaratibu wa kuhakikisha kwamba madini haya yanamnufaisha moja kwa moja mwananchi wa kawaida na hususan katika eneo analoishi.  Wanapata taabu, wanafukuzwa kwenye maeneo na sheria haiwalindi Watanzania.  Wanalipwa fedha kidogo sana halafu wanakuwa *displaced*, kesho na kesho kutwa unamtegemea Mtanzania huyo huyo aje aunge mkono kuwepo kwa uchimbaji wa madini hayo! Haiwezekani.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iangalie mambo haya kwa makini sana, lakini kwa kuzingatia nchi yetu, kwa kuzingatia watu wetu na lazima wahusika wawe na uzalendo.  Maana yake matatizo mengi haya yanasababishwa na Watanzania wenzetu, viongozi ambao wanaweza kuamua halafu tunatumia muda mwingi sana hapa kuzungumzia kero ambazo kama mambo yangekuwa yamepangwa vizuri tusingefikia hapo.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kilimo.  Nina hakika wananchi wa Kahama hususan wakulima wa zao la pamba.... *(Hapa kengele ililia)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.  *(Makofi)*

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

Kwanza kabisa ningependa kutoa pongezi zangu za dhati kwa Waziri wa Mipango na Waziri wa Fedha kwa Bajeti nzuri ambayo imepata mapokeo mazuri kutoka kwa Watanzania wengi.  Bajeti hii imejikita katika nyanja nyingi na inatuonyesha wazi uwezekano wa kutekelezeka kwa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa kwanza wa Fedha mwanamke kwa kuandaa Bajeti ambayo inajali mazingira.  Naishukuru Serikali kwa sababu sasa hivi imeona kwamba Tanzania tumefikia mahali tutumie gesi.  Hayo ndiyo maendeleo.  Tunawapongeza kwa kupunguza ushuru kwenye gesi, lakini tukumbuke kwamba asilimia zaidi ya 80 ya Watanzania ni watu ambao wanaishi Vijijini,

ambao wengi wao ni maskini, ndio wanaotumia mkaa na kuni na kupikia kwenye mafiga matatu. Hawa hawa, wengi wao wanaishi kwenye zile nyumba tunazozijua *full suit*, udongo juu, udongo kwenye kuta. Wenye *improvement* ni wale ambao wameezeka kwa nyasi. Sasa *system* ya gesi nilikuwa na wasiwasi kwamba itafungwa kwenye hizi kuta za udongo au wapi?

Nilikuwa na mapendekezo matatu kwa Serikali. Kwanza, sasa hivi tujitahidi kuboresha hizo Sheria na Kanuni za Kuzuia Uvunaji Miti Holela, kusudi tuweze kuboresha mazingira yetu na kuyahifadhi. Hilo la kwanza.

Lakini la pili, basi tungetafuta namna ya kuhamasisha wananchi wazidi kupanda miti mingi na wapande misitu mbadala kusudi hao ambao hawawezi ku-*afford* gesi na mafuta ya taa waweze kuendelea kutumia kuni kwa wakati huu. Serikali hii itafute Wawekezaji na kwa kutumia asasi mbalimbali ambazo zina fedha kusudi waweze kujenga nyumba kwa gharama nafuu, watu wapewe hizo nyumba waendelee kulipa pole pole kwa muda mrefu kusudi tuweze kuboresha maisha ya watu wetu. Kila mtu awe na nyumba nzuri ya kudumu aweze kufunga *gas system.*

Lakini lingine tunao watu ambao kweli sio masikini kama wanavyofikiria. Mtu ana ng'ombe mia nne, mia tano, lakini anakaa kwenye hiyo nyumba ya *full suit* ambayo ni udongo juu na chini. Mtu huyu anachohitaji ni elimu. Nafikiri Waheshimiwa Wabunge wenzangu inabidi tuwaelimishe wananchi wetu wajue umuhimu wa kujenga hizo nyumba za kudumu kwa sababu maisha bora ni pamoja na mahali unapoishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, walioutembelea au walioufahamu kwenye miaka ya 1950, 1970 wanajua kwamba Mkoa wa Kagera ulikuwa umekwenda mbele kimaendeleo tofauti na sasa. Mkoa wa kwanza ulikuwa Kilimanjaro wa pili ulikuwa Kagera na wa tatu ulikuwa Mbeya. Wakati huo watu wa Kagera walikuwa wanaitwa Wasomi. Baada ya hapo Mkoa ukaanza kupiga *mark-time,* ukarudi nyuma baada ya vita vya Kagera na kila kitu kikarudi nyuma, mambo yakaharibika wakaanza kuwaita Nshomile, hiyo ilikuwa ni neno kama la kejeli hivi, baada ya kugundua kwamba mambo hayaendi sawa.

Kufika kwenye mwaka 2000/2001 jumla ya watoto waliopaswa kwenda kuanza Darasa la Kwanza kwenye Mkoa Kagera, wa walikuwa umeteremka mpaka asilimia 50 au 60, wakati MMEM inakuja kuanza. Kuonyesha kwamba mambo yalikuwa hayaendi sawa, Mkoa wa Kagera kwenye matokeo ya Darasa la Saba, ulikuwa umefikia mpaka kushika nafasi ya 17 na 19 katika Mikoa 20 ya wakati huo.

Mtakumbuka kwamba tumepata vita vya Idd Amin, Mkoa wa Kagera umeshambuliwa vile vile na Wakimbizi wanaotoka sehemu mbalimbali, Mkoa wa Kagera kuna UKIMWI na yatima ni wengi, uchumi umekwenda chini kwa sababu watu wengi wanalima kwa jembe la mkono na wanapanda bila ya kutumia mbolea. Pia, Mkoa wa Kagera walikuwa wanategemea zao moja tu ambalo lilikuwa ni kahawa. Baada ya bei kuteremka kwenye Soko la Dunia, mkulima wa Kagera akajikuta amekosa kipato chochote, basi akaendelea kuwa masikini. Kulikuwa na maji kwenye Vijiji. Baada ya

hizo *system* zote kuharibika, basi kukawa hakuna maji na umeme umebakia kwenye Makao Makuu ya Wilaya na Vijiji kama viwili vinavyozunguka pale Makao Makuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru Serikali kwa kututengenezea angalau barabara moja sasa kwa kiwango cha lami kuanzia Mtukula mpaka Kagoma. Lakini kama kama walivyokwishasema wenzangu, Mkoa Kagera umetengwa na *the rest of Tanzania* na *Lake Victoria.* Nisizungumzie hii meli ambayo imezama juzi juzi, kuna nyingine ambayo imezama *almost ten years ago* ambayo inaitwa *MV Bukoba.* Ilizama na Watanzania, watu wa Mikoa ile zaidi ya elfu moja, walipoteza maisha na ile ni kwa sababu meli ilikuwa imeshazeeka na haikuwa haijapata matengenezo. Sasa hivi tunayoitumia *MV Victoria* mambo yake ni yale yale na yenyewe imezeeka. Nafikiri hali ya Kagera ya wakati ule ni tofauti na ya sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao uwanja mdogo wa ndege ambao ni uwanja wa udongo. Mvua zikinyesha, basi inakuwa ni matope. Mwenyewe nimewahi kushuhudia ndege imekwama kwenye matope. Mwezi uliopita alipokuja Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye ziara, siku anaondoka mvua zilinyesha nyingi tukaanza kusali kwamba ile ndege ikikwama kwenye matope sasa itakuwa kasheshe.

Nafikiri ingekuwa ni vizuri zaidi kuuangalia upya ule Mkoa wa Kagera kwamba mambo sasa sio sawasawa. Tujengewe kwanza uwanja wa ndege kwa kiwango cha lami, wa-*improve* hii *transportation* kwenye maji kusudi tuweze kutafutiwa vyombo vya usafiri vingine. Nasema hivyo kwa sababu Mkoa wa Kagera una ndizi nyingi. Sasa hivi tunasema ni masikini, hawana kipato, lakini ndizi waziuze wapi? Kama kungekuwa na uwanja mkubwa, ndege zikatua hapo, zikabeba ndizi zikapelekwa mpaka Ulaya, watu wa Mkoa wa Kagera wangeweza kupata kipato ambacho kingeweza kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kwa niaba ya Wana-Kagera iweke mikakati ya makusudi kuboresha ule Mkoa. Kwa nini? Kwa sababu Mkoa wa Kagera kuna mvua miezi minane kati ya miezi 12, Mkoa wa Kagera una vivutio vya utalii vingi tu ambavyo vinahitaji *improvement,* Mkoa wa Kagera una hali ya hewa safi na tuna umeme wa uhakika unaotoka nchi ya jirani, Uganda. Sasa kwa sababu kuna kianzio, ukiwekeza kwenye Mkoa huo unaweza ukapata matokeo mazuri ambayo yanaweza yakasaidia Tanzania nzima.

Kwa hiyo tukiweza kuboresha miundombinu tuka-*attract* Wawezeshaji, tukahakikisha kwamba tunavyosema sasa tunakwenda kufanya mageuzi ya kilimo, tukaanzia kule, hata kama mkitaka kumwagilia kuna *Lake Victoria*, kuna Mto wa Kagera, kwa hiyo, tunaweza tukaanzia kule. Ninawahakikishia kwamba tukiweza kulima kwa kilimo cha kisasa Bukoba Vijijini, Misenye, Ngara, Karagwe, Biharamulo na Chato tuna uhakika wa kujilisha na kulisha Mikoa mingine mitano au sita. Tunachohitaji ni Serikali itusaidie kuboresha miundombinu na kuweza kutupatia hizo nyenzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa mpango mzuri sana wa MMEM. Huu mpango umetuletea mafanikio makubwa sana na umetupa sifa nyingi sana

duniani.  Wote mmeshuhudia kwamba wanafunzi wengi waliofikia umri wa kwenda Shule wamekwenda Shule na kwa taarifa yenu, mwaka jana 2005 vijana 393,946 walihitimu Darasa la Saba.  Wamefaulu wengi, Mheshimiwa aliyekuwa Waziri wa Elimu alikuwa anasema haya matatizo yanayojitokeza ni matatizo ya maendeleo.  Kwa hiyo, sio mabaya.  Lakini wengi wakashindwa kwenda Shule za Sekondari, ikabidi Mheshimiwa Rais wetu atamke na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa, akasimama kidete Mkoa na kwamba wale watoto waliokuwa wamefaulu angalau wakapunguzwa punguzwa.  Lakini mimi kwangu naiona ilikuwa ni zimamoto pamoja na kwamba imeleta matunda mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Elimu ametueleza kwamba kuna upungufu mkubwa wa Walimu. Anazungumzia kwa watoto ambao tunao sasa hivi, bado MMEM haijaanza kuzaa matunda.  Watoto wa MMEM hawajafika Sekondari. Tuna upungufu wa Walimu 3,000 na kuendelea.  Sasa ukaanza mpango wa MMES. Mpango wenyewe ulikuwa mzuri, ulianza vizuri, lakini ukawa na matatizo kwa sababu wananchi waliotakiwa kuchangia hawakuchangia kwa sababu hawakuhamasishwa vya kutosha na Serikali nafikiri ilikuwa inategemea Wafadhili ambao hawakuleta fedha *on time.*

Kwa hiyo, tangu mwaka jana 2005 Julai mpaka sasa hivi mradi wa MMES ulikuwa unasuasua.  Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza basi, Rais wetu amesema *priority number one* ni elimu, kipaumbele namba mbili ni elimu na kipaumbele namba tatu ni elimu. Tunajiandaaje kupokea watoto milioni moja na laki nne na ushee watakaomaliza Shule ya Msingi mwaka 2008 na wale watakaoingia; Je, wale ambao ni *product* ya MMEM, Tumejiandaaje kuwapokea?  Mbona hata nilipoangalia kwenye Bajeti sijaona vizuri kile kiwango kikubwa cha kujenga madarasa, mabweni na kuwaandaa Walimu? Je, tunataka tena tuje tufanye zimamoto?  Je, tunataka kuongeza *just numbers in schools* au tunataka elimu bora?  Lipi zuri? Bora elimu au elimu bora?!

Nilikuwa naomba basi, Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa wakati huu kama sijachelewa kuomba, mwongeze fedha kwenye Sekta ya Elimu kusudi tuone kwamba *we are serious* na kweli tunataka kuwapokea hawa watoto.  Nasema hivyo kwa sababu kuna utandawazi unakuja, watoto wetu watakaokuwa wanapata *Division* 0 – 3 unampeleka mtoto, unaajiri Mwalimu mmoja kwenye Shule, anashindwa Kidato cha Nne, unasema ameshindwa.  Si wanashinda wanacheza tu Darasani! Wanajifunza nini.

Kwa hiyo, lazima tuhakikishe kwamba Shule zetu tunazozitayarisha zinakuwa *well equiped* kusudi tuweze kupata Watanzania waliopata elimu bora na hawa wanawezi kuingia kwenye soko la ushindani kama hizi nchi za jirani.  Je, kwenye milioni moja na laki nne watoto watakaomaliza Darasa la Saba, tunasema *transition rate* itakuwa ni asilimia 50.  Kwa hiyo, tutachukua laki saba, hawa laki saba wanaobaki wanakwenda wapi?  *After ten years* watakuwa ni milioni saba.  Hivi leo kwa nini mnashangaa kwamba wizi, vibaka, watoto wa Mitaani wameongezeka, hawa watoto wanamaliza Darasa la Saba wakiwa na miaka 13 au 14 huwa wanakwenda wapi?  Hawa ambao hawachaguliwi kwenda Sekondari,  Serikali kwa nini tunaamua kuwatupa tu!

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na pendekezo kwamba tufuate mfano wa Canada sio kwamba kila mtoto anao uwezo wa kuingia kwenye mtiririko wa kawaida wa Sekondari kwenda mpaka *University* wanakuwa *alternatives* tumlee huyu mtoto wa miaka 13 aliyemaliza Darasa la Saba na kumpa elimu itakayomsaidia angalau *four years* afikie miaka 18. Sisi tunachukua wale wanaoingia Sekondari tu, wengine tunawaacha. Nafikiri sasa hivi tuanze kufikiria *compulsory Secondary Education* kusudi tuweze kuwasaidia hawa watoto ili tuweze kujenga Taifa letu. *(Makofi)*

Naishukuru Serikali kwa kurekebisha maslahi ya wafanyakazi. Nina uhakika kwamba mtakuwa mmepunguza kero. Waliokuwa wanatoroka, kutoka kwenye ajira za Serikali na waliokuwa wanakwenda nje kutafuta *green pastures,* sasa hivi watatulia. Nilikuwa na angalizo, sasa basi tujaribu kudhibiti ule mfumko wa bei kwa sababu bila kufanya hivyo, kodi itapanda, bei za bidhaa zitapanda, usafiri utapanda, hivyo huyu mfanyakazi atashindwa kufaidi hilo ongezeko. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri suala hili liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, ilani imetamka kwamba imetambua uwezo na mchango wa vijana na wanawake katika maendeleo. Mheshimiwa Rais ameahidi kwamba atawawezesha. Tunangoja sasa kwenye Bajeti za Wizara mbalimbali kwa sababu tunajua haya maswali ya vijana na wanawake ni ya mtambuka. Tunangoja tuone wazi wazi mtakavyotekeleza ahadi za Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nianze kusema kwamba hakuna Bajeti duniani ambayo ni mbaya. Ni mbaya kama tu haitekelezwi. Bajeti zote ni nzuri kama zinatekelezwa. Kwa hiyo, Bajeti hii mimi naona ni nzuri kama itatekelezwa kwa kulingana na yaliyomo. Sio lazima Bajeti ionyeshe kila kitu, kibarabara fulani katika Kijiji cha kila Mheshimiwa! Mtu anafanya kulingana na anapojikuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kwanza nianze kutoa pongezi kwa Mawaziri wetu wote wawili kwa kutuwasilishia Bajeti yao nzuri kabisa na pamoja na Watendaji wao. Kwa kweli wamefanya kazi nzuri. Pongezi za ziada ni kwa Wizara ya Fedha kwa kutumalizia jengo letu la *BoT* kule Zanzibar pamoja na Ofisi ya Bunge Zanzibar, nawashukuru sana.

Lakini pongezi vile vile nazidi kuzitoa kwa wataalamu wetu waliobuni mchoro huu wa jengo hili. Nasisitiza tuwape pongezi na nilisema siku ile kwamba ikiwezekana wapewe *special award* nikiwa na maana yangu. Wanamichezo tumewaita hapa tumewapa, sasa na hawa tuwaite.

Mheshimiwa Waziri Mkuu hawa ni wanasayansi wetu. Tunalia tu vijana hawataki sayansi kwa sababu gani? Hawa ndio wanasayansi wenyewe. Kwa hiyo, ninaomba tena vijana wetu wakiwemo na Wagogo wa Mpwapwa wakumbukwe wapewe *special award. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza na suala la simu. Jamani mimi naunga mkono Serikali kwa kuongeza asilimia hizo mbili, tena zingefika hata kumi. Naunga mkono kwa sababu Serikali inajua kabisa inafanyaje lakini ninachowaomba, wawabane wale watu *tariffs* zisiongezeke, wanavuna mapesa mengi sana. Tunao wataalamu humu sisi wamefanya kazi *TTCL*, *VODACOM* wanafahamu. Waheshimiwa Wabunge, wamenung'unika sana hapa barabara mbovu, Shule hatuna na kadhalika. Sasa apate wapi fedha jamani? Mheshimiwa Meghji kauze nyumba yako, basi uwape. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la mafuta aliposema kwamba kodi hamna, watu tumeshangilia. Hakuna hata Mbunge mmoja amesema aah, hapana. Kwa nini? Serikali itapata wapi fedha jamani? Mwakani tumeomba tupewe na Mfuko wa Jimbo, fedha zitoke wapi? Mfuko wa Jimbo fedha zitatoka wapi Serikalini? Basi ikiwezekana toa ushuru wote tuangalie, barabara zitajengwa mwakani. Jamani ni lazima sisi tusiwe tunalaumu tu, tuangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa nataka nichangie suala la afya. Naipongeza Wizara ya Afya kwa kuweza kunijengea hospitali jimboni kwangu Bububu. Nashukuru sana na ningependa pia Waziri anapokwenda kule, basi anikumbuke twende pamoja. Wananchi wa Bububu wamefurahi sana. Lakini pamoja na hayo Wizara ya Afya kuna wafanyakazi wetu hapa Manesi pamoja na Madaktari ambao kwa kweli wanakabiliana na maradhi ya kuambukizwa. Sasa naomba tu wakatiwe Bima za Maisha. Ni vyema wakakatiwa Bima za Maisha ili tuwape motisha. Sitakuwa nazungumza *in detail,* nitakuwa nazungumza kidogo kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia suala la *TRA* Zanzibar. Naipongeza sana *TRA* kwa kuzidi kiwango walichokusudia. Mtu akifanya vizuri anasifiwa. Lakini Waswahili wanasema: "Mgema akisifiwa, tembo hulitia maji." Ndugu zetu pamoja na kufanya vizuri, lakini wafanyabiashara wa Jimbo langu la Bububu wamenituma, sijui kwa sababu ni Mbunge wao au kwa sababu mimi wameniona ni Msukuma au Mnyamwezi! Lakini jamani mnaniona napeleka madai yenu? Nayawasilisha kwa Mheshimiwa Waziri ambaye naye ni Mzanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema *TRA* inawahumiza Dar es Salaam, wanalipia ushuru magari yao/bidhaa mara mbili. Kwa nini? Wanataka kufahamu *TRA* Zanzibar na *TRA* Bara Dar es Salaam ni *TRA* tofauti? Kama ni tofauti, basi Zanzibar liandikwe jina lingine isiwe *TRA,* wajue kwamba kumbe hiyo sio *TRA.* Lakini kama ni sawasawa, kwa nini watofautiane? Bidhaa zinatoka Tanzania Bara zinakwenda kule, kwa mfano magari zikifika kule hamna ushuru. Huku hakuna *road licence,* ikifika kule yanakwenda magari wala hawaulizwi *road licence*. Namwomba Mheshimiwa Waziri, suala hili halitaki gharama ni suala la kuwaita tu Watendaji wake wakae pamoja walitatue waangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa yako tu, tuna makabila yote ya Bara yako kule. Kuna Wanyamwezi, Wasukuma, Wandengereko, Wazaramo, Wamakonde, Wamakua hata Wamasai wapo na Wakwere wapo. Kuna Mtaa mmoja unaitwa

Kiwengwa, kuna Kijiji kinaitwa Monduli. Sasa hivi ukifika pale utacheza ngoma ya Wamasai. Watoto sasa hivi wanajua yero ni nani? Wanacheza ngoma za Wamasai, wanazungumza lugha ya Kimasai. Sasa ukishaanza kubagua Zanzibar ikoje, makabila ya huku yako kule wananunua magari yao, wakiona sasa wamechoka walete huku, anakuja hapa unamwambia gari ushuru mara mbili. Kwa nini? Usumbufu. Mimi sizungumzii suala la *registration,* lenyewe liko *automatic* pamoja na huo usumbufu wa magari kwa sababu ukileta ZNZ, basi utaambiwa sijui *plate number* laki tatu. *How comes?*

Kwa hiyo, ninazungumza kwa machungu kwa kweli, hii inatusababisha Muungano wetu uzidi kuwa mbaya. Sisi tuko Zanzibar, mimi Msukuma, lakini ni Mbunge, hamwoni ajabu! Sasa kwa nini mtunyanyapae jamani? Tuna Mawaziri kule Mwakanjuki, mnamjua Waziri wa Mawasiliano, hakuna ubaguzi na CCM haibagui! Kwa hiyo, nazungumza kwa uchungu kwa sababu nimeona ni nafasi nzuri ya kuyasema haya. Ujumbe utakuwa umefika, hata nikisema namna gani lakini ujumbe ndio umefika, kero za wananchi wa Zanzibar, *TRA* inakera, irekebishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie kuhusu Sekta ya Ardhi. Naipongeza Serikali kwa kuwatambua wananchi ambao walikuwa wamejenga katika maeneo yasiyopimwa rasmi. Mipango ambayo inatayarishwa sasa hivi ya kupima Vijiji. Lakini ni kitu kimoja tu, naona sasa hivi ule muda, kibali kinachotoka wanaita *Resident Permit Certificate* miaka miwili, sasa lengo ni kwamba ile nyumba aliyopewa yule jamaa kwamba tupate mikopo, sidhani kama hakuna Benki itakayokupa mkopo kwa cheti chao cha miaka miwili. Sasa tunaomba uongezwe muda na ikiwezekana ilingane kabisa na kile cheti kinachotolewa na maeneo waliyopimwa ili wananchi wapate kutumia kwa mikopo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumze suala la SMZ kupata zile fedha asilimia 4.5 ya fedha za msaada. Mimi kilichonifurahisha sasa ni Tume ya Pamoja pande zote mbili kwamba sasa itakaa iangalie hili suala. Inaonyesha kwa kweli pesa ni kidogo asilimia 4.5. Sisi kwa kweli kama mtatupa asilimia 20 kwa miaka mitatu, basi tunamaliza mambo yetu, sisi tunarudi. Kwa kweli mwakani mimi nitaangalia kifungu kile kwa makini sana kiwe kimerekebishwa na ninawaomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, basi Kamati ziwasilishe maombi yao ili mwakani tuone mabadiliko haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la elimu. Kama nilivyowahi kuzungumza kwamba Wizara ya Elimu sasa hivi inasikitika kwamba vijana wengi hawapendi masomo ya sayansi, binadamu jamani ni mjanja.

Hata sisi mwaka 2010 tutakuwa na kazi jamani. Watu wanatuona tunazunguka kwenye viti humu, sasa mwaka 2010 fanya juhudi yako unazunguka hapa tutakuwa na kazi. Lakini tungekuwa tunakaa chini ya mazulia, tusingekuwa na kazi. Kwa hiyo, binadamu nataka kusema huwa anaangalia nini kule mbele aliyenitangulia aliyepitia mfumo huo vipi? Yukoje? Akiona maisha yake ni mazuri, basi atafuata mfumo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu nafikiri isimtafute mchawi, mchawi ni wenyewe Serikali. Kuna mfumo huu wa *engineering.* Mimi najua *engineering* ni

moja ya sayansi. Masomo ya Ufundi kwa kweli mfumo wake ulikuwa mbaya sana, una-*discourage*.

Kuna kitu hiki *Certificate in FTC* na *Advanced Diploma in Engineering* kwa kweli kilikuwa ni kipindi ambacho ni kigumu kwa watu hawa. *Marks* ni nzuri *Form Four* kwenda huko. *Division One majority* wanakwenda *FTC*, mimi nimepita. Lakini baadaye kuna masharti, lazima awe na *average CBP* aende *University*. Sasa jamani kuna watu ambao wana *average D* ambao wamekwenda Uingereza, wamerudi na *Masters*. Sasa hapa lazima uende sijui na *average CBP*.

Pamoja na hivyo wanaobahatika kulingana na *Advanced Diploma* nao sasa inalazimishwa. Sijawahi kuona mfumo nchini kwamba mtu anasoma *Advanced Diploma* anatahiniwa na Baraza la Mitihani. Aah! Inakuwakuwaje jamani? Nisome miaka mitatu halafu uje unitanie hujui

Sasa mimi ninachoshangaa hapa Ma-*engineer, Engineer* Manyanya huzungumza kwa nini? Wamenyanyaswa watu hapa! Kuna kesi nyingi hapa za Vyuo kama hivi kama *DIT* na vingine. Juzi juzi hapa wamefukuzwa wamekwenda Mahakamani wameshinda. Ile *engineering*, yaani *science* kwa kweli hatuitaki. Lakini nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hatua ambazo ameanza kuchukua. Kwanza ku-*reshuffle* lile Baraza la Mitihani. Mitihani ilikuwa inatembea kama nyanya. Unaambiwa mtihani wa Taifa Darasa la Saba mwaka 2007, wewe mwaka 2006 unaambiwa huu hapa, kwa kweli ilikuwa ni tatizo.

Lakini nataka kusema kwamba wale *Engineers* ambao wamemaliza Chuo Kkuu au amemaliza wapi, maisha yao kwa kweli yanakuwa duni sana. Hawa ni wanasayansi jamani. Sasa kama maisha yao ni duni, nani atapenda watoto waende huko? Wao wanajua baba hali mbaya, yeye mwenyewe baba atamwambia hakuna *engineering*, nenda Uhasibu. Mimi nakwambia nawafahamu watu waliosomea *FTC* wakaenda Chuo cha Uongozi wa Fedha, sasa hivi ndiyo hao tunazungumza *TRA* wanatuhangaisha. Wanakusanya mapato wana matumbo hayo kwa kweli! *(Makofi)*

Kwa Wahandisi wetu tuwaangalie. *Engineer* Manyanya mbona hujayazungumza! Tuwaangalie! Ndiyo, Wanasayansi tuwaangalie, ndiyo maana nikasema hawa watu walio-*design* kitu hiki wapewe kumbukumbu maalam. Nimezungumza makusudi, hili kwa kweli hatutajivunia kitu cha nje.

Mheshimiwa Naibu Spika Naomba kuunga mkona hoja. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia hoja ambazo zimewasilishwa hapa Bungeni. Naomba nichukue nafasi ya pekee kwa kuwapongeza Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango na Uwekezaji pamoja na wataalam wao kwa kuweza kuandaa Bajeti hizi na kuwasilisha kwetu hapa Bungeni.

Kwa namna ya pekee, naomba niipongeze Serikali kwa kulipa suala la uhifadhi wa mazingira kipaumbele na pia naomba niwapongeze Waziri wa Maliasili na Waziri wa Nchi , Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa kuandaa mikakati madhubuti ya kuweza kupambana na suala la udhibiti wa mazingira ya hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi michango yangu itakuwa ni midogo tu. Kwa sababu mengi yameshachagiwa na wengine naomba niende moja kwa moja kwenye Sekta ya Kilimo. Sekta ya Kilimo kwa hapa Tanzania kila mmoja anafahamu kwamba ni uti wa mgongo wa uchumi wetu. Lakini inasikitisha kuona kwamba sekta hii siku baada ya siku inazidi kushuka. Kwa kweli inasikitisha sana.

Hapo nyuma Sekta hii ilichangia kwa sehemu kubwa pato la Taifa. Ilichangia kwa sehemu kubwa kwa sababu, natumaini kabisa kipindi hicho ilipewa kipaumbele na Serikali. Wakulima waliangaliwa kwa karibu walipewa pembejeo, waliangaliwa hata bei ya mazao yao, Serikali ilifuatalia mpaka kuona kwamba bei ya mazao wanayolima wakulima wanapata bei inayolingana na thamani ya mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini leo ninavyoona ni kwamba Serikali bado haijaanda mkakati kabambe wa kuweza kuboresha Sekta hii ya Kilimo. Tunapozungumzia Mikoa iliyoendelea kwa mfano Kilimanjaro, Kagera na Mbeya ukiangalia msingi wa maendeleo ya Mikoa hiyo inakuta ni kilimo. Leo Kilimanjaro inaongoza kwa maendeleo, ukiangalia kabisa utaona kwamba zao la kahawa ndilo lililosaidia Kilimanjaro ikawa hapo sasa hivi.

Kulikuwepo na mashamba makubwa *estate* tunaziita, wakulima wadogo wadogo, kila mmoja alikuwa na shamba lake. Lakini waliangaliwa kwa karibu sana. Bei zilikuwa zinapanda za kahawa, mimi mwenyewe na wengi hapa Bungeni watathibitisha kwamba tulisoma kutokana na kilimo. Lakini mwananchi wa sasa hivi hawezi kusomesha mtoto wake kwa kilimo kwa sababu hata akilima vipi, kwanza ni ngumu kulima kwa kiasi kikubwa, hana pembejeo; pili, hata akilima bei ya mazao yake bado ni ndogo mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Tabora ni wakulima wazuri sana wa tumbaku, lakini cha ajabu tumbaku ile haiwafaidishi kabisa mpaka sasa hivi. Tangu mwaka 2000 bei inafahamika kwamba ni Sh. 1,570/= kwa kilo ya tumbaku. Lakini mkulima anapata Sh. 700/= mpaka sasa hivi. Huyo mkulima atajikomboa lini kutokana na kilimo?

Halafu pia naiomba Serikali ione kwamba kutoa ruzuku peke yake kwenye pembejeo bado haijafanya kazi ya kutosha. Kwa sababu kule Tabora kuna Benki ambazo zinatoa pembejeo kwa kupitia Vyama vya Ushirika. Wanakopeshwa wakulima kwa ajili ya kusaidia kulima mazao yao. Lakini ni kichekesho cha ajabu kabisa, mkulima anakopeshwa pembejeo mazao ya mwaka mzima anayoyalima na kuuza, hayatoshi kulipa pembejeo ile aliyokopeshwa. Kwa hiyo, kwa mwaka mzima anauza mazao yake na anaambiwa bado unadaiwa. Kwa hiyo, mwakani bado ulime uweze kufidia deni, anajikuta hajafaidika na pembejeo zile na hajafaidika na kile kilimo kwa mwaka mzima. Kwa hiyo, unakuta mwananchi anabaki kuendelea kuwa masikini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kabisa Sekta ya Kilimo ndiyo pekee inayotoa ajira kwa watu wengi pamoja na vijana wengi sana. Wakati tukiwa na *estate* nyingi, tukiwa na mashamba ya mifugo ambayo tunayaita *ranches*, vijana wengi waliajiriwa kwenye Sekta hizo na waliweza kujipatia maendeleo na maisha kwa ujumla. Leo mashamba yote yamekufa. Hata ukitembelea Kilimanjaro, leo mashamba makubwa ya *coffee* yamekufa. Tunataka mipango iwepo, Serikali iseme kwamba imeandaa mkakati gani wa kuweza kufufua yale mashamba ambayo yalisaidia kutoa ajira kwanza kwa vijana kule Vijijini; pili, hata vijana walioendea mpaka Vyuo Vikuu.

Kuna Vyuo vya Kilimo vilianzishwa, kwa sababu kulikuwepo na mashamba hayo walipotoka Vyuoni waliweza kwenda kufanya kazi kule. Kuna mashamba ya mifugo, kuna vijana walimaliza digrii za mifugo wakijua kwamba wana sehemu za kwenda kufanyia kazi. Leo tuna vijana wana-*graduate* toka Vyuo Vikuu hawana sehemu za kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali itakapobuni mpango kabambe wa kuweza kuboresha Sekta hii, kwanza itakuwa imeondoa umaskini kwa mtu mmoja mmoja; pili, itakuwa imesaidia ajira kwa vijana wanaotoka Vyuo Vikuu ambavyo tunazidi kuviongeza hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye suala la madini. Kinachochangiwa kutoka Sekta ya Madini kwenye pato la Taifa Tanzania ninaona *a peanut* kabisa. Ni kidogo mno, hakilingani na thamani ya madini hayo kwa wananchi wa Tanzania! Tanzania tumejaliwa tuna maliasili nzuri, tuna madini kila kona, lakini wanaofaidi maliasili hii ni watu wa nje, sio Watanzania.

Sasa hivi Serikali iko kwenye mikakati ya wataalam waanze kuchunguza maeneo mengine ya kuachimba madini. Lakini hata yale machimbo machache ambayo tunayo hatujaweza kuyasimamisha kikamilifu na hii ni kwa sababu sisi Watanzania bado hatuna wataalam wa kutosha kuweza kusimamia madini hayo. Sasa yanasimamiwa na wawekezaji kutoka nje ambao kazi yao wale ni wafanyabiashara. Wanachokifanya ni kuhamisha kutoka hapa kwenda kusaidia uchumi wa nchi zao. Sisi bado tunabaki masikini na tutaendelea kubaki masikini. Pamoja na kuwa tuna rasilimali nyingi, lakini hatujaweza bado kuzitumia kikamilifu.

Mimi ninaiomba Serikali, badala ya kuendelea kuingia mikataba mingine ya kufanya utafiti wa wapi tuchimbe madini, kwanza ichikue mbinu na mikakati ya kusomesha vijana wa kutosha kwenye *level* ya kuweza kusimamia machimbo hayo. Baada ya hapo, wawekwe kwenye hayo machimbo waweze kusimamia kikamilifu. Baada ya kuona tunapata nini kwanza kutoka kwenye machimbo yaliyoko sasa hivi, ndiyo baadaye tuanze kuchimba mengine ambayo yako chini. Tanzania tuna madini mengi na hili hata Mwalimu Nyerere alitambua hilo, alijua kabisa kuna madini, lakini kwa kujua kwamba bado hatujafikia kwenye *level* ya kuelewa vizuri, akaona ni bora yakae huko chini vizazi vijavyo vije viyafaidi. Watakuja na mbinu mpya na mkakati mpya wa kujua ni jinsi gani wachimbe na ni jinsi gani wasimamie kuweza kufaidisha Taifa hili.

Lakini tusije tukawa watizamaji kana kwamba rasilimali hii inahamishwa na wajanja wachache taratibu huku tukiwa tunachekelea tukisema kuwa tuna Mikataba. Ni dhahiri kabisa hata Mikataba ambayo ipo sio mwananchi wa kawaida, sio Mbunge, sio viongozi, kila mmoja anatambua kwamba haitunufaishi sisi. Hata hivi karibuni, Naibu Waziri wa Nishati amesema kwamba kuna usiri mkubwa sana kwa wale wanaosimamia hiyo migodi. Bado hakuna ukweli. Kwa hiyo, wanaficha mambo mengi. Lakini sasa kinachoshangaza ni kwamba tunaendelea kuchunguza tupate wapi migodi mingine. Tuliyonayo sasa hivi hatuwezi kuisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali ingalie suala hili kwa makini kabisa ili maliasili yetu iweze kunufaisha jamii hii badala ya kuendelea kulia kwamba sisi ni masikini wakati mali zetu zinakwenda kunufaisha Mataifa ya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Utalii, Watanzania tumejaliwa, tuna maliasili nzuri tena za kupendeza ambazo kama tungeweza kuzitumia kikamilifu, tusingekuwa leo na uchumi ambao ni tegemezi. Lakini uchumi wetu ni tegemezi kutokana na kwamba hatujaweza kuutumia kikamilifu hizo fursa zetu tulizokuwanazo. Tuna vivutio vingi ambavyo vipo lakini havifikiki kwa sababu hakuna miundombinu. Tuna vivutio vingine vipo lakini havitambuliki kwa sababu havijatangazwa kikamilifu. Kuna maeneo mengine ambayo kwa kweli bado Serikali hayajayaangalia kikamilifu ili tuweze kujitangaza vya kutosha na tuweze kupata fedha kutoka nje.

Ninaiomba Serikali iangalie kwa makini, ianze kuboresha miundombinu katika maeneo ya Kusini. Tukiangalia sasa hivi maeneo ya Kaskazini miundombinu ni mizuri, ndiyo maana watalii wakija wanaelekea upande mmoja. Lakini Kusini bado tuna vivutio vizuri sana havijatangazwa kikamilifu *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nchi ya Kenya ambao mimi nimepata bahati ya kuitembelea, *almost National Parks* zote za Kenya ukiziangalia kwanza namna wanavyohifadhi ni tofauti na sisi. Wenyewe wameweka *fence* kwa ajili ya kufungia wanyama wakae, lakini kwa *nature* ya mnyama anatakiwa awe *free range*. Sisi tunahifadhi inavyotakiwa, wanyama wetu tumewaachia wako *free* lakini unakuta watalii wengi bado wanakwenda Kenya, ni kwanini?

Ukiangalia hawana hata ile *nature environment* nzima. Ya Kenya sio nzuri kama ya Tanzania! Lakini ukiangalia watalii bado wanakwenda kule kwao, kwa sababu wanatangaza kwa juhudi kubwa. Mlima wetu wa Kilimanjaro kwa upande wa Kenya unaingiza hela tofauti na tunavyoingiza sisi hapa Tanzania. Yote haya ni kutokana na kwamba wamewekeza kwenye utalii, wanatangaza inavyotakiwa na wanapata mapato mengi sana. Pato kubwa la sehemu ya Kenya linaongozwa na Sekta ya Utalii na hiyo ni kwa sababu ya mbinu madhubuti wanazozitumia kutangaza utalii wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba, Tanzania tuna *opportunities* nyingi sana, kinachotakiwa ni mipango mizuri ya kuweza ku-*utilize* hizo *opportunities* ili iweze kutuletea pato la kutosha, tusiendelee kuwa tegemezi. Ni aibu kabisa! Kwa sababu nchi nyingi zinafaidika na maliasili ya Tanzania hii. Nina imani kabisa kama Serikali ya

awamu hii itakuwa makini ndani ya miaka mitano, kwa kweli hata kama tutakuwa tegemezi, ni kidogo sana. Lakini tutakuwa tumejitosheleza kwa sehemu kubwa na wananchi wetu watakuwa wameondokana na umasikini, ujinga na maradhi ambayo tunalia nayo kila siku.

Tukimsaidia mwananchi mmoja, tumesaidia Taifa zima kwa sababu maendeleo yanaanzia kwa mtu mmoja, yanakuja ngazi mbalimbali mpaka yanafika juu. Haisaidii kusema kwamba uchumi unakua wakati mwananchi wa chini bado ni maskini, bado magonjwa, bado hili na lile. Ni oungo kusema kwamba uchumi wetu unakua wakati huo wananchi bado wana hali ngumu.

Lakini nina imani kabisa kama Serikali ya awamu hii itakuwa makini kuweza kutumia vizuri hii maliasili yetu na kupanga mikakati dhahiri, tutaondokana na hali hii na kuweza kuwasogeza wananchi wetu kuwapeleka mahali ambapo tunatarajia na wenyewe pia wanatarajia kwamba watakuwa katika hatua nzuri kwa sababu wana imani kubwa na Serikali ya awamu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hii hotuba ya Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango. Nichukue nafasi hii kwanza kuishukuru Serikali kwa jinsi inavyotekeleza majukumu yake na kwa jinsi inavyopambana na matatizo ya nchi hii kwa kadri yanavyojitokeza. Ni ukweli usiofichika kwamba awamu hii ni awamu ya kasi mpya kwa maana ya Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Baraza lote la Mawaziri. Nami ninayo mifano hai ambayo inaonyesha kwamba ni kwa kiasi gani awamu hii inajitahidi sana kutekeleza au kupambana na matatizo kwa jinsi yanavyojitokeza

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka mitano iliyopita kule Jimboni kwangu Musoma ni Mawaziri wasiozidi watatu katika kipindi chote cha miaka mitano walifika. Lakini safari hii chini ya miezi mitano wameshafika Mawaziri zaidi ya sita. Kwa hiyo, hii inaonyesha ni kwa kiasi gani Serikali inajituma katika kutekeleza majukumu yake.

Napenda sasa nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Fedha kwa namna ambavyo ameweza kuwasilisha Bajeti hii na kwa kweli Bajeti ambayo inaonyesha kwamba ina lengo la kumsaidia mwananchi hasa mwenye kipato cha chini na hasa kwa wale watumishi. Hili tumeliona wazi kwa jinsi ambavyo Serikali katika awamu hii imejitahidi kuwakumbuka watumishi kwa maana ya kuwaongezea kipato cha mishahara yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii sio kwamba itapunguza ukata wa maisha yao, lakini vilevile itasaidia kuleta hali ya utumishi katika utendaji wao wa kazi. Nami sasa nazidi kuiomba Serikali hebu izidi kuweka nguvu zaidi katika maslahi na mishahara ya watumishi hawa. Maana ni ukweli usiojificha kwamba mishahara hii ambayo watumishi

wamekuwa wakilipwa kwa kweli ni mishahara ambayo haikidhi mahitaji ya watumishi hawa. Mathalani mtumishi analipwa Sh. 60,000/=, tafsiri yake ni Sh.2,000/= kwa siku. Akienda kazini kwenda na kurudi lazima atumie Sh.600/= kwa ajili ya daladala, hata angejibanaje lazima atumie Sh. 500/= kwa ajili ya chai. Sasa matokeo yake ni kwamba kwa siku anarudi nyumbani na Sh. 900/=, asomeshe watoto, awapeleke watoto hospitali pamoja na familia iweze kuishi. Kwa hiyo, kwa kweli ni kiasi ambacho kimekuwa hakitoshi kabisa.

Mimi bado ninaona mifano hai katika yale maeneo yote ambayo Serikali imejaribu kuyaboresha, ni kwa kiasi gani ambapo hata wale watu wanajaribu kufanya kazi. Labda nitoe tu mifano michache, leo unapozungumza kwamba labda Askari Polisi wanakula rushwa, kwa kweli lazima tukubali kwamba kitu kikubwa kinachochangia ni kipato kidogo wanachokipata.

Mimi nakumbuka mwezi jana Naibu Waziri wa Usalama wa Raia alikuja katika Jimbo langu la Musoma na tukaweza kutembelea Kambi ya Askari Polisi. Kwa kweli ulikuwa ukifika pale huwezi kuamini macho yako. Tuliweza kuingia katika yale makazi yao Askari Polisi wanalala kwenye ukumbi. Sasa ndani ya ule ukumbi kila Askari ameweka maturubai tena yale ya Wakimbizi. Sasa unajiuliza, kwenye hicho chumba kimoja kuna Askari zaidi ya sita. Kwa hiyo, katika maisha kama yale kwa kweli hata wanaokwenda kazini wanakuwa hawana hata moyo wa kufanya kazi.

Kwa hiyo, ndiyo maana nasema kwamba katika hili suala la mishahara, basi Serikali iendelee kuongeza. Leo ukiangalia kwa mfano Idara ya Wanayamapori, kwa jinsi wanavyowajali wale watumishi wao Maasakri, mtu ana hiari aache Uaskari kwenye Jeshi la Polisi akiwa na nyota aende kule aanze moja, kwa sababu kule kipato wanachokipata ni kizuri na ndiyo maana hata kule mambo ya rushwa ni mara chache sana kusikia.

Lakini sio hapo tu, labda nizungumzie ndugu zetu wa *TRA*. Tukikumbuka sio muda mrefu, miaka tu ya nyuma walikuwa wanakusanya chini ya bilioni 25 na wakati wanakusanya hivi, kila mmoja alikuwa akisimama anasema *TRA* wanakula rushwa na kwa kweli walikuwa wanakula rushwa sana na hili walikuwa wanafanya kwa kweli, kipato chao walikuwa hawapati chochote. Lakini baada ya kuwa wameboreshewa, leo hawana *complain.* Pamoja na kwamba sio kweli hawali kabisa, lakini ni kwamba wanajitahidi sana katika kutokula rushwa. Lakini vilevile kazi wanayoifanya leo tumeona wameshaongeza makusanyo kutoka bilioni 25 mpaka leo wanakimbilia ziadi ya bilioni 200. Kumbe hili linawezekana tu kwa sababu angalau kipato chao kidogo kinaruhusu japokuwa naamini bado wangehitaji kuongezewa, lakini bado tuwaambie hata haya makusanyo hebu waendelee kuongeza. Maana tumeambiwa kwamba wenzetu wa Kenya wanakusanya mara mbili yetu, basi angalau wajitahidi ikiwezekana siku wafike kwenye bilioni 300.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili suala la mishahara kwa kweli linahitaji liangaliwe katika kada zote kwa maana ya Waganga, Manesi, mabwana shamba, watumishi wa Halmashauri na wenzetu kule Waheshimiwa Madiwani wale ndiyo uache na kusema. Maana unampa uwezo wa kuamua kwa mwaka matumizi ya Shilingi bilioni

tano, lakini huyo Diwani unamlipa Sh.30,000/=, hivi unategemea nini? Kwa hiyo, ni kwamba katika hali hii, basi ndiyo maana wakati wote tunalia tunasema hawafanyi kazi zao, lakini tatizo kubwa linalosababisha yote haya ni kwa sababu ya vipato vidogo wanavyovipata.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kwa ufupi sana suala la uwezeshaji. Tunapozungumzia suala la uwezeshaji, kwa kweli ninaamini ni suala muhimu sana katika kumsaidia mwananchi wa kawaida na hili Serikali yetu imelizungumza, viongozi mbalimbali wamelizungumza, lakini hata Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi imetamka wazi katika ukurasa wa 66 Ibara ya 48 kwamba kwa kweli inajukumu la kumwezesha mwananchi ili aweze kujikomboa kutoka kwenye hili dimbwi la umasikini. Lakini hata katika hotuba ya Waziri wa Mipango, tumesikia ukurasa wa 68 na 69 amezungumzia suala la uwezeshaji.

Waziri wa Fedha katika ukurasa wa12 amezungumzia uwezeshaji. Lakini hata Mheshimiwa Rais wetu wakati anatoa hotuba yake tarehe 30 mwezi Desemba mwaka jana 2005, naomba kunukuu mambo machache. Alisema kwamba: "Tutawawezesha Watanzania kwa makundi. Kundi la watanzania ambao ni wasomi na kundi la pili la Watanzania ni wale wenye miradi midogo sana na miradi midogo, na mikubwa, ya kati na kundi la tatu ni kundi la wakulima wadogo, wavuvi na wafugaji wadogo."

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tujiulize hivi ni kwa kiasi gani sasa Serikali imejiandaa kuyawezesha haya makundi ili yaweze kujikomboa. Maana leo unapozungumza naona kaka yangu Waziri wa Kazi bahati nzuri unaniangalia kwa makini. Unakumbuka kabisa kwamba katika Mikutano yetu na katika ilani zetu, tumeendelea kuwahamasisha watu wajiunge katika makundi ili Serikali iweze kuweka mkono. Waheshimiwa Wabunge wamehamasisha kweli na hata mimi katika Jimbo langu la Musoma watu wengi sasa wamejiunga katika *SACCOS*. Sasa wanasubiri nguvu yako Mheshimiwa Waziri waone kwamba utafanya nini.

Lakini sio hapo tu, hata tukienda katika Wizara ya Elimu, mimi nashukuru kwa mwaka huu kwamba Wizara ya Elimu imeshirikiana na wananchi wa Jimbo la Musoma. Tunashukuru kwamba katika Elimu ya Sekondari wale watoto waliofaulu katika Jimbo la Musoma wamekwenda Sekondari kwa asilimia mia moja. Lakini hizi zote ni juhudi ambazo wale wananchi wamezifanya kwa kushikiana na Serikali. Lakini sasa wamekwenda Sekondari kwa maana watamaliza Kidato cha Nne, lakini baada ya hapo Serikali imewawekea mazingira gani, kwa maana ya katika kuendelea katika *High School* na Vyuo Vikuu?

Mheshimiwa Nabu Spika, hii Wizara imejiandaje kuongeza angalau *Diploma* katika hivi Vyuo vya *VETA* ili basi visiambulie kutoa *Certificate* tu? Lakini hata wale ambao wanabaki hivi, sasa Serikali inawasaidiaje?

Kwa hiyo, haya yote ni makundi ambayo bado yapo na yanahitaji msaada wa kuwezeshwa. Kwa hiyo, haya yote ni baadhi ya maeneo ambayo yanahitaji kupewa kipaumbele zaidi katika kuwezeshwa. Leo tunazungumza suala la kilimo, lakini bado

watu wetu wengi kwa asilimia kubwa wanatumia kilimo cha jembe la mkono na hiki kilimo cha jembe la mkono tunajua kabisa kwamba hakiwezi kumkomboa mwanachi wa kawaida. Kama hivyo ndivyo, hivi tumejiandaaje katika kuwasaidia hawa wakulima wadogo? Kwa hiyo, hizi zote ni changamato tulizonazo na tunahitaji kuzifanyia kazi ili tuweze kuona ni namna gani tutaweza kuwakomboa hawa watu wa kawaida. Lakini sio makundi ya hawa watu wadogo tu, hata haya makundi ya kati na makundi makubwa.

Mheshimiwa Nabu Spika, kwa ajili ya uharaka wa muda, ningeomba nichangie kwa ufupi sana suala la ujenzi wa reli ya Tanga Musoma. Suala hili la reli ya Tanga - Musoma limezungumzwa katika ilani kwamba itajengwa reli hiyo ya Tanga - Musoma ambayo itasaidia kusafirisha mizigo si tu ndani ya nchi. Lakini vilevile hata katika nchi za jirani, ipo nchi ya Uganda, Rwanda, Burundi na Congo. Hawa wote leo ukija kufanya utafiti ile Bandari ya Mombasa ni Bandari ambayo haiwatoshelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa haiwatoshelezi, hivi sasa kile kitendo cha hii reli kujengwa ingetupatia nafasi nzuri ya kuweza kuwavuta hawa wote wakaweza kuitumia reli hii katika kuhakikisha kwamba kumbe tunaingizia Taifa letu kipato ambacho kingesaidia kukuza uchumi wa nchi yetu. Lakini, ukiangalia katika Bajeti, hakuna mahali limezungumzwa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda wakati Mheshimiwa Waziri anafanya majumuisho, atajaribu kutueleza Serikali ina mpango gani kuhusiana na hii reli na ambayo kwa kweli kwetu sisi Musoma ingesaidia sana kwanza kuongeza ajira, lakini vile vile kuongeza kipato, sio cha watu wa Musoma tu, lakini vile vile kipato cha Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajili ya muda, nakushukuru sana. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Njombe Magharibi kwa imani yao ya kuniwezesha nije katika Ukumbi huu wa kifahari, wa kisasa. Kwa kweli nawapongeza sana, nawashukuru sana huko waliko Njombe Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kazi nzuri anayoifanya pamoja na Baraza lake la Mawaziri na Waziri Mkuu jinsi wanavyochapa kazi na jinsi maendeleo yanavyokuja kwa kasi kama wananchi walivyokuwa na imani naye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu nimepewa muda wa kuchangia hii Bajeti ya Wizara ya Fedha, Mipango na Uwezeshaji, kwa kweli nilikuwa na mengi ya kuzungumza ,lakini naona mengi wameshaongea wenzangu. Sasa ni vizuri nijikite kuchangia kwenye Jimbo langu kwamba hii Bajeti watu wa Jimboni kwangu kwa kweli wameipokea kwa mikono miwili ingawaje wao wanalalamika kwamba Jimbo la Njombe Magharibi huwa mara nyingi kwa vile sijui liko mpakani mwa Mbeya huwa linasahaulika. Hali siyo nzuri kule, hasa kwenye huduma za kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia kuhusu suala la mbolea ya ruzuku. Mbolea ya ruzuku watu wa kule wanapenda ije mapema zaidi, yaani ifike mwezi wa Nane au wa Saba. Inapokuja mwezi wa Kumi na Moja, kuna baadhi wanaridhika, lakini kuna sehemu nyingine kama Kata ya Igosi, Kata ya Imalinyi, kwakweli wanaona haiwasaidii. Kwa hiyo, tunaomba Serikali kwa sababu wapo hapa, ile mbolea ya ruzuku iwahishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kitu kingine waliniagiza kuhusu suala la usimamizi. Usimamizi siyo mzuri. Kuna hii mbolea ya ruzuku, wengine wananufaika, wajitajirisha hasa wafanyabiashara. Kwa hiyo, unaweza ukaona usimamizi unakuwa siyo mzuri pamoja na kwamba kuna sehemu nyingine wamepata mbolea, sehemu nyingine walikosa kabisa, kiasi kwamba imesababisha kuwepo na njaa. Kwa hiyo, hilo nalo wanasema usimamizi ni vizuri ungefanyika kwa upande wa *SACCOS*.

Hizi *SACCOS* zetu kwa kweli ndio mkombozi kwa mwananchi wa kawaida hasa wa kipato cha chini. Kwa hiyo, tuombe Serikali iimarishe hizi *SACCOS*, hivi Vyama vya Kuweka na Kukopa vingekuwa na msaada mkubwa sana. Pamoja na kwamba kwenye Jimbo langu, watu wanajitolea sana kujiunga na *SACCOS*, lakini kuna baadhi ya watumishi kwa nia ya ubinafsi tu, wanakwamisha juhudi za wananchi za *SACCOS* na bahati nzuri nimesha lalamika kwa Waziri wa Kilimo na Ushirika na Naibu wake, nilipiga kele sana. Nadhani amelifanyaia kazi.  Wale watumishi ambao sio waaminifu wanaokwamisha juhudi za Ushirika, nadhani atalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine nataka nizungumzie kwenye Jimbo langu kwamba, suala la simu za mikononi, kwao imekuwa ni tatizo. Kuna kipindi fulani nilielezea kuhusu hao wenzetu wa *Vodacom* wangekuja kwenye Jimbo langu. Kuna Vijiji kama vya Igosi, Kidugala, kuna huduma kubwa za sekondari, huduma za nini, watu wanapata sana shida ya mawasiliano. Kuna siku niliwaeleza kwamba watu wangu wanapata mawasiliano kwa taabu sana. Wakati fulani wanalazimika kutegea muda fulani wa usiku au jioni, wanapanda kwenye kaburi, wanasimama ndiyo wanapata mawasiliano. Au wakati fulani wanakaa kwenye mti mrefu pale Igosi. Watu walifikiri ni utani, ndiyo wanapata mawasiliano. Sasa tuna hofu wananchi wangu wasije wakaanguka na wanaweza wakapata madhara nikashindwa kupata kura tena mwaka 2010. Watu wa *Vodacom* na *Celtel* kama wananisikia, waliangalie kwa makini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine, nizungumze suala la Vinyungu. Hivi vinyungu, yaani kilimo cha umwagiliaji, watu wanapokuwa kwenye maeneo ambayo kuna maji, isiwe ni kero au adhabu kwao, kwamba waanze kunyanyaswa kwamba wahamishwe, wasitumie yale maji ambayo Mwenyezi Mungu amewaletea pale. Kuna baadhi ya watumishi ambao siyo waaminifu, wanapopewa masharti kwamba wananchi wasilime kwenye vyanzo vya maji, wao ile kauli wanaitumia vibaya. Wanaanza kunyanyasa watu. Kwa mfano, wananchi wangu wa Malangali katika Kata ya Luduga wanasumbuliwa sana. Sasa, wale watu ina maana wafe! Kwa sababu miaka na miaka vile vyanzo vilikuwepo na ndiyo maisha yao yalikuwa yanategemea.  Siku za nyuma, wananchi wetu

walikuwa wanakimbilia Tanga kwenye Manamba, sasa hivi wanaona njia mbadala ni kulima kilimo cha umwagiliaji.

Kwa hiyo, ninaiomba Serikali, pamoja na kwamba inazuia, itafute njia mbadala. Kwa mfano ikawawezesha kutengeneza mabomba pale wakawa wanamwagilia au kutengeneza mabwawa makubwa wakawa wanamwagilia, wakaendesha maisha yao. Kwa sababu unapomnyima, unaposema asizuie maji, halafu! Inatakiwa iangalie njia mbadala, kwa sababu badala ya kusema kuna MKUKUTA au huu MKURABITA, itakuwa hatujasaidia wananchi wa kawaida na mimi ndiye Mwakilishi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, nizungumze kuhusu suala la pale Mpanga, hizi *Game Reserves,* Maliasili. Kwa kweli, lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba mwananchi anapata unafuu wa maisha. Mtu ameishi miaka na miaka kwenye Kijiji cha asili pale, wanasema kuna Mbunga za Wanyama. Mbuga za Wanyama, lengo ni kusaidia wananchi ambao wako kwenye maeneo yale. Sasa inavyotokea, zile Mbunga inakuwa kama ni kero kwa wananchi. Wanaanza kunyanyaswa, wanafukuzwa, halafu mbaya zaidi wakihamishwa zile fidia hawalipwi na kama wakilipwa inakuwa kiduchu. Unampa mtu mzima Sh.50,000/= fidia akajengee nyumba, au Sh.100,000/= au Sh.200,000/=.

Kwa hiyo, tunaelewa kwamba labda kuna ujanja ujanja, hela zinakuja kwa wingi, zikifika pale wanadanganywa. Halafu wengine ndiyo mpaka sasa hivi wamekuja wanaandamana kwangu, mimi Mbunge kwamba wanahitaji fidia tena, vijana wenzangu ambao wanateseka, ni nguvu kazi. Walikuwa wanalima pale, wanahamishwa kwa nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali nadhani mnanisikia. Ni vizuri wale watu mwangalie upya kwa sababu nimekwenda hata kwa Mkuu wa Wilaya, bado ninaona ni kama ananizungusha zungusha tu. Kwa kweli watu wanapata tabu na mimi ndiye Mwakilishi wao. Kwa hiyo, ndiyo hilo nilitaka nichangie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni suala la lumbesa. Sijui kama nitakuwa narudia tena! Hii lumbesa hasa kwa wakulima wa Igosi pale wanateswa, hakuna vipimo maalum. Hao wafanyabiashara wanakwenda kuwalangua wananchi wangu na kwa sababu hawana jinsi wanauza kwa hasara kubwa. Magunia yanayopelekwa pale, unaweza ukaona yanakuwa ni makubwa sana kupita kiasi na wanaibiwa. Ilitokea baadhi ya wananchi wangu walivunjika migongo kwa sababu ya lumbesa. Sasa, nilikuwa nafikiria mamlaka zinazohusika ziangalie huu unyonyaji wa wafanyabiashara wanaowalangua, hasa tatizo ambalo lipo kwenye Vijiji vya Igosi na Imalinyi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, nataka nizungumzie kuhusu suala la mambo ya hizi Halmashauri. Hizi Halmashauri kwa kweli kwa sisi Wabunge huwa tunanyanyasika sana. Inabidi tuwe tunawabembeleza sana Wakurugenzi ili walete maendeleo kwenye Majimbo yetu. Nitatoa mfano kwenye Jimbo la Wilaya ya Njombe.

Wilaya ya Njombe ina Majimbo matatu. Sasa pale, sisi Wabunge tuko watatu. Inatakiwa ujibembeleze sana kwa Mkurugenzi, useme kuna barabara, kuna maji, na kama huna uhusiano mzuri na Mkurugenzi, basi anakupiga dana dana. Nitatoa mfano.

Kuna hela zilikuja, Serikali ilileta hela nzuri tu, milioni karibu 300 kwa ajili ya Vituo vya Afya. Masikini, katika Tarafa zangu tatu, Mdandu, Imalinyi na Wanging'ombe, nilikosa hela kabisa! Sasa watu wangu wanaendelea kufa. Nimekwenda kumweleza Mkurugenzi pale, anaona kama nafanya mchezo. Kwanza hakuwa anasikiliza hata kusikiliza! Anasema kwamba sisi tulishapanga bwana! Ninyi mmepata hela za Zahanati. Sasa, watu wanazidi kufa na kule kuna maambukizi makubwa ya Ukimwi na kuna watoto yatima. Kwa hiyo, hili nilikuwa nafikiria kwamba tulipokuwa tunajadili kwamba kunakuwa na mfuko ule wa Maendeleo ya Jimbo, niliona kwa kweli badala ya kusema sasa hawa Wakurugenzi wawe nusu Miungu, wawe wanatunyanyasa Wabunge, tunasema ni ukombozi, kwa sababu mimi kwa kweli Jimbo langu liko nyuma sana.

Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria kwamba kama huu Mfuko wa *CDF*, hii *Consistuency Development Fund* ukianzishwa kama wenzetu wa Kenya, kwa sababu nilikwenda kule Nairobi, itakuwa ni mkombozi mkubwa. Badala ya kunyanyaswa sisi Wabunge kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu, itasaidia sana. Nazungumza kwa uchungu kwa sababu ni vitu ambavyo vinanikuta na inabidi nipiganie. Tarafa zangu tatu ya Mdandu, Imalinyi na Wanging'ombe, utashangaa Jimbo zima linakosa Kituo hata cha Polisi. Ukienda kwa Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa kwamba tunahitaji Kituo, anasema ujenge. Lakini, kuna majengo ambayo yanakaa bure tu. Wanasema tujenge wananchi wachangie. Sasa wananchi watachangia lini? Lakini kwenye Majimbo mengine wanasema wasichangie, kuna vituo vya Polisi. Kwa hiyo, wananchi wangu wanateseka, ujambazi unakithiri. Sasa, tutalilia wapi na watu wanalipa kodi?

Kwa hiyo, ninaishauri Serikali iangalie vizuri kwamba inapofika upande wangu, iangalie kwamba Jimbo la Njombe Magharibi na Mji Mkubwa ambao ni mashuhuri kwetu ni Ilembula. Ukifika Makambako au Njombe Mjini kule hakunihusu kabisa. Mimi kunakonihusu ni Ilembula. Kwa hiyo, nalilia watu wa Ilembula na Vitongoji vyake wapate maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hilo tu, hata baadhi ya viongozi wa Chama na Serikali wa Kitaifa, hawajaingia kule, wanaingia wachache sana, nawashukuru sana. Wanaishia Njombe pale Mjini. Sana sana wanakimbilia Makambako, imetosha. Kule kwa walalahoi kwenye Jimbo langu hawafiki. Utashangaa kwa mfano Mawaziri ambao wameingia kwenye Jimbo langu hakuna. Nafikiria kwa sababu tumeanza kwa kasi mpya na kwa vile wanasikia, watakuwa wanakuja kunitembelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nizungumzie kuhusu suala la utalii. Mimi nilikwenda Japan. Kule Japan kuna vivutio, lakini ukilinganisha na vivutio vilivyoko kwenye Jimbo langu pale Nyumbanitu Kata ya Mdandu, pale Mlebele kuna Kijiji cha jadi, kinaitwa Nyumbanitu. Kile Kijiji kwa kweli kina maajabu! Kizuri! Inavyosemekana, hata makabila mengi, kile ndiyo chanzo. Kwa hiyo, ninashauri kwa Waziri anayehusika na Mawaziri wengine kama wanataka kutembelea pale, tukipatengeneza vizuri panaweza pakaleta faida kubwa sana kwa Taifa. Watu wanashuka kwa ndege, wanakwenda kuangalia Kijiji cha jadi. Kuna kuku, kuku weusi. Sasa, hawa kuku weusi ni wa

kimaajabu, yaani kuna muda mzuri unaona wanaongezeka , lakini wengine ndiyo hivyo tena ni *natural*. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vivutio kama hivi, hata Japan havipo. Kwa hiyo, ukifika pale wale kuku kwa kweli ni wazuri na nategemea watu wengi watakuja kuviangalia vile vivutio. Kwa hiyo, kinachotakiwa pale ni uwekezaji. Kwa hiyo, tukipata wawekekzaji wazuri au Serikali ikaweka Jengo pale zuri, nchi yetu itakuwa tajiri sana. Marais wa nchi mbali mbali wakija wanafikia. Kwa mfano nilitegemea hata Rais leo, angempeleka pale Nyumbanitu aangalie yale mapango na vile vivutio vile. *(Makofi)*

Halafu kuna mimea ambayo wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sokoine huwa wanakwenda pale, makundi kwa makundi wanakwenda kusoma. Kuna mimea ambayo sehemu nyingine haipatikani. Kwa hiyo, ninachoongoza kwa kweli *I'm serious, it's a good place*, panaweza pakatusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ninachotaka kuzungumzia ni kuhusu suala la miundombinu. Kuna Uwanja pale Ilembula unasahaulika. Kuna Uwanja wa Ndege unatakiwa kuboreshwa, mzuri tu na bahati nzuri tuna *Game Reserve* ile *Kipengule Game Reserve* na Mpanga *Game Reserve*. Ule Uwanja ukiboreshwa, unaweza ukasaidiana na Uwanja wa Mbeya wa Songwe, kukawa kuna hali nzuri kuliko kuhangaika kutumia gharama kubwa. Uwanja upo, unahitaji kukarabatiwa tu. Umeme upo jirani pale pale, kwa hiyo ni mambo mazuri. Ni Uwanja mkubwa sana.

Kingine ninataka nizungumzie kuhusu suala la Watumishi. Hawa Watumishi wa Serikali kwa kweli mishahara yao ni midogo sana na watumishi wengine katika sehemu mbali mbali. Mbaya zaidi nataka nizungumzie kuhusu yale makato. Wanasema, *pay as you earn*. Nikipiga hesabu na mimi kwa sababu nilikuwa mfanyakazi wa *CRDB*, nilikuwa nalipa. Nilikaa muda mrefu *CRDB*. Ile *pay as you earn* inayotozwa na *TRA* ni kubwa sana. Ukipiga hesabu ni kama asilimia 13.4. Sasa, unamkata mfanyakazi na unasema mshahara wake analalamika bado ni mdogo bado unakata. Kwa mfano, mtu analipwa Sh. 900,000/= tuchukulie mfano, mnakata Sh.200,000/=, *it's unfair*. Ninashauri kwamba Serikali Ingewezekana ile *pay as you earn* ilipwe kidogo.

Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana! *(Makofi)*

**MHE. BALOZI ABDI HASSAN MSHANGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Bajeti hizi mbili, Wizara ya Mipango na Uwezeshaji na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kukupongeza wewe, Mheshimiwa Spika na Wenyeviti wa Kamati za Bunge kwa kazi nzuri, kwa namna nzuri mnayoifanya ya kuendesha Bunge letu. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Waziri Mkuu - Mheshimiwa Edward Lowassa na Baraza la Mawaziri kwa kazi nzuri ambayo

wameifanya katika muda mfupi wa miezi sita. Matumaini ya wananchi ni makubwa sana. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nichukue nafasi hii kuwapongeza Waziri wa Mipango na Waziri wa Fedha kwa Bajeti nzuri. Niliwahi kufanya kazi katika Wizara hizo kwa miaka 20 katika nafasi ya kutayarisha Bajeti. Kwa kweli Bajeti sio jambo jepesi. Mahitaji ni makubwa na uwezo ni mdogo. Kwa hiyo, niwapongeze wataalam wote wa Wizara hizo na Wizara nyingine kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue pia nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wote wa Jimbo la Lushoto kwa kunichagua mimi kuwa Mbunge, Mbunge ninayekidhi viwango vya Ari Mpya, Kasi Mpya na Nguvu Mpya. Wameshuhudia kwamba ndani ya miezi minne, tumeweza kujenga Sekondari tano mpya na kuwezesha kuwapatia nafasi Kidato cha Kwanza wanafunzi wote. Nasema wote waliomaliza Darasa la Saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefarijika sana leo kumsikia Mheshimiwa Rais wa Ireland kwamba wao wamewekeza sana katika nguvu kazi ya elimu. Mtoto wangu wa mwisho alisoma kule kwa Dublin na kweli wenzetu mfumo wao ni mzuri na Mheshimiwa Waziri wa Elimu akipata nafasi, atembelee kule. Mtoto wangu alifika kule akiwa katoka Kidato cha Pili. Walipoona umri wake, walisema hapana. Huyu aingie moja kwa moja Kidato cha Nne na wana utaratibu wa kumpa masomo ya nyongeza na akafanya mtihani wa *Form Four* kule. Akafaulu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie kwanza hotuba ya Waziri wa Mipango. Sera za msingi za uchumi endelevu, nianze na eneo la kilimo Ibara ya 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri katika Ibara ya 50 anasema lengo hapa ni kuboresha upatikanaji wa chakula cha kutosha. Sasa, uzoefu umeonyesha kwamba kwa kutegemea jembe la mkono na *Peasant farming* itatuchukua muda mrefu sana. Wenzangu wachumi wanakubali kwamba bei ya vyakula inakuwa na athari kubwa sana katika *Exchange Rate* na katika Mfumko wa Bei. Mimi nilidhani, tuige mifano ya nchi nyingine zilizoendelea. Kule kwa wenzetu utakuta wanategemea zaidi mashamba makubwa ya kibiashara. Kama hatuendi huko, ama ya vikundi au vya watu wenye fedha. Lakini, kwa jembe la mkono, itatuchukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu hii inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Kikwete na Mheshimiwa Waziri Mkuu Edward Lowassa imetuonyesha kwamba tukijipanga, inawezekana. Serikali imejipanga katika suala la elimu. Waziri Mkuu ametuhamasisha na tumefanya maajabu katika muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi Waziri wa Afya alitutangazia azma ya Wizara yake ya kuwa na Kituo cha Afya katika Kila Kata na Zahanati katika kila Kijiji. Sasa mimi nadhani muda huu wa miezi sita ni mdogo na tusiitegemee Serikali kufanya miujiza. Lakini, nadhani katika Bajeti ijayo, hebu Serikali itafute uwezekano wa kuwa na Ari Mpya na Kasi Mpya katika Sekta ya Kilimo na hasa mashamba makubwa ya kibiashara.

Sisi kule Mkoa wa Tanga tumebinafsisha mashamba ya katani. Baadhi ya hayo ni mapori. Mashamba yale ni maeneo mazuri sana kwa kilimo cha mahindi. Wale waliopewa mashamba yale washauriwe walime mahindi kwa wingi kibiashara au mashamba yale wayaachie wapewe wengine ambao wangeweza kufanya kazi ile vizuri zaidi. Ninakwenda haraka haraka kwa sababu muda najua ni mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende sehemu ya maliasili, Ibara ya 65. Mheshimiwa Waziri wa Mipango anazungumza pale kuendeleza uhifadhi na uvunaji endelevu wa maliasili. Waheshimiwa Wabunge hapa wamesema na Mheshimiwa Kabuye, alisema itakuwa vigumu sana kwa kweli kuwaelekeza wananchi wetu wasitumie mkaa. Lakini tukichukua mfano wa nchi za Ulaya, nchi ya Ufaransa walikuta misitu imekwisha, wakaamua kupanda misitu. Wakaona kuhifadhi peke yake hakutoshi, kupanda mashamba makubwa ya misitu. Sasa hivi nadhani Ufaransa ni nchi ya tatu katika Ulaya ukiondoa Finland na Sweden kuwa na misitu mingi sana. Nchi yote ni misitu.

Sasa, nchi yetu sisi ina maeneo mengi ambayo mengine ardhi haifai kwa kilimo hasa maeneo ya milimani. Nadhani wakati umefika, tuwe na mpango kabambe wa kupanda miti kama wendawazimu. Hivi karibuni nilipokuwa kwenye Jimbo la Lushoto, kulikuwa na harambee fulani. Nikaona pale kulikuwa na akimama kumi waliokuwa wamebeba watoto wao wachanga migongoni, nikawaambia njooni. Nikasema watoto hawa mkiwapandia miti 100 kila mwaka, watakapokuwa wakubwa kwenda Sekondari watakuwa hawana shida na karo ya Shule. Kwa hiyo, mimi pale nikawafadhili wale kwa kuwaanzishia miti hamsini hamsini ili waendelee na utaratibu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tujipange kupanda mashamba makubwa ya miti ya Serikali, ya Halmashauri, ya Vijiji na ya mtu mmoja mmoja. Tukifika huko, hili suala la kusema mkaa itakuwa si tatizo kwa sababu watu watakuwa wanakata misitu ya kibiashara kwa lengo hilo. Nafahamu kwamba wenzetu kule Makete na kule Mkoa wa Iringa wanaendelea vizuri katika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Mazingira nadhani linafanana na hilo suala nililozungumza la misitu. Tukipanda miti kwa wingi na tukawa na mashamba makubwa ya kilimo, hasa mahindi na mpunga kwa vile ndiyo chakula kikubwa na haya mashamba yakafuata utaratibu mzuri wa kilimo cha kisasa na wananchi wakaelekezwa ilivyo, basi mimi nadhani tutaweza kupiga hatua nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala la Ubinafsishaji, Ibara ya 100. Ubinafsishaji huu, kuwawezesha Watanzania, mimi nadhani kwa kweli bado. Lakini, naipongeza sana Serikali kwa kufikiria suala zuri hili la kuwasaidia wananchi wazalendo kwa namna mbalimbali ili waweze kupata mitaji nao washiriki katika miradi mikubwa. Nchi nyingine wameweka sheria na sisi najua tunayo, lakini labda ni ya kuboresha kwamba Mgeni akiwekeza analazimika kwa asilimia fulani, *shareholding* iwe ya mwananchi. Nadhani huo utakuwa utaratibu mzuri wa kutuwezesha hatua kwa hatua kuweza kumiliki sehemu kubwa ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye hotuba ya Waziri wa Fedha. Kwanza nimpongeze sana kwa hotuba nzuri. Kwa muda mfupi aliokaa pale nadhani hiyo Wizara ameilelewa vizuri, kwa hiyo nampongeza sana. Kabla sijasahau niseme kwamba naunga mkono hoja zote mbili mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye malengo ya uchumi mapana. Pato la Taifa kukua kwa asilimia tano hadi tisa hadi asilimia saba, niseme kwamba hapa inabidi tuwe waangalifu sana ili tuwe na *remedial measures* katika maeneo ya chakula, umeme, bei ya mafuta. Hayo ndiyo maeneo ambayo yakisimamiwa vizuri , ujazi wa fedha utaweza ukapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende haraka haraka kwenye Ushuru wa Forodha. Kwanza niipongeze *TRA*, wamefanya kazi nzuri sana kukusanya mapato. Lakini mimi sina hakika ya msaada tunaopata wa Makampuni haya tuliyoajiri ya kufanya kazi kwa niaba au kama wakala wa *TRA*. Nchi nyingi hawatumii Makampuni haya. Mimi nadhani wakati umefika tuimarishe watu wetu wenyewe na Taasisi zetu. Huu utaratibu wa kuchukua Makampuni ya nje eti ndio wao wafanye tathmini ya thamani ya bidhaa zinazoingia, mimi binafsi siuamini kabisa. Tutapoteza pesa nyingi, tutawanyima watu wetu wa *TRA* fursa ya kujiamini. Mimi nadhani tutazame vizuri mikataba hii na ikiwezekana tuifute, tuimarishe watu wetu kwa kuwapa mafunzo ya ndani ana nje ili kazi hiyo ifanywe na watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu haraka haraka kwa kusema kwamba kwa kweli, hatukutarajia Serikali yetu hii ifanye mambo yote kwa miezi sita. Wamefanya vizuri, sasa la muhimu hapa tusaidiane na wananchi wetu ili hatimaye mwakani sasa tuweze kufanya tathmini nzuri, tuweze kuwa na Bajeti nzuri zaidi itakayokidhi malengo makubwa zaidi katika maeneo ya miundombinu, maji, huduma za afya na kuboresha elimu ya Kidato cha Tano na cha Sita, maana ukishapanua Elimu ya Msingi inabidi upanue Sekondari, ukipanua Sekondari inabidi upanue Elimu ya *A' Level* na Elimu ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kama nilivyosema, muda uliobaki hauwezi kumtosha Mheshimiwa mmoja kupata nafasi ya kuzungumza.

Waheshimiwa Wabunge, tunapokuwa wengi, lazima kuwe na utaratibu wa kufanya kazi. Sasa, napokea vi-*note* kwamba wapo Wabunge waliochangia kwa Wizara hizi mbili, wanataka tena wachangie kwa Waziri Mkuu. Sasa, sisi tunasema hivi Kanuni 49(2), kwamba: "Endapo maombi ya kuchangia katika hoja fulani yatakuwa mengi zaidi kuliko muda uliotengwa wa kujadili hoja hiyo, Spika atazingatia kigezo kwamba Wabunge ambao bado hawajachangia katika hoja zilizotangulia kujadiliwa katika Mkutano huo unaoendelea au waliochangia mara chache zaidi, wanapewa nafasi ya kwanza.? Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba wale waliochangia katika hotuba ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Fedha, hawatapewa kwa Waziri Mkuu kwa sababu mpaka

ninaposema sasa, kwa kesho tutakuwa na kipindi cha Maswali na Majibu mpaka saa nne. Tutakuwa na nafasi ya kuchangia Wabunge wengine tu kwa saa moja tu mpaka saa tano.

Kwa hiyo, maana yake ni kwamba tutakuwa na Wabunge wanne tu kati ya hao watakaokuwa wamebaki, Wabunge 23 hawatapata nafasi. Hilo la kwanza.

La pili ni utaratibu wa kuomba kuchangia kwenye makaratasi. Kuna watu wameandika barua kwa Spika, toka tunaanza Bunge hili kuchangia kwa Waziri Mkuu. Sasa zile Barua tuna-*discard* zote mpaka itakapotoka *Order Paper* halafu ukaona *subject* kwamba Wizara ya Waziri Mkuu itajadiliwa ndiyo mnapeleka barua. Kwa hiyo, hata hawa 23 wanaruhusiwa kuomba sio kwamba u-*take for granted* kwamba niliomba katika Wizara hizi mbili sasa sikupata nafasi, kwa hiyo, nahamishiwa kule, hatuhamishiwi *automatically*. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kuna wengine wameshaomba Wizara nyingine za baadaye, sasa haiwezekani. Kwa hiyo, mnapochukua *Order Paper* fungua mwisho wa *Order Paper* baada ya Maswali utakuta shughuli za siku hiyo zimepangwa. Andika fomu za kuomba kuchangia, sio vikaratasi tena. Tuna fomu zetu za kuomba kuchangia. Halafu pia anayekuta amekosa Wizara inayohusika kuna karatasi ndefu kubwa za kuchangia za maandishi. Kwa hiyo, Waziri ukimpa muda wa kutosha kwa maandiko ataweza kuingiza katika majibu yake.

Kwa hiyo, naomba utaratibu huu uzingatie vikaratasi vidogo vidogo vya kuomba kuchangia vya namna hii, havitakuwa vinapata heshima yake. Halafu mtakuwa mnaanza kuomba kuchangia baada ya *Order Paper*. Kwa hiyo, *Order Paper* ikitokea, soma mwishoni kwanza, baada ya maswali angalia shughuli gani zinafuata, ukiona hoja inayofuata omba kuchangia. Kwa hiyo, huo ndio utaratibu ambao uko kikanuni.

Kwa hiyo, nimeagizwa kutangaza kwamba kesho tutakuwa na Wabunge wachangiaji kutoka saa nne mpaka saa tano. Baada ya hapo kutoka saa tano mpaka saa sita, Serikali inaanza kujibu hoja. Wataanza Manaibu Mawaziri watatu, tutawapa dakika 20 kila mmoja. Kutoka saa sita mpaka saa saba Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ataendelea kujibu hoja. Tukirudi kipindi cha mchana saa 11.00 mpaka saa 12.00 Waziri wa Fedha atajibu hoja. Baada ya hapo, nawasihi kila Mbunge kesho awepo hapa kwa sababu tutaanza kupiga kura ya kutaja jina la Mbunge mmoja mmoja. Kwa hiyo, tutamaliza na tuko wengi, kwa hiyo, tunakadiria kwamba tutachukua zaidi ya saa moja kufanya kazi hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Katiba ya nchi, hiyo kazi ndiyo inafanyika.

Kwa hiyo, naomba mtu yoyote asipuuze, kama kuna wenzenu waliokuwa mbali huko muwaite, kama kuna wengine muwaarifu kwamba kesho tunahitajika kuwa wote hapa na itapigwa kengele kusudi wote wawepo humu ndani. Kwa hiyo, nategemea kwamba hilo mtalikumbuka.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kueleza hayo, sasa naomba kuahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.44 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa Tarehe 23 Juni, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*